ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/ Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
57.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 29 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 152

Uharibifu wa Mazingira katika Skuli ya Lumumba

Mhe. Nassor Salum Ali – Aliuliza:-

Kumekuwa na kilio kikubwa kutoka kwa uongozi wa Skuli ya Sekondari ya Lumumba juu ya uharibifu uliokithiri wa mazingira yanayozunguka Skuli hiyo yenye historia ya pekee hapa Zanzibar. Kuna taarifa kuwa uongozi wa skuli hiyo umechukua hatua mbali mbali kueleza tatizo hilo katika ofisi yako, lakini hadi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kuona uharibifu huo.

(a) Je, Wizara yako haioni kuwa kuendelea kuiacha hali hiyo ni kukaribisha janga la kimazingia kwenye eneo hilo?

(b) Kama Wizara ina mpango wa kuchukua hatua, ni lini tutarajie kupata ufumbuzi wa tatizo hili?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kwanza naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Ni kweli kwamba eneo la Skuli ya Sekondari ya Lumumba kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira kuzunguka skuli hiyo. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais iliarifiwa mwanzo mwa mwezi huu wa Juni, 2012 kwa taarifa isiyo rasmi. Hata hivyo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais iliizingatia taarifa hiyo na iliiagiza Idara ya Mazingira kufuatilia suala hili.

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imegundua kwamba mawasiliano ya awali yalifanywa kwa nyakati tofauti kwenda kwa Sheha wa Shehia ya Makadara, Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Mkuu wa Wilaya ya Mjini pamoja na Jeshi la Polisi kupitia kwa Mkuu wa Polisi (OCD) wa Wilaya ya Mjini na Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Makadara.

Madhumuni ya mawasiliano hayo ilikuwa ni kutoa taarifa juu ya tatizo liliopo, lakini zaidi ni kuomba ulinzi wa kukabiliana na hali iliopo. Wakati JKU waliushauri uongozi wa Skuli ya Lumumba kuwasiliana na Jeshi la Polisi. Jeshi hilo kupitia kwa Kamishna wake hapa Zanzibar liliahidi kulishughulikia tatizo hilo, ila liliutaka uongozi wa Skuli ya Lumumba kuwa na subira.

Baada ya muda kupita uongozi wa Skuli ya Lumumba umewasilisha maombi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupatiwa fedha ndani ya kipindi hiki cha bajeti, ili kuinusuru hali ya uharibifu wa mazingira iliopo skulini hapo. Uongozi wa skuli unaamini kuwa vijana ambao wanadaiwa kuvuta bangi ndio wanaofanya uharibifu huo wa kuchimba mchanga wakiwa na mapanga, pauro na mbwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 152 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inasikitishwa sana na hali hiyo, kwa sababu kuendelea kwake ni uharibifu mkubwa unaoweza kupelekea jangwa kwenye eneo hilo.

(b) Kwa hivi sasa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika kuratibu tatizo hili, inawasiliana na Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ili kulitafutia ufumbuzi suala hili. Hivi sasa eneo lililoharibiwa linashauriwa kupandwa miti ambayo hata hivyo itahitaji kupatiwa ulinzi wa usiku na mchana, ili ising'olewe na waharibifu hao.

Suala la msingi ni kwamba Jeshi la Polisi na Vikosi vya Ulinzi na Usalama kutoa ulinzi wa dhati, ili kulinusuru eneo hilo pamoja na Skuli ya Lumumba ambayo ni sehemu muhimu ya kuwapatia elimu vijana wetu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ni vyema Mhe. Mwakilishi wa jimbo pamoja na Waheshimiwa wengine wakishirikiana na Shehia ya Makadara kuweza kuhakikisha kwamba, kunakuwa na Kikosi cha Ulinzi Shirikishi, ambacho kitasaidia sana katika kutunza amani kwenye maeneo haya. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Wakati alipokuwa akijibu swali hili ameeleza na amekiri kwamba lipo tatizo katika skuli ile.

Je, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni lini hasa watashirikiana, ili kuweza kujenga uzio pamoja na kupanda miti katika skuli ile? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza kwamba ofisi yangu katika kuratibu suala hili inawasiliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, nia ni kuhakikisha kwamba maombi yaliyopelekwa na Skuli ya Lumumba yanazingatiwa na wizara, ili kuweza kupatiwa fedha kwa ajili kutunza eneo hilo. *(Makofi)*

Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, tunawasiliana na Idara ya Misitu ambayo ndiyo inayoandaa *operation* maalum ya kuweza kuwakamata hawa waharibifu wa mazingira ambao kwa sasa wameenea katika nchi yetu. Nadhani hili litakuwa ni muhimu sana pia tunahimiza kwamba Jeshi la Polisi pamoja na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kuweka ulinzi wa kutosha katika eneo hili kama ni sehemu muhimu sana ndani ya visiwa vyetu. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa kwa mintarafu ya kushughulikia shughuli zetu za kitaifa. Vile vile nikushukuru wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi hii.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amejibu vizuri tu. Lakini kutokana na historia ya skuli ile na kwa kuwa mambo mengi yanatendeka katika sehemu ile na wala si hilo tu, isipokuwa ni mambo mengi yanatendeka na mengine Mhe. Mwenyekiti samahani ya ufuska.

Je, atakubaliana na mimi kwamba kwa sababu si yeye peke yake kushirikiana na wizara husika na wala sio kujenga uzio na badala yake uwe kujenga ukuta? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba niuchukue ushauri wa Mhe. Mwakilishi, ili kwa pamoja tuweze kuufanyia kazi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na kama itawezekana kuweza kuangalia kwamba tunajenga ukuta huo kwa ajili ya kuweka ulinzi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri tena ni matamu sana kama asali.

(a) Mhe. Waziri unaonaje hivi sasa wizara yako ikajikita zaidi kwa hawa Polisi Jamii, na kuweza kuwatafutia fedha na kulinda eneo hilo?
(b) Nadhani si vyema kuwachukua Askari Polisi na kuwapa mzigo mkubwa wakati hivi sasa wao wanao ulinzi wa nchi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, wazo la Mhe. Mwakilishi ni zuri, lakini naomba afahamu kwamba kuna taasisi mbali mbali na kila taasisi ina majukumu yake. Kwa hivyo, suala zima la Ulinzi Shirikishi kwa maana ya Polisi Jamii liko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi. Kwa kweli ofisi yangu kupitia Idara ya Mazingira haina kifungu cha bajeti kwa ajili ya kusaidia vikosi hivyo katika kuchunga ulinzi wa maeneo yetu. *(Makofi)*

Nam. 118

Eneo la Kufanyia Biashara

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Hivi sasa wananchi wa Zanzibar wamekuwa wafanyabiashara hasa katika sehemu ya Darajani, ambayo sehemu hiyo imejaa na hata wananchi kupata usumbufu wa kukosewa na magari.
Je, kwa nini Serikali haiwatengei wananchi hawa eneo lililokabiliana Bwawani, ambalo lilikuwa likiwekewa makontena.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia vyombo vyake imetenga eneo la Saateni kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo kuendesha shughuli zao. Serikali inaendelea kuliendeleza eneo hilo kwa kuimarisha miundombinu na mahitaji mbali mbali yaliyo muhimu na yanayostahiki.

Serikali inatoa wito kwa wafanyabiashara wote ambao tayari walipatiwa maeneo katika eneo la Saateni na walikwenda kujenga vibanda vyao au meza zao za biashara, basi warejee katika sehemu hizo kufanya shughuli zao. Tumegundua kwamba msongamano anaousema Mhe. Mwakilishi Darajani ni wafanyabiashara wengi ambao hawako pale kihalali na nje ya taratibu, na tumejaribu sana kuwaomba na kuwanasihi, ili tufuate Taratibu za Mipango Miji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine ushauri alioutoa Mhe. Mwakilishi kwa eneo la Bwawani, naomba kumjuilisha kwamba serikali ina mipango mingine mikubwa ya kuliendeleza eneo la Bwawani. Kwa hivyo, kwa sasa haitakuwa vyema kuwatoa wafanyabiashara kule na kuwapeleka Bwawani. Ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa eneo la Saateni ni eneo kubwa, na kwa kuwa eneo lile lina matatizo ya kuwa na majambazi kidogo, ambao wanapora biashara pale. Vile vile Serikali ilikubaliana na wafanyabiashara wale kuwajengea uzio eneo lile. Je, serikali imefikia hatua gani katika suala hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwenye mchanganyiko mkubwa wa watu si sokoni tu, lakini sehemu nyingi sana hasa katika mji mambo ya udokozi, ubadhirifu huo wa kuwaibia wengine pamoja na uhuni upo. Lakini tutajitahidi kwa kushirikiana na walinzi wetu, Askari wa Manispaa pamoja na wenye maduka kwa umoja wao kulipiga vita suala hili.
Upande wa pili wa swali lako kuhusu uzio Mhe. Mjumbe nashukuru kwa kutukumbusha tutalifuatilia hilo na tuone linatekelezwa mara moja. Ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, nashukuru kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia mrundikano wa watu katika eneo la Darajani wakiwemo watalii. Mhe. Mwenyekiti, rasilimali watu ni bora zaidi kuliko mpango mwengine wowote ambao serikali inao ukitilia maanani huo mpango wanaotaka kufanya pale Bwawani.

Je, Mhe. Waziri anaweza kuwaeleza Wazanzibari ni mpango gani mkubwa unaoshinda rasilimali wao walionao ambao wanataka kuendeleza pale Bwawani? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, huo mpango ambao serikali inao, na kwa sababu kwa sasa ndio kwanza unatengenezwa, unajua kitu kama ndio na wazungu wanasema kwenye *pipe line*, basi si vizuri kukizungumza, ni vyema tuone hiyo mipango inavyotengenezwa na halafu pengine Mhe. Mwakilishi kwa uzoefu wako tunaweza kukushirikisha katika hiyo mipango.

Kwa hivyo, tusubiri kwanza mipango hiyo tuiandae na baadae kwa dhahiri tutakuja na mipango hiyo itawajumuisha watu wengi zaidi, na pengine watu wote wa Darajani watamezwa. Jambo la msingi ni kuomba salama hiyo mipango ile tu na tuombe Mungu. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali mama linasema kwamba sehemu ya Darajani imeshajaa kutokana na wafanyabiashara, na katika majibu ya swali mama Mhe. Waziri alisema kwamba eneo la Bwawani serikali ina mipango maalum. Je, Mhe. Waziri ni mipango gani hiyo ambayo serikali imekusudia kufanya katika eneo la Bwawani?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilieleza wakati nilipomjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, naomba kurejea tena kwamba pale Bwawani kuna mipango mikubwa ya kiserikali kwa ajili ya kupaendeleza. Sasa tukisema kupaendeleza ni mipango mingi sana kama vile kibiashara, majengo, lakini hivi sasa serikali ndio inapanga. Kwa hivyo, si vyema kuweza ku-*forecast* na hiyo mipango yenyewe iko wapi, basi vyema tusubiri itakapoiva na tutakushirikisheni Waheshimiwa na mtaambiwa wakati itakapoiva. *(Makofi)*

Nam. 53

Utafiti wa Utawala Bora

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Mapema mwaka jana, Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikishirikiana na Taasisi ya *International Law and Policy Institute (ILPI)* ya Norway ilifanya utafiti kuhusiana na Utawala Bora Zanzibar, utafiti ambao uliwahusisha pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(a) Je, utafiti huo ulikuja na matokeo yepi?

(b) Ni lini matokeo ya utafiti huo yatatolewa hadharani, ili wananchi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wajue hali halisi ya mtazamo wa wananchi kuhusiana na Utawala Bora nchini?

(c) Serikali imepanga kuchukua hatua gani katika kufanyia kazi matokeo ya utafiti huo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 53 lakini kabla kujibu swali hilo naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, mapema mwaka jana Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilipata udhamini kutoka Ubalozi wa Norway kwa ajili ya kufanya utafiti kuhusiana na utawala bora hapa Zanzibar. Kazi hiyo ilipewa Taasisi ijulikanayo *International Law and Policy Institute (ILPI)*, ambayo ni Taasisi isiyo ya Serikali kutoka Norway.

Mhe. Mwenyekiti, utafiti huu ulihusu utambuzi (*perception*) wa wananchi kuhusu masuala ya utawala bora. Kulikuwa na makundi matatu ya wananchi ambao walihusika katika kuulizwa au kuhojiwa. Makundi hayo ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Watumishi wa Umma na wananchi wa kawaida katika shehia mbali mbali za Unguja na Pemba. Mambo yaliyoulizwa au kujadiliwa katika utafiti huo yalikuwa ni utawala bora kwa jumla, rushwa na huduma za jamii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Matokeo ya utafiti huo yalionesha kwamba wananchi wengi hawajui misingi mikuu inayojenga utawala bora. Kuhusu rushwa utafiti uligundua kwamba wananchi wengi wanajua vyema maana ya rushwa na madhara yake.

(b) Matokeo hayo yatatolewa hadharani mara tu baada ya kukamilika hatua za upokeaji wa ripoti kutoka kwa watafiti, hasa baada ya kuziangalia na kukubaliana juu ya takwimu zilizotumika na maudhui ya ripoti. Ripoti ya awali iliwasilishwa katika Kikao cha Makatibu Wakuu na waligundua maeneo ambayo taarifa zake zimekosewa na kuelekeza kufanyika marekebisho. Kazi hiyo itakapokuwa tayari na kuridhiwa na kuidhinishwa na serikali, basi zitachapishwa rasmi na kupewa wananchi wote kwa jumla. *(Makofi)*

(c) Serikali kwa mujibu wa sera ya Utawala Bora itazitumia tafiti za utawala bora zinazofanywa na zitakazoendelea kufanywa katika kutayarisha Ripoti za mwaka za Utawala Bora. Aidha itatumia matokeo ya tafiti hizo kama ni taarifa za msingi (*base line information*) kwa tafiti zitakazofanywa siku zijazo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pia naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake fasaha na ya kina, naomba kumuuliza swali moja tu la nyongeza.

Zipo taarifa Mhe. Mwenyekiti, kwamba matokeo ya utafiti huu kama majibu ya Mhe. Waziri yalivyojionesha kwamba yamefika ngazi ya Makatibu Wakuu tu, na hadi hii leo hayajafika katika kikao ambacho ndicho chenye dhamana kwa mujibu wa Katiba yetu ya Masuala yote ya Sera, yaani Baraza la Mapinduzi.

Je, Mhe. Waziri anaweza kulithibitishia Baraza hili suala hilo na kama ni kweli sababu zipi zilizopelekea Makatibu Wakuu kukwamisha matokeo ya utafiti huu yasifike Baraza la Mapinduzi, ambao ndio wenye dhamana Kikatiba kwa Masuala yote ya Sera katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu mama kwamba ripoti ya utafiti huu ilifikishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu kama taratibu za serikali zinavyoelekeza kama ni Kamati ya Kitaalamu inayolishauri Baraza la Mapinduzi.

Baada ya kugundua ripoti hiyo ilirejeshwa kwa masawazisho. Mhe. Mwenyekiti, napenda kuishukuru Taasisi hii ya *ILPI* kwa uungwana wao wa kuweza kufanya marekebisho na kukubaliana na takwimu ambazo zimejengewa hoja na Makatibu Wakuu, na hivi sasa tayari taarifa hizo zimeshawasilishwa tena kwenye wizara yangu, ili hatua ya kuirejesha tena kwa Makatibu Wakuu ifanyike.

Kwa hivyo, baada ya hapo mara tu baada ya kurudi kwa Makatibu Wakuu, mimi kama Waziri mwenye dhamana nitaifikisha taarifa hii rasmi kwenye Kikao cha Baraza la Mapinduzi, ili iwe ni taarifa inayoweza kutumiwa na wananchi wa nchi hii rasmi. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake alisema kwamba ripoti hii itapitia kwa Makatibu Wakuu. Je, huoni kupitia kwa Makatibu Wakuu ripoti hii itanyima ule ukweli na uhalali wa ripoti wenyewe utakuwa haupo?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu waelewe tu kwamba huu utafiti uliofanywa, umefanywa kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu, na nchi hii inaongozwa kwa mujibu ya misingi ya sheria na Katiba.

Sasa kwa sababu taarifa hizi zinatakiwa serikali wakabidhiwe rasmi, na hii taasisi basi lazima zipite kwenye taratibu zinazohusika, Kamati ya Makatibu Wakuu ni Kamati ya Kitaalamu inayoishauri serikali juu ya mambo mbali mbali ambayo yanaletwa kwake na yanafanyiwa kazi.

Kwa hiyo, kwenda kwa Kamati ya Makatibu Wakuu sio kukwamisha makusudio ya ripoti hii, isipokuwa ni utaratibu tu ambao upo kiserikali, kwamba jambo lolote ambalo linataka kwenda kwenye Kikao cha Baraza la Mapinduzi, basi lazima lipite kwenye Kikao cha Makatibu Wakuu.

Lakini kama nilivyomjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba asiwe na wasi wasi kuhusu kukwamishwa, ripoti hii ipo na itakuwa wazi kama Sera ya Utawala Bora inavyoeleza. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kwenye jibu lake la msingi Mhe. Waziri amekiri kwamba katika utafiti huu ilionekana kuwa Wazanzibari hawajui lolote kuhusiana na mambo haya ya utawala bora, lakini wanajua kuhusu rushwa na madhara yake.

Kwa kuwa Zanzibar tayari tumeanzisha Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa kuendelea kucheleweshe taarifa hizi kutofika kwa wananchi si kuwafanya wananchi kukosa haki zao za msingi ikiwemo ile ya kupatiwa Vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba utafiti umeonesha kuwa wananchi wengi hawajui dhana ya utawala bora. Kutokana na hali hiyo, ndipo pale Serikali ikaja na mpango mzima kwanza wa kutengeneza Sera ya Utawala Bora. *(Makofi)*

Vile vile kama nilivyosema juzi kwamba vitabu na muongozo wa sera hiyo nitavigawa kuanzia kesho kutwa hapa Baraza la Wawakishi kwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiviona vile vitabu basi watawasaidia pia kuwafahamisha wananchi dhana ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ina mpango kabambe kabisa wa kuhakikisha kwamba elimu ya utawala bora inawafikia wananchi. Kwa msingi huo wa kuwa mpango huo tunao na tutahakikisha taaluma inatolewa. Sasa mwenye tatizo la vitambulisho, mwenye tatizo la *passport*, mwenye tatizo lolote lile, akishaelewa haki zake za msingi katika dhana nzima ya utawala bora kwa kufuata msingi ya katiba na sheria, mimi nadhani hilo litakuwa sio tatizo. Kwa hivyo, mheshimiwa aendelee kustahamili hatua kwa hatua tutaendelea kufanya hizi kazi ili wananchi wetu waweze kufaidika na dhana nzima hii ya utawala bora.

Nam. 67

Ujenzi wa Jengo Uwanja wa Ndege

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Jimbo la Muyuni):- Aliuliza:-

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar inaendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhi abiria katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, lakini kuna taarifa kuwa ujenzi umesimama kutokana na matatizo ya mkataba wa ujenzi wake.

(a) Je, taarifa hiyo ni kweli, kama sio kweli ni sababu gani zilizopelekea kukwama kwa mradi huo.

(b) Kuna taarifa kuwa awali mradi huo ulikuwa unagharimu dola za Marekani milioni 57, lakini inadaiwa mradi huo gharama zake zimeongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 70. Je ni sababu gani zimepelekea mkataba mmoja wa ujenzi kuwa na gharama mbili za ujenzi.

(c) Ni lini mradi huo utakuwa umekamilika na ramani za ujenzi wa jengo hilo zimezingatia vipi upatikanaji wa huduma zote muhimu ikiwemo suala la abiria kupanda ndani ya ndege bila kuroa wakati wa mvua na sehemu ya Ibada.

(c) Je, ni watu wangapi hadi sasa wamelipwa fidia kutokana na ujenzi wa uwanja wa ndege na wangapi hawajalipwa na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 67 lenye vifungu (a) (b) (c) na (d). Kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikubaliana na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd* ya China kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Zanzibar kwa mfumo wa usanifu na ujenzi (*design and build*). Katika mpango huu wa usanifu na ujenzi kazi ya usanifu huwa haikamiliki kwa wakati mmoja, kwa maana ya kuwa usanifu wa michoro unakuwa ni endelevu na kufanyika hatua kwa hatua.

Katika utekelezaji wa mradi huu, Kampuni ya BCEG ilitayarisha michoro ya awali ya jengo la abiria na kuiwasilisha kwa muajiri Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambapo Wizara kupitia mshauri wa Kampuni ya *Sir Fredrick Snow Ltd* ya Uingereza ilifanya mapitio ya michoro hiyo na kupendekeza kuwa ujenzi wa jengo la abiria na jengo la vifaa unaweza kuanza kutokana na michoro ya *structure* ya jengo hilo kufikia kiwango (*structural adequate*) na hivyo kuruhusu ujenzi huo uanze kwa hatua hiyo.

Hata hivyo, mshauri huyo alibainisha kuwa kuna mapungufu kadhaa katika usanifu wa ndani na jengo la abiria na ufinyu wa nafasi katika baadhi ya maeneo ya kutolea huduma, na hivyo kupendekeza kuwa kuna haja ya kufanya mabadiliko ya usanifu katika maeneo hayo wakati ujenzi unaendelea.

Wizara ilikubaliana na ushauri huo na kumtaka mjenzi kufanya mabadiliko ya usanifu wa ndani wa jengo la abiria kulingana na mapendekezo yaliyotolewa wakati ujenzi ukiendelea, aidha, kwa kuzingatia haja ya kuhudumia ndege kubwa zaidi Wizara pia ilimtaka mkandarasi kufanya mabadiliko ya mikonga ya kuhudumia ndege kubwa zaidi ya iliyopendekezwa katika mchoro wa awali.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vifungu a, b, c, na d kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo yangu yaliyotangulia ni dhahiri kuwa kusita kwa ujenzi wa jengo la abiria kumetokana na mchakato wa usanifu wa michoro ya jengo hilo la abiria, na hivyo pamoja na mapungufu ya mkataba kati ya Serikali na mjenzi na kutoa nafasi kwa mjenzi kufanya mabadiliko ya usanifu wa ndani ya jengo kama ilivyopendekezwa na muajiri kabla ya kuruhusu hatua nyengine za ujenzi wa ndani kuendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu awali ulikadiriwa kugharimu USD 57.5 milioni. Hata hivyo, Serikali iliona ni vyema kuongeza kiasi cha USD 12.9 milioni hadi kufikia USD 70.4 milioni ili kufanikisha upatikanaji wa vifaa na huduma muhimu katika jengo hilo ikiwa ni kuongeza huduma za lazima za kiwanja, ili kiwanja hicho kiweze kukidhi mahitaji na malengo ya Serikali.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mradi huu unatarajiwa kumalizika mwezi Januari 2014 na umezingatia takribani huduma zote muhimu za katika viwanja vya ndege vya kuweza kuwahudumia abiria, ndege na mizigo ikiwemo mikonga mikubwa pamoja na maeneo ya kufanyia ibada yaani misikiti.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani jumla ya wananchi 60 wamelipwa fidia kutokana na ujenzi huo na kiasi ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika katika kulipa fidia hiyo kutokana na uwezo wa Serikali kulipa hatua kwa hatua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri hayakidhi swali la msingi naomba kuuliza maswali madogo ya ziada.

Katika majibu yake Mhe. Waziri ulikiri kuwa Wizara ya Miundombinu imekubaliana maana ya kukubaliana kwa kusaini mkataba. Je, kati ya mchoro na mkataba kipi kimefanyika mwanzo kwa nini Serikali hawakuweza kuziona kasoro hizo. Je, si unataka kutwambia sawasawa kuku na yai kipi kilichokuja mwanzo.

Mkataba kusainiwa baada ya makubaliano inakuwaje mkataba mmoja kusainiwa mara mbili.

Kumbukumbu zinaonesha mikataba mingi ya airport inakuwa ya matatizo na mizengwe. Je, utakuwa uko tayari kuundwa Kamati Teule kufuatia kadhia hii, ili wananchi wapate kuelewa ukweli wa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti katika majibu mama tumeeleza wazi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia katika mkataba na kampuni ya BCEG. Na katika mkataba wetu huu ni mkataba wa usanifu na ujenzi yaani *design and build*. Na miongoni mwa mkataba kama huu wa *design and Build* ni kwamba mjenzi ana jukumu la ku-*design*, mwajiri kwa maana ya anaejengewa ana jukumu la ku- approve ile michoro baada ya kwisha kuridhika nayo ndio unamruhusu kwenda katika uendelezaji. Sasa katika msingi huu mwanzo unakuwepo mkataba, na huo mkataba ndio unaolinda huo utaratibu wa namna gani mnakwenda kufanya hiyo biashara ya kujengeana au jengine lolote ambalo mmekubaliana.

Kwa hivyo msingi ni kwamba tulikuwa tuna mkataba na mkataba upo, mkataba wenyewe unasema kwamba mjenzi ata-*design*, wajibu wa Serikali kama mwajiri kujiridhisha na michoro ataporidhika Serikali atamrejeshea mjenzi kama nimeridhika endelea na ujenzi. Ikiwa mjengewa kwa maana Serikali hajaridhika anamwambia fanya mabadiliko haya baada ya kufanya *consultation* anamrejeshea, baada ya kuridhika mara ya pili anarejeshewa ikiwa ameridhika ndio anapewa ruhusa ya kuendelea.

Jibu la (b) Mhe. Mwenyekiti nimeeleza kwamba Serikali imeingia mkataba wa milioni 57.5 baada ya kuona Serikali kuna haja ya kupata vifaa muhimu ikaongeza gharama dola milioni 12.9 mkataba ukawa gharama milioni 70.4. Na kilichochelewesha tumeeleza kwamba kulikuwa kuna mapungufu ya kisheria. Serikali imekaa na mjenzi kwa kupitia mkataba huu tumeshapitia kisheria na tumeridhika kwa mujibu wa taratibu baada ya kuwa na *addendum*, na hivyo sasa hivi kuna mkataba mmoja mkataba uliopo wa Serikali ni mmoja wa milioni 70.4 ndio unaojengwa na ndio unaotekelezwa.

Jibu (c) Mhe. Mwenyekiti maamuzi ya Kamati Teule nafikiri yatakuwa kwako wewe sina jukumu la kuyajibu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri alikiri kwamba katika hatua za kutiliana mkataba kuna hatua ya *approval* ambayo hufanywa na Serikali, na bila shaka jengo hili lilianza baada ya Serikali kuridhia hiyo *design* yenyewe iliyoletwa na mtaalam. Kwa kuwa jengo limeanza na limefikia hatua baadae Serikali ikagundua kwamba mkataba umekosewa, atakubaliana nami kwamba Wizara yake na wataalam wake wazembe na wameingiza Serikali hasara.

(b) Katika hatua ya mwanzo Wazanzibari walipata taarifa kwamba mikonga ya kuteremkia abiria ingekuwa minne, hivi sasa kuna mikonga mitatu, je ni haya makosa ambayo Mhe. Waziri amezungumza, lakini sisi hebu atwambie Mhe. Waziri kwa nini kila mradi ambao Wizara yake inaanzisha ikiwa barabara ya Mtoni/Darajabovu kunakuwa na *delaying* ni uzembe wa nani ni wa wataalam au wa Wizara yake kwa jumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti tumeeleza kwamba utaratibu wa mkataba huu, ulikuwa ni *design and build*, na tulichosema kwamba baada ya kuletewa ule mchoro sisi pamoja na mshauri wetu, mshauri wetu alichotushauri kwamba katika *structure* ile ya nje ameridhika nayo na Serikali ikawa

imeridhika. Lakini maoni yake mshauri kwamba ndani *internal structure* eneo ni dogo ni vyema tukafanyia tena *modification* na hicho ndicho kilichofanya tukachelewa.

Sasa hapa kilichopo hakuna uzembe wala wataalam hawajapotosha, maana kilichopo ujenzi wa lile jengo mnatengeneza *structure* baadae ndani mnafanya *partition.* Sasa mle ndani namna ambavyo wame-design mwanzo ndivyo mshauri akatwambia eneo litakuwa finyu, ni vyema mkamwambia mjenzi wenu akaendelea kufanya *modification* tena kuongeza eneo litakalokidhi mahitaji. Na hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hivyo katika kufanya utaratibu huu hakuna sehemu ambayo wataalam wetu wametupotosha au wamefanya uzembe. Sisi kama Serikali tumeridhika kwamba kazi waliyoifanya ya kutushauri imekwenda vizuri.

Jibu (b) Mhe. Mwenyekiti miongoni mwa hayo mabadiliko ni kwamba katika ule ujenzi wa mwanzo kulingana na ule mchoro tungeweza kupata kweli mikonga minne lakini *type* (b) ni hizi *precision* ndege ndogo azma ya Serikali ni kuhudumia ndege kubwa tunataka kwenda kwenye hatua kubwa, illi tuweze kwenye hatua hiyo lazima mikonga ibadilike. Na kila mkonga mmoja una gharama yake. Sasa mikonga minne midogo haiwezi kuwa gharama sawa na mikonga mitatu mikubwa. Hii ndio iliopo tunakubaliana nacho kwamba tunaondoa mikonga minne type (b) tunakwenda kwenye mikonga miwili mikubwa ya type (e) na *foundation* moja. Haya ni makubaliano kwa kutambua kwamba manufaa na shufaa tunayoitaka ndipo tutakapofikia, tunataka uwanja wetu uwe wa kimataifa. Hatuwezi kuwa na uwanja wa kimataifa ikiwa unahudumia ndege ndogo hauna uwezo wa kuhudumia ndege kubwa.

Matumaini yetu kwamba *type* (e) ikikamilika mikonga hii itaweza kukidhi kutoa huduma kubwa zinazoweza kukidhi ndege kubwa zilioko duniani.

Jibu (d) Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba kuna baadhi ya miradi yetu inachelewa, lakini changamoto ziko nyingi likiwepo suala la fedha sio wataalam tu wa Wizara yetu. Sisi kama Wizara tunajipanga vizuri sana mipango yetu inakuwa mizuri kinachotukwamisha ni fedha. Mimi naamini mchakato uliopo kwetu uko katika Serikali nzima kama Serikali yetu ingekuwa na fedha za kutosha siamini kama kuna mradi utakaochelewa. Azma ya mradi wetu wa barabara ya Amani tumeshatangaza kwamba mategemeo yetu fedha kutoka mfuko wa barabara tutakamilisha katika mwaka huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kufafanua zaidi majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wangu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nilitegemea kwa hatua hii ambayo Serikali imechukua basi badala labda Serikali au Wizara kushtumiwa uzembe ingesifiwa kwa umakini wake. Serikali inajenga kitu ambacho inahitaji, suala la *design and build* ni *system* duniani iko kote ina masharti yake. Na kama alivyoeleza Naibu Waziri una-*design* anaetaka kujengewa ana-*approve* au anasema hapana fanya hivi mkishakubaliana ndio anajenga na haya haongezi gharama. Suala la mikonga hakika kwamba sasa tunakwenda kwenye *generation* nyengine, lazima tuhakikishe *run way* yetu ni kubwa sana kwa Afrika Mashariki ziweze kutua ndege kubwa. *Boeing* au *Air bus 3* kwa mikonga ya *class b* au *category b* madege hayo hata yangetua ingebidi watu wachukuliwe uwanjani kwa mabasi.

Kwa kuwa na *category e* madege hayo yatatua watu wataingia kupitia mikonga na watatoka kwenye ndege kupitia mikonga na madege makubwa hayatakuwa na *restriction* ya kuja hapa kama ambavyo sasa hivi *restriction* hiyo ipo hakuna mikonga hiyo. Kwa hivyo mimi ninafikiri Waheshimiwa Wawakilishi wangethubutu kabisa wakasifu umakini wa Serikali katika hili. Na nyongeza ya 12.9 ni nyongeza kutokana na matakwa ya Serikali, kwamba *original drawing* ni hizi lakini sisi tungehitaji hiki na hiki na hiki. Na hatua hii Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe inaendelea, kila tunapoona kwamba tukiongeza hiki itavutia zaidi basi Serikali itafanya maamuzi hayo. Na kwa taarifa yenu tayari Serikali imeshafanya maamuzi mengine ya kuongeza ili kufikia kiwango ambacho Serikali na wananchi wa Zanzibar wataridhika kwamba jengo hili ni jengo la kisasa na kila mtu anaridhika na wadau katika wasafiri wa anga nao wataridhika.

Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nifafanue hayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Kutokana na majibu yanayotolewa na Naibu Waziri na Waziri kwa majibu wa nyongeza inazidi kuthibitisha kwamba Serikali ilikuwa haijui inataka nini, na kila siku inabadilisha mipango yake. Sasa nilikuwa nataka kujua tu kutokana na maelezo yaliyotolewa na Waziri na Naibu wake Baraza hili likithibitisha

kwamba taarifa hizi si za kweli kumepitikana uzembe na hata ukiukwaji wa taratibu. Je, Uongozi wa kisiasa wa Wizara hii utakubali kujiuzulu mbele ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa Mhe. Waziri ameomba urudie swali lako.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nasema kutokana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri na Waziri kwamba ndani ya miaka tatu hii tangu mradi huu umeanza kila siku yanatokea mabadiliko inathibitisha kwamba Serikali haina mipango wala haijui inachokitaka katika miradi yake. Na kutokana na majibu haya ikiwa Baraza hili litathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapa si za kweli, na kwamba kulikuwa na uzembe lakini hata ukiukwaji wa taratibu katika ku-*sign* mikataba hii miwili iliyopelekea matatizo haya na kuitia hasara Serikali. Je likithibitishwa hilo na Baraza hili Uongozi wa kisiasa wa Wizara hii uko tayari kuwajibika kwa kujiuzulu na kubeba jukumu la majibu haya.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru sana Mhe. Jussa kwa swali pamoja na ushauri. Mhe. Mwenyekiti inaonekana *concept* ya *design and build* wengi hawajaifahamu. Suala la mapungufu katika mkataba tumesema ni miongoni mwa vitu ambavyo vipo, na ni mapungufu hayo ambayo Serikali iliyo makini imekaa kitako ili mapungufu hayo kuyasawazisha. Kwa hivyo si suala la uzembe hatungeweza kuendelea na jengo lile wakati huku tuna mambo chungu nzima ambayo hatujaweka sawa.

Kilichofanyika, kwanza jengo halijasimama nasema limesita, na wakati wowote baada ya makubaliano haya ambayo yamerekebishwa mjenzi BCG ataendelea kujenga jengo letu kwa mujibu wa *system* hiyo ya design and build. Kwa hivyo si suala la uzembe wa Serikali au ya Wizara au wataalamu ni suala system yenyewe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawajaielewa vizuri labda tungemleta mtaalamu hapa akaeleza vizuri maana system ya *design and build* na ikiwezekana hata huo mkataba ulivyoandikwa.

Kwa hivyo si suala la kuwa kuna uzembe mtu ajiuzulu au vipi. Mimi ninafikiri hii system watu hawajaifahamu, wakielewa vizuri na umakini wa Serikali yenyewe katika suala hili, hili suala wala lisingefika hapo.

Mhe. Mwenyekiti huo ndio ufafanuzi wangu.

Nam. 121

Changamoto zinazoikabili Skuli ya Ufundi Kengeja

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 128

Usafirishaji wa Wagonjwa nje ya Nchi

Mh. Bikame Yussuf Hamad: Aliuliza;

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya huwa inapeleka wagonjwa nje ya nchi kila mwaka kwa matibabu.

a) Je, Serikali hutumia utaratibu gani ambao uko wazi na hauna upendeleo wa kuchagua na kupitisha wagonjwa hao wanaopelekwa nje kwa matibabu.

b) Je, fedha za wagonjwa wanaopelekwa nje bajeti yake hutengwa kwenye bajeti ya Wizara gani na kwa mwaka 2011/2012 zimetengwa kiasi gani.

c) Je, ni wagonjwa wangapi wamepelekwa nje ya nchi kwa kupata matibabu zaidi katika mwaka huo wa fedha.

Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 128 lenye vifungu (a), (b), (c) kama ifuatavyo:-
Mhe. Mwenyekiti Serikali kupitia Wizara ya Afya huwapeleka wagonjwa nje ya nchi unatumiwa utaratibu ufuatao.

a) Mgonjwa kwanza huchunguzwa katika hospitali za hapa Zanzibar na hutibiwa kama tatizo lake linawezekana. Pale ambapo daktari katika uchunguzi wake au baada ya kumtibu na akiona kuwa hakuna maendeleo mazuri ya kiafya, mgonjwa huyo humuandikia ripoti ambayo hupelekwa kwenye bodi ya madaktari. Bodi ya madaktari hupitia ripoti na kuangalia hali ya mgonjwa na kutathminini hatimae hutoa maamuzi wapi apelekwe.

b) Mhe. Mwenyekiti, fedha zinzotumika kwa wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi zinatokana na Bajeti ya Wizara ya Afya, na kwa mwaka 2011/2012 Jumla ya shilingi 11,000,000 zilitengwa kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.

c) Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 jumla 116 walipelekwa kutibiwa nje. Wanawake 46, wanaume 51 na watoto 19.

Nam. 145

Kubakwa kwa mtoto mlemavu

Mhe. Asha Bakari Makame (Kny. Mhe. Mgeni Hassan Juma): Aliuliza:

Gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 14 Machi 2012 lilitoa taarifa ya kubakwa kwa mtoto mlemavu na kupewa ujauzito ambapo mpaka hii leo bado haki haijatendeka, ingawa wazazi wa mtoto huyo wameripoti katika vyombo mbali mbali vya sheri.

a) Je, Wizara yako inayo taarifa ya tukio hili.
b) Kama inayo taarifa hiyo imechukua hatua gani.
c) Kutokana na uzoefu wa Wizara yako katika masuala kama haya, wapi huwa kuna kikwazo kinachosababisha kesi hizi kuchelewa kuhukumiwa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Alijibu:
Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 145 lenye kifungu (a), (b) ns (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na Wizara inayo taarifa za kutosha juu ya tukio hilo.

b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefuatilia kesi hiyo kupitia kituo cha Mkono kwa Mkono pamoja na Kituo cha Polisi Mazizini na mtuhumiwa tayari ameshachukuliwa damu kwa ajili ya kipimo cha D.N.A. na kwa utaratibu wa Mahkama kesi hutajwa mara tatu, na endapo ushahidi haukukamilika inapelekea kesi kufutwa. Kwa kuondoa utata huo wa kufutwa kwa kesi ndio maana suala hili bado lipo chini ya Kituo cha Polisi Mazizini kwa kusubiri majibu ya kipimo cha D.N.A. ili kukamilisha ushahidi na kupelekwa mahakamani.

c) Mhe. Mwenyekiti Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto masuala yanayokwaza kesi hizi kuchelewa kuhukumiwa ni kutokana na sababu zifuatazo:-

- Mashirikiano madogo kwa jamii katika suala zima la kutoa ushahidi mahakamani.
- Upelelezi wa Polisi kuchukua muda mrefu kutokana na mashirikiano madogo na jamii.
- Kesi zinazofika mahakamani huchukua muda mrefu kusikilizwa hadi kufikia kutolewa hukumu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini je atakubaliana nami kwamba uzembe unaohusiana na mambo haya hufanywa kwa makusudi, ili ushahidi upotee. Na

kama ushahidi unapotea atakubaliana nami Mhe. Waziri kwamba Wizara yake ina wajibu wa kukata rufaa na kuhakikisha kwamba wanaofanya uzembe huu wanachukuliwa hatua.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kumjibu Mhe. Asha Bakari rafiki yangu, shoga yangu ingawaje siku moja alisema sina ushoga mimi kwenye mambo ya kazi. Lakini naomba niseme kwamba ninakubaliana na yeye na yote aliyonambia, na kwa kweli sisi Wizara wakati mwengine huwa tunakata rufaa kwa kesi zilizowazi ambazo bado hazihukumiwi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kumuuliza Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mtoto yule hakuwa na nia ya kuwa na mtoto mwenzake kipindi hiki. Na kwa kuwa wazee wa mtoto yule hali yao ni duni. Je, Wizara yako na Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais ambayo inasimamia haki za watoto walemavu, mnamsaidiaje mtoto yule kukimu mahitajhi ya mtoto aliyezalishwa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Wanu wa Nafasi za Wanawake kupitia vijana kama hivi ifuatavyo:-

Si jambo baya kushirikiana na Wizara ya Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya jambo hili kwa sababu yule mtoto ni mlemavu kwa hivyo tutashirikiana vya kutosha ili tuhakikishe jambo hili linafanikiwa.

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri katika majibu yake mama amesema kwamba kesi haijapelekwa Mahakamani kwa sababu ya kusibiri majibu ya kipimo cha *DNA.* Na kwa kuwa kipimo cha *DNA* bado hapa Zanzíbar hatuna na ndio maana kesi nyingi zinachelewa kuamuliwa kutokana na kipimo hiki kuwa hatuna na kesi zinapotokea kipimo kinapelekwa Bara na kusubiri matokeo. Je, Mhe. Waziri wizara yako itasaidia vipi kupatikana kwa mashine hii.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, (Mhe. Mgeni Hassan Juma) bado wizara yangu au wizara ya serikali inahangaika kutafuta kipimo hiki cha *DNA*, lakini bado hatujafanikiwa kwa hivyo tusubirini kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya waziri wetu napenda kuchangia kuhusu suala hili. Inaonekana si wananchi, si viongozi hatusikilizi taarifa za habari wala hatuangalii, ni juzi tu na jana vyombo vya habari, magazetivimeandika kwamba kipimo cha *DNA* karibu kitafanyika Zanzíbar kwa sababu mwezi ujao mashine zinakuja.

Nam. 162

Ukiukwaji wa Haki na Sheria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa mujibu wa Sheria kama haki yake akiona imenyongwa au kunyimwa au Sheria kuvunjwa mtu huyo anatakiwa kwenda Mahakamani kupata haki yake au maelekezo kuwa Sheria ifuatwe kwa upande mwengine *ZFA* ambao wanasimamia Sheria za Michezo wanapoona kuwa haki yake amenyimwa mtu huyo akienda *ZFA* amejifukuza mwenyewe.

(a) Je, Mhe. Waziri, *ZFA* hawaoni kitendo hicho ni kwenda kinyume na utaratibu wa kisheria.

(b) Kuna sababu gani za kutisha watu kwa mujibu wa Sheria, kama *ZFA* mambo wanayofanya majukumu yao kwa mujibu wa Sheria kuna sababu gani ya kuwatisha watu wasiende Mahakamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 162 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kulijibu swali hilo napenda kwanza kutoa maelezo yanayohusiana na utaratibu na maelekezo ya Shirika la Soka Duniani (*FIFA*). Mhe. Mwenyekiti, chini ya utaratibu wa shirika hilo ni marufuku mambo yanayohusu mpira wa miguu kwenda Mahakamani. Utaratibu huo hauna maana kwamba vyama au vilabu haviwezi kutafuta haki Mahakamani, lakini zitakapofanya hivyo ni kuifanya *FIFA* kuchukua hatua kali kwa chama kinachosimamia soka cha nchini ikiwa ni pamoja na kufutwa kabisa katika uanachama wa *FIFA*. Mhe. Mwenyekiti, chini ya utaratibu huo kumewekwa kamati ya usuluhishi na ya rufaa kuwa ndizo zinazotakiwa kutatua matatizo ya soka. Endapo uamuzi wa kamati hizo hautoridhisha, walalamikaji wanatakiwa kuwasilisha madai yao kwenye Mahakama ya mambo ya soka ya *FIFA* iliyoko nchini Switzaland.

Baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Chama cha Soka cha Zanzibar (*ZFA*) kuzizuia timu kwenda Mahakamani si kwenda kinyume na taratibu za kisharia za chama hicho.

b) Mhe. Mwenyekiti, sababu ya *ZFA* kuvikataza vilabu visiende Mahakamani hakuna nia ya kutisha watu, lakini ni kujikinga na kuiepusha Tanzania na adhabu ya kufutwa uanachama wao wa *FIFA* na pia kuepuka Zanzibar kuwa ni kigezo cha kuvunja taratibu za *FIFA* wakati bado tunaendelea kupigania kuomba kuwa mwanachama wa shirikisho hilo la soka duniani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa masikitiko makubwa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami Juni mwaka jana *FIFA* imetupia mbali maombi ya Zanzibar kujiunga na *FIFA* kutokana na kukosa sifa kuwa Zanzibar imejiunga na Jamhuri ya Muungano, leo unakuja kutwambia Mhe. Naibu Waziri tunafuata *FIFA* sheria hiyo iko wapi ya *FIFA*?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba mwezi wa Juni, 2011 Chama cha Mpira wa Miguu Duniani *FIFA* ilisema kwamba maombi ya *ZFA* kutaka kujiunga na shirikisho hilo hayakukubaliwa. Lakini naomba nimwambie kwamba, juhudi hizo zilichukua muda wa miaka karibu 10 na sisi Zanzíbar kama nchi tunahisi bado kwamba juhudi zinaweza zikachukuliwa zaidi kupeleka upya maombi yetu na taratibu hizo tunazizingatia zaidi.

Lakini kuhusu suala la msingi ambalo aliliuliza kuhusu vilabu vya mchezo wa mpira wa miguu kwenda Mahakamani ni kwamba *ZFA* wanachama wake ni vilabu vya michezo wa mpira wa miguu ambavyo vimeunda katiba yao, katiba yao ya *ZFA* ambayo imeundwa na vilabu vyenyewe vya mpira wa miguu ikiwemo hiyo Malindi ambayo ameizungumza, ndio ambayo kwa pamoja wamekubaliana kuwa Katiba ya *ZFA* isiruhusu migogoro na mivutano inayohusiana na mpira wa miguu kwenda Mahakamani, kwa hiyo, ni katiba yao wenyewe.

Lakini pia tusisahau kwamba Zanzíbar kupitia *ZFA* pia ni mwanachama wa *SECAFA* na mwanachama wa *CAF* ile ya Afrika ambayo yote hairuhusu kabisa migogoro ya mipira ya miguu kuamuliwa Mahakamani. Kwa hivyo, kimsingi ni Katiba ya *ZFA* Ambato vilabu vyetu vya Zanzíbar vimekubaliana kuiunda yenyewe. Sasa ni muhimu kwa vilabu vya mpira wa miguu vya Zanzíbar kuheshimu katiba yao, kama wameona kwamba hicho kipengele kinakwenda kinyume na *interest* zao basi wakutane wakibadilishe, lakini kwa hivi sasa kwa vile ndio katiba inayoongoza mpira wa miguu lazima iheshimiwe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kama ilivyoelezwa mwanzo kwamba Zanzíbar si mwanachama wa *FIFA* na kwa kuwa Mahakama tayari imeshaamua kwamba Malindi irudi kwenye daraja la kwanza na kwa kuwa kesho tu *ZFA* wanachagua rais wao. Je, isingekuwa vyema hii amri ya Mahakama ikafuatwa kusudi akikaa Rais wa *ZFA* haya mambo yameshakamilika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, uamuzi wa Mahakama katika nchi yoyote ile ndio **supreme** sasa sisi kama wizara ambao tunaisimamia *ZFA* hatuwezi kwamba Mahakama ishatoa uamuzi wake basi tukapingana na uamuzi wa Mahakama itakuwa si utaratibu mzuri. Hiyo ni kinyume na utawala bora ambao Mhe. Waziri yupo pale na ambapo tumekubaliana kuwa nchi yetu inau-*observe*. Sasa Mahakama imetoa uamuzi wake na *ZFA* kupitia wizara yetu tunauzingatia.

Nam. 117

Migogoro ya Ardhi Zanzibar

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa hapa Zanzibar kumekuwa na mgogoro wa ardhi ambao wananchi kunyang'anywa sehemu ya ardhi yao na watu wenye uwezo wa fedha au kwa uwezo wa madaraka.

(a) Je, serikali inawajuwa wananchi wangapi walionyang'anywa ardhi zao.

(b) Kama inawajua imechukuwa hatua gani ya kurekebisha tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Ahsante Mhe. Mwenyekiti**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 117 lenye vifungu a na b kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake naomba kutoa ufafanuzi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi wa visiwa vya Zanzibar mara nyingi wamekuwa wakivamia maeneo na kuanzisha ujenzi bila ya kufuata Sheria ya Taasisi husika ya Ardhi. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ndio yenye Mamlaka ya kutoa umiliki wa ardhi kwa mtu/Watu au taasisi nyengine.

Baada ya ufafanuzi huo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali hainyang'anyi ardhi za wananchi wake kwa kuwa wananchi wengi wa Zanzibar wamejenga mazoea ya kutofuata Sheria na Taratibu za Ardhi na ikitokezea mwananchi kukiuka mwongozo wa upewaji wa haki ya matumizi ya ardhi (*Conditions*) au kuvamia ardhi na kuanzisha ujenzi kinyume na taratibu ndipo serikali huchukua hatua ya kuzuia ujenzi huo na kufuta hati ya umiliki huo na ndipo hapo wananchi huona wananyang'anywa ardhi zao na serikali.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Je, anakubaliana nami kwamba migogoro hii bado ipo na itamalizika lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakiri kwamba migogoro ya ardhi ipo na kama alivyozungumza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika hotuba yake juzi kwamba, serikali inajiandaa rasmi kuyashughulikia masuala haya na kuyapatia ufumbuzi. Na ni kweli kwa kuonesha moyo wa serikali wa wananchi wake kulikuwa na eneo katika kijiji cha Nungwi ambacho kilikuwa kinataka kujengwa Ikulu, lakini baada ya kukosekana tu ujenzi huo eneo hilo lilivamiwa na wajanja. Kwa hivyo, eneo hilo rasmi limerejeshwa na serikali katika kipindi cha wiki ya nyuma iliyopita. Huo ni muongozo au mwelekeo wa serikali kuyashughulikia matatizo ya aina hii.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika swali lake kuu amesema kuwa si kweli serikali hakuna mtu iliyomnyang'anya viwanja. Je, Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kuna mwananchi katika maafisa wako mwenyewe wamemnyang'anya hati na hati ile wakaichukua wakenda wakamuuzia tajiri.

Kama ni kweli uko tayari kumrejeshea hati yake huyu mwananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ieleweke kufanya kazi serikalini si sababu inayosababisha kunyang'anya ardhi ikisha ikasingiziwa serikali. Hilo kwanza lieleweke. Isitoshe kwamba wapo kweli baadhi ya watendaji ambao hushirikiana na wajanja lakini hawa serikali kwa nguvu zake na kwa kuyafuatilia masuala haya basi itajitahidi kufanya uchunguzi na yule yeyote atayekwenda kinyume na utaratibu basi serikali ina misingi yake ya kuchukua hatua kwa mfanyakazi ambaye anakwenda kinyume na utendaji na utaratibu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 37 ningemuomba Mhe. Naibu Waziri wangu anijibu vizuri lile swali ambalo nimemuuliza. Nilichomwambia kuwa katika jibu lake alisema kuwa serikali haimnyang'anyi mtu ardhi, lakini mimi nikamwambia kuwa wapo mafisa wake watendaji ambao tayari wamemnyang'anya mwananchi hati yake na mpaka leo anadai hajarejeshewa. Je, yuko tayari kama hili suala kulifuatilia na kurejeshewa hati yake yule mwananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi naomba kuongezea swali la nyongeza alilouliza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Makame Mshimba kwa kusimamia haki za wananchi wetu na hiyo ndio wajibu wa kila mwakilishi. Nataka nimhakikishie kwamba serikali situ zote itachukua kila hatua kuhakikisha kwamba haki za wananchi wake zinalindwa, na pale watendaji wa serikali wanapokwenda kinyume na taratibu zilizowekwa za kisheria basi serikali itachukua hatua kali hasa kwenye masuala haya ya ardhi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe tushirikiane alete vielelezo vinavyothibitisha kwamba wananchi wamenyang'anywa haki yao kwa kutumia fursa walizonazo watendaji wetu ili jambo hilo tulishughulikie na tulikomeshe mara moja. Mambo haya hayatakiwi yaonekane yakifanyika kwa kudhulumiwa wananchi wetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti,

Nam. 86

Elimu ya Mabadiliko ya Miongo kwa Wakulima

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza:-

Mhe. Waziri alipokuwa anajibu miongoni mwa masuala ya Wajumbe katika Mkutano uliopita alisema kuwa wananchi wetu wana haraka ya kulima wakati miongo inabadilika.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako imechukua hatua gani katika kuwaelimisha wananchi juu ya suala zima la mabadiliko ya miongo.

(b) Kwa kuwa wakulima wamekuwa ni wengi na matrekta ni kidogo na hivyo kupelekea wakulima hao kuchelewa kulimiwa mashamba yao. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuongeza zaidi matrekta ili kuwaondolea wakulima tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 86 lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili imekuwa ikifuatilia kwa karibu taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania kwa lengo la kuwapatia taaluma na ushauri wakulima kabla ya kuanza kwa msimu wa kilimo juu ya mazao gani na muda gani wapandaji kwa mujibu wa hali halisi ya hewa inayokadiriwa.
Taarifa hizi hutolewa kwa wakulima kupitia mfumo wa utoaji elimu kwa wakulima katika ngazi za Mkoa, Wilaya na Shehia, kwenye Mabaraza ya Wakulima yaliyoanzishwa na kuwezeshwa kielimu na vifaa katika kila Wilaya, kwenye Skuli za Wakulima na kupitia taarifa maalumu zinazoandaliwa na kutolewa katika Jarida la Kilimo linatolewa kila miezi mitatu na katika vyombo vya habari.

b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wakulima wengi wamejitolea kutaka wapate huduma ya kulimiwa kwa matrekta mwaka huu ili kuwahi wakati, hali ambayo imepelekea katika baadhi ya maeneo huduma hii kuchelewa kuwafikia wakulima hao kutokana na uchache wa matrekta tuliyonayo. Katika kukabiliana na

hali hiyo, wizara katika msimu huu ililazimika kununua matrekta 10 mapya kutoka SUMA-JKT ili kuongeza nguvu na imejipanga kununua matrekta mengine 20 na zana za kupandia mpunga (*Planters*) 30 kabla ya kuanza msimu ujao, ili kuongeza ufanisi wa huduma za matrekta na zana za kilimo kwa kuwahudumia wakulima kwa wakati. Aidha, sambamba na matrekta hayo, zana za kupandia mpunga napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza lako kuwa wizara tayari imeshanunua zana za kuvunia mpunga (*Combine harvesters*) 14 kutoka China ambazo zitawasili hapa nchini mwanzoni mwa mwezi wa Julai na zitaweza kutoa huduma za kuvuna mpunga katika msimu wa kilimo.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali hili alisema kweli huduma hiyo ilichelewa kutolewa kwa kuwalimia wakulima mashamba yao. Katika Wilaya ya Kaskazini 'A' kulikuwa na wakulima tayari wameshalipa pesa zao na wakacheleweshewa kulimiwa mashamba yao na wakatumia majembe ya mikono. Je, Mhe. Waziri wananchi wale walirejeshewa fedha zao. Kama wamerejeshewa ni lini walikabidhiwa pesa zao hizo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, suala la fedha, fedha hizo ziko chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na zimewekwa kwa sababu ya kutumika kwa kipindi kijacho. Kwa mtu yeyote yule ambaye atahitajia pesa zake basi aende Wizara ya Kilimo atarudishiwa fedha zile ambazo alitoa wakati huo.

Mhe. Panya Ali Abadía: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipatia na mimi fursa hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa wakulima wetu msimu huu walichelewa kulimiwa mapema na kuikosa hiyo miongo vizuri. Je, wizara ina mpango gani kwa msimu ujao ili wakulima waweze kulimiwa kwa wakati muwafaka.
Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ishara inaonekana wazi kwamba tatizo hilo linaweza kuondoka na linaendelea kuondoka, kutokana na ununuaji wa vifaa ambavyo vinanunuliwa na Wizara ya Kilimo kwa kipindi hiki. Ukichukulia kwamba *planters* 30 zimeongezwa, matrekta 20 nayo yameongezwa, *combine harvesters* 14 zimeongezwa na bado tunaendelea kuongeza vifaa vingine ili kuwaondoshea wakulima wetu katika hali hii ya kilimo kipya cha hivi sasa.

Mhe. Salim Abadalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama aliazozieleza Mhe. Waziri na mabadiliko ya hali ya hewa kwa bahati mbaya safari hii imetokezea kwa wakulima wetu wa mpunga kilimo chao kimekuwa kibaya sana na wamepata hasara Kubra sana. Je, wizara ina mpango gani wa kutoa fidia au msaada kwa wakulima hawa ambao ndio wengi kwa hasara hii waliyoipata.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ningempa ushauri kwamba wale wanaochelewesha hii tukashirikiana naye kwa sababu inaonekana yeye ana ujuzi mkubwa katika suala hili ili tukatatua tatizo hili kwa wananchi wetu pamoja.

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti): Waheshimiwa Wajumbe kidogo nitamuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutengua kifungu ili serikali iweze kutoa taarifa Ambato imeletwa mbele yetu kuhusu usajili wa meli za nje. Mhe. Waziri nakuomba utengue kwanza kifungu ili tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Kanuni ya 43 na 27(4) tunaomba kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tulileta taarifa hii kwako na kwa kuwa Baraza lako tukufu jana lilitaka tutoe taarifa mbele ya Baraza kuhusu usajili wa meli za nje uliofanywa na Serikali za Mapinduzi ya Zanzíbar. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, uturuhusu kabla ya kuendelea na shughuli za leo za Mhe. Waziri kuwasilisha hotuba yake ili Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano apate nafasi ya kutoa kauli ya Serikali kuhusu usajili wa meli za nje.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ruhusa yako tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Niwahoji wale wanaokubaliana na hoja, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA YA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kukubali na niwashukuru Wajumbe kwa kuunga mkono nipate fursa ili kutoa taarifa ya serikali kuhusu usajili unaofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa Meli za Nje na uvumi ambao umetokea hivi siku za karibuni. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba nifanye hivyo.

Taarifa hii ni taarifa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mhe Mwenyekiti, tarehe 27/6/2012 vyombo vya habari haya nchini, Gazeti la *The Citizen* na lile la nchi za nje *International News Agency, Bloomberg*, viliandika makama kuhusu usajili wa meli kumi za mafuta (*Tankers*)**.** Ilidaiwa katika makala hayo kuwa meli hizo zilisajiliwa Zanzibar na zinapeperusha bendera ya Tanzania na kwamba zinafanya biashara na Kampuni ya Serikali ya Iran.

Gazeti la *The Citizen* la tarehe 27 Juni, 2012 lilikuwa na kichwa cha Habari '*Iran Tankers adopt Tanzania Flag to avoid Embargo'.* Kwa tafsiri ya Kiswahili ni kwamba Meli za Mafuta za Iran zinatumia Bendera ya Tanzania kukwepa Vikwazo.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar ni mamlaka iliyoundwa kwa sheria Nam. 3 ya mwaka 2009 ambayo pamoja na kazi nyengine inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Baharini Zanzibar ya mwaka 2006, (*Zanzibar Maritime Transport Act. 2006*). Sheria ya *Zanzibar Maritime Transport Act.* 2006 Kifungu Nam. 8 cha sheria hii kinasomeka kama ifuatavyo:

Section 8 (1). There shall be established the registers of Tanzania Zanzibar ships to be Known as:-

- ***(a). Tanzania Zanzibar International Register of Shipping for ocean going ships; and***
- ***(b) Tanzania Zanzibar Register of Shipping for coastal Ships.***

- ***(2). A ship shall be a Tanzania Zanzibar ship for the purpose of this Act if that ship is registered under this part.***

Katika kutekeleza jukumu la usajili wa meli kama ilivyoelekezwa katika kifungu 8(1) (a) hapo juu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetiliana mkataba na kampuni ya PHILTEX ya Dubai kufanya usajili wa meli za kimataifa. (Open Registry). Usajili huu umekuwa ukifanyika tangu mwaka 2009 na mpaka sasa ZMA kupitia Wakala wake imesajili meli 399 ikiwa ni pamoja na meli za mafuta, makontena, *General cargo* na meli za Abiria.

Kama nilivyoeleza hapo awali, vyombo vya habari vimechapisha makala ya usajili wa meli 10 ambazo zinadaiwa ni meli za IRAN kulingana na makala zao hizo.

SMZ inatoa taarifa rasmi juu ya meli za mafuta ilizosajiliwa wiki mbili zilizopita pamoja na majina ya meli, ukubwa wake, majina ya makampuni inayomiliki meli hizo na nchi zilizotoka kabla ya kupata usajili kwa ZMA, kama ifuatavyo:

Jina la meli	*GRT (Ukubwa)*	*Company name*	*Ilikotoka*
1. Daisy	**81479**	**Daisy Shipping Co. Ltd**	**Malta**
2. Justice	**164241**	**Justice Shipping Co. Ltd**	**Cyprus**
3. Magnolia	**81479**	**Magnolia Shipping Co. Ltd**	**Malta**
4. Lantana	**81479**	**Lantana Shipping Co. Ltd**	**Malta**
5. Leadership	**164241**	**Leadership Shipping Co. Ltd**	**Cyprus**
6. Companion	**64241**	**Companion Shipping Co. Ltd**	**Malta**
7. Camellia	**81479**	**Camellia Shipping Co. Ltd**	**Malta**
8. Clove	**81479**	**Clove shipping Co. Ltd**	**Malta**
9. Courage	**163660**	**Courage Shipping Co. ltd**	**Cyprus**
10. Freedom	**163660**	**Freedom shipping Co. Ltd**	**Cyprus**
11. Valor	**160930**	**valor Shipping Co. Ltd.**	**Cyprus**

Jumla ya GRT ni 1,388,368 tons

Mhe. Mwenyekiti, meli hizi ni 11 kama zinavyoonekana katika orodha hapo juu ni miongoni mwa meli nyingi zinazobadilisha usajili wao (*De-registration*). Meli zilizosajiliwa na Zanzibar zinatoka nchini Cyprus na Malta na sio Iran. Sambamba na meli hizi 11 zilizosajiliwa na serikali, meli za mafuta nyengine 20 ambazo zinasemekana zilikuwa kwenye usajili wa nchi za Ulaya zimebadilisha usajili wao na kwenda usajili wa "TUVALU Islands".

Serikali ilimtaka Wakala wake *Philtex Corporation* kuwaita wenye meli hizi na kuwataka kujieleza kuhusu uhusuiano wao na Serikali ya au makampuni ya mafuta ya IRAN. Philtex kama wakala wa *Zanzibar Maritime Authority* mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikutana na Wamiliki hao siku ya Alkhamis tarehe 28/06/2012 katika afisi za *Philtex Corporation* na Wamiliki hao wameeleza kwamba hawana uhusianao na Serikali au mamlaka yoyote nchini Iran na wameamua kuja kusajili Zanzibarikwa ridhaa yao na kwa kufuata matangazo ya usajili wetu wa nje (*Open Registry*).

Mhe Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, wamiliki hao wametangaza kwamba ikiwa Zanzibar haiko tayari kuendelea na usajili wa meli zao, wanaweza kufuta usajili wao na tayari wanafikiria kufanya mazungumzo na open Registry nyengine (PANAMA) lakini hawana nia ya kurudi walikotoka, yaani Cyprus na Malta.

Mhe. Mwenyekiti, kinyume na maelezo yaliyotolewa na vyombo vya habari juu ya uraia wa wamiliki wa meli hizi, Wamiliki wa meli hizi kama walivyoeleza hapo juu katika usajili wa meli zao wana uraia wa *British Virgin Islands* na *Sychelles*.

Kulingana na *"United Nations Convention Law of the Sea"*, Article 91, na za *"Geneva Convection of Registration" articles* 6, 7 na 8, na kulingana na Zanzibar *Maritime Transport Act of* 2006, *section* 8, Zanzibar ikiwa ni nchi moja kati ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayo haki ya kusajili meli yoyote kulingana na taratibu na Sheria za Zanzibar, na sheria za Kimataifa zinazoongoza usajili huo.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo haya yanatolewa na serikali ili kutoa ufafanuzi wa uvumi kuwa Zanzibar imesajili meli za IRAN ambazo zimewekewa vikwazo na Marekani na nchi za Umoja wa Ulaya (European Union) juu ya usafirishaji na uuzaji wa mafuta kutoka Iran.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hizi za vyombo vya habari kwa tafsiri nyepesi hazina madhumuni yoyote zaidi ya kuwavunja moyo wenye makampuni ya meli wanaotaka kusajili meli zao kwetu.

Hivyo basi Serikali inatamka wazi kwamba Usajili uliofanywa kwa meli hizi umefuata taratibu zote zilizowekwa kisheria na kwamba Serikali imekuwa ikifanya na itaendelea kufanya mazungumzo na wenye meli mbalimbali ili kuongeza idadi na ukubwa wa meli inazosajili nje ya nchi. Biashara hii ya ukubwa wa GRT 1,388,368 Tons katika kipindi cha wiki mbili na maombi mapya matano kwa meli zitakazokuwa na ukubwa wa zaidi ya GRT 500,000 imeshtua Makampuni mengi na hata nchi nyengine zisizoitakia mema Zanzibar katika juhudi zake za kukuza mapato na uchumi wake.

Hata hivyo mamlaka itafata sheria zote zilizowekwa kitaifa na kimataifa katika biashara ya usafiri baharini na itahakikisha meli zinazosajiliwa chini ya mamlaka hii zinafata taratibu ilizoweka.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya taarifa hizi za vyombo vya habari (The Citizen), Waziri wa Uchukuzi wa SMT Mhe. Harisson Mwakyembe) alipokuwa akijibu swali Bungeni hivi juzi tarehe 22 mwezi wa sita hakuonesha kurishika kwake katika usajili wa meli (Open Registry) inayofanywa na Zanzibar na kuahidi kufanya ziara ya kuja Zanzibar kuonana na Waziri anayehusika kuzungumzia suala hili. Taarifa za "*The Citizen*" zaweza kuwa ni muendelezo wa kutoridhika kwa Mwakyembe katika usajili unaofanywa na Serikali kupitia uwakala wake huko Dubai.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar haifungiki kusajili meli za nchi yoyote. Hili ni suala la kibiashara na kwamba kwa Serikali yetu hii ni njia moja ya kuongeza mapato yanayoendesha Serikali, alimradi tu usajili huo hauvunji sheria za Kimataifa na kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina uhusiano mkubwa na wa muda mrefu na nchi nyingi ikiwemo IRAN na hivi karibuni Zanzibar ilipata ugeni (Makamo wa Rais wa Iran) na viongozi wetu wa kitaifa walifanya mazungumzo ya namna gani IRAN itaendelea kusaidia Zanzibar katika miradi ya Maendeleo. Zanzibar haingependa kuingizwa kwa visingizio vyovyote na kwa njama zozote katika migogoro isiyowahusu.

Hivyo basi Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa hii, Serikali inakanusha rasmi uvumi wa vyombo vya habari kuhusiana na suala hili kama taarifa hii ilivyofafanua hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimwa Wajumbe naomba kuwasilisha.

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti): Ahsante sana Mhe. Waziri, sasa Waheshimiwa Wajumbe kutokana na kifungu hicho hicho cha 43 (3) kinaruhusu kuweza kumuuliza maswali Waziri yanayohusu taarifa ambayo kaitoa.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe nakuombeni tuwe *very brief* muda sio mkubwa tulionao ili tuweze kuendelea na shughuli zetu nyengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii pamoja na kuwa hatujadili na sikusudii kujadili, naomba uniruhu niishukuru na kuipongeza sana serikali kwa umakini wake lakini kutoa ufafanuzi wake ulioutoa leo hii, ninaamini utasaidia sana kuondosha hayo yanayokusudiwa kufanywa dhidi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili.

La kwanza…

UTARATIBU

Mhe. Ali Mze Ali: Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii ni taarifa nzito na Barazani imeletwa, lakini tumetakiwa tutoe kikawaida sasa hivi hii taarifa hatuna.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa mimi naona tuendelee kwanza na maswali halafu baadae sasa, taarifa hiyo imesomwa ninafikiria maamuzi yametoka jana kama sikosei. Kwa hivyo uwezo wa kufanya yote jana ulishindikana, hivyo naomba muukubali hii taarifa maswali yaulizwe halafu baadae mimi naamini Waziri ataitoa taarifa vizuri ili hata kifungu kinaweza kikaruhusu tukaweza tukajadili vile vile.

Naomba tuendelee na maswali.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, Baraza haliendeshwi kwa fikra. Cha msingi hii si mara ya kwanza taarifa kama hii.

Taarifa ya vitu chakavu kwenye meli na vyenginevyo, hakuna ubaya wowote, hakuna haraka yoyote. Taarifa hii igaiwe, sio kama tujadili kesho au jioni au siku nyengine, itakuwa haina maana. Lakini tungepewa taarifa tutaisoma tutaijadili kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tangu awali nilisema katika Kanuni ya 43 (3), tunaambiwa kwamba hakutakuwepo na majadiliano yoyote kuhusu kauli yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii.

Lakini wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika kumuuliza maswali Waziri aliyetoa kauli hiyo kwa madhumuni ya kuwaeleweshwa zaidi juu ya maendeleo ya kauli hiyo. Hakuna sehemu inayosema kwamba wajumbe lazima wawe na karatasi au taarifa kabla, hamna.

Kwa hivyo naomba tuendelee na kuuliza maswali kama kawaida.

Mhe Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijamsikia mtu aliyesimama akaomba idhini yako kuwa tuizungumze.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe naomba hapa turidhiane tufanye hii shughuli ili tumalize kwa utaratibu huu ambao tumeupanga. Tukianza kulumbana hapa Mhe. Mjumbe itakuwa kazi haifanyiki.

Kwa sababu mimi niliyekuwepo hapa sio Spika, mimi ni Mwenyekiti. Kwa hivyo naomba mheshimiwa atakapofika hapa kwa sababu ninafanya kazi ya Spika aseme hayo maneno ambayo wewe unaombwa yasemwe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, sikusudii kuingia katika mjadala huu lakini sidhani kama ninalazimika kuomba idhini yako, kwa sababu kwa kule kutamka tu kwamba tunaweza kuuliza maswali ndio tayari idhini. Ninadhani nikiisoma Kanuni ya 43 (3) inajieleza vizuri kwa hivyo sidhani kama nahitaji kuomba ruhusa, madhali umeruhusu tuulize maswali, ndio umetoa hiyo idhini.

Sasa niendelee Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nilikuwa na maswali mawili.

La kwanza ni kwamba kwa sababu suala hili tangu lilivyoripotiwa katika vyombo vya habari lilikuwa na sura ya uchonganishi fulani katika nyanja za uhusiano wa kimataifa, na kwa sababu suala hili la usafiri baharini na usajili wa meli kwa jumla Zanzibar imeshafanya maamuzi tangu mwaka 2004 kupitia katika semina ya Wawakilishi na baadae ikaletwa Barazani, Zanzibari ikatunga sheria yake ya *Zanzibar Maritime Transport Act* iliyotofauti na *Merchant Shipping Act* ya Jamhuri ya Muungano.

Swali langu kwa Mhe. Waziri ni kwamba katika kulinda heshima na hadhi ya Zanzibar na kutokuharibu mahusiano yake mema sio tu na Iran lakini na nchi nyengine ambazo tumejaribu kuchonganishwa nazo, kwa mfano nchi za Ulaya na Marekani ambazo ndizo zilizoweka vikwazo hivi.

Serikali ina mpango gani wa kuwasiliana na afisi hizi ili kuweka sawa suala hili na kuondosha uwezekano wowote wa kuleta athari za kiuchumi wa Zanzibar kama alivyosema Mhe. Waziri Zanzibar kwa kusajili meli hizo haikiuki maagizo ya kimataifa kwa kupitia chombo kinachotambulikana ambacho ni Umoja wa Mataifa. Hilo la kwanza.

Swali langu la pili Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo ya Waziri amesema kitu ambacho sote tumekisikia kwamba Waziri wa Uchukuzi anayeambiwa wa Jamhuri ya Muungano, ingawa mimi ninavyojua uchukuzi si suala la muungano, ametoa taarifa katika Bunge ambapo imeishutumu Zanzibar kwa utaratibu wake wa usajili wa vyombo vya baharini umekuwa haumridhishi, jambo ambalo yeye halimuhusu.

Jee, serikali inafikiria kuchukua hatua gani za kuwasilisha na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuwapa onyo Mawaziri ambao hawahusiki na muungano kutoingilia mamlaka Zanzibar katika mambo ambayo yapo na kuekwa Kikatiba na kwa mujibu wa mkataba wa muungano.

Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi ya leo kuweza kumuuliza Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Waziri kwa kweli hiyo haki ambayo wenzetu wanataka kutufanyia sio jambo busara katika kutuingilia katika mamlaka ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar imeturuhusu kuweza ku-*register* hizo meli za nchi za nje.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ninataka nimuulize swali. Mhe. Waziri hamuoni kwamba sasa imefika haja ya hivyo vikao vyenu munavyokaa kujadili masuala ya muungano kuwa ndio basi.

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akitoa maelekezo yake ndani ya Bunge alisema kwamba, meli zote chakavu zinaelekea Zanzibar kwa ajili ya usajili. Jee, Mhe. Waziri anaweza kututhibitishia kwamba kauli ina ukweli kiasi gani.

Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba sasa Waziri sasa ajibu maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe. Karibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kujibu maswali na kutoa ufafanuzi kwa Wajumbe wako ambao wametaka kujua mambo yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwanza nataka nianzie nambari tatu kuja juu.

Mhe. Mahmoud ameeleza namna ambavyo Waziri wa Uchukuzi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania alivyokuwa akishutumu kuwa meli zote zinaelekea kusajiliwa Zanzibar ni chakavu.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe usajili wa meli una taratibu zake. *Definition* ya uchakavu nayo pia inajulikana katika masharti hayo. Lakini ninachowathibitishia Wajumbe kwamba hakuna meli inayosajiliwa na wakala wetu kwa sheria zetu na za kimaitaifa kama haijakuwa-survey na. *International surveyors* wanatoa *certificate* kwamba hii meli hadhi ya kwenda baharini.

Sasa suala la uchakavu ni *definition* ya mtu lakini tunachohakikisha ni kwamba hakuna meli si *workless'* baada ya ukaguzi wa kimataifa. Kwa hivyo hili si suala ambalo mtu anaweza akafikiria.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mshimba alitoa shauri au aliuliza kwamba kutokana na haya mambo yanayoendelea suala kama hili si la muungano lakini watu wanaingilia katika mamlaka ambayo si ya kwao, kwa nini vikao hivi vya kero za muungano visisimamishwe visiwe basi.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika hili nasema huu ni utaratibu wa serikali hizi mbili katika mambo ya muungano. Katika mambo ya muungano mimi ninakubali kuwa vikao hivi viendelee, lakini katika mambo si ya muungano tuachiwe wenyewe na wao wafanye shughuli zao.

Kwa hivyo si suala la vikao vyetu sisi na wao katika mambo yetu. Vikao vyetu sisi na wao ni katika yale mambo ya pamoja. *Zanzibar Maritime Authority* na kule wana Sumatra. Sisi katika SUMATRA hatuwaingilii katika jamabo lolote.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa ni vizuri Wajumbe wafahamu kwamba meli zetu zinapepea bendera ya Tanzania. Basi mimi ninafikiri katika kujadili hili tupate ufumbuzi kwamba sasa meli zetu zipepee bendera ya Zanzibar. (*Makofi*).

Hili tutalichukua tutakwenda nalo na pengine katika mjadala huu wa Katiba si ajabu suala hilo likatumbukizwa. Kama mulikuwa hamulioni Waheshimiwa Wajumbe na hilo liingizeni, kwamba kwa yale mambo ya Zanzibar yalioko nje huko basi shughuli zetu na afisi zetu, meli zetu tunazosajili basi ipepee bendera ya Zanzibar badala ya bendera ya Tanzania. Hii kupepea bendera ya Tanzania ndio wenzetu wana nafasi sasa ya kusema hivi na hivi.

Kwa hivyo vikao hivi vya muungano mimi ninasema ni utaratibu wa serikali mbili viendelee na hivi vyetu sisi tunaweza tukashauriana si vibaya. Lakini si kufanya maamuzi ya upande mmoja kwa upande mwengine.

Mhe. Jussa alisema kwamba sura ya taarifa hizi ni kama uchonganishi. Na alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuwasiliana na ofisi ya vyombo hivi ili kujua hali halisi.

Mhe. Jussa hii taarifa ambayo tumeitoa tumeifanyia kazi kutokana na magazeti kwanza, lakini ndio magazeti *international* ya *citizen* limo kwenye mtandao ulimwengu mzima. Kwa hivyo taarifa hii vile vile ni imani yangu nayo itakwenda katika mtandao wa ulimwengu mzima.

Serikali inakanusha tuhuma hizi na kwa ushahidi huu. Lakini vile vile itabidi tuwaite watu wa gazeti la *citizen* ili tuwaulize taarifa hizi zimetoka wapi, ilikuwaje kwa sababu mbona hawakuja kwetu wakatuuliza kabla ya taarifa hizi kuziandika.

Kwa hivyo ni masuala ya uhakika. Ni masuala na ni ushauri mzuri tu na kila chombo ambacho kilihusika na hili Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ahadi hapa kwamba serikali itakaa tutashirikiana na vyombo mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni mkuu wa shughuli za serikali ili tuone kila aliyehusika katika hili tunachukua hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, swali lake la pili la Mhe. Jussa ni kwamba taarifa hizi ambazo ni shutuma kutoka ya Serikali ya Muungano wa Tanzania, jee serikali yetu itachukua hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, hili sina jawabu la moja kwa moja. Kama nilivyosema bado serikali zetu zinauhusiano lakini bila shaka tutachukua hatua kiasi ambacho kama suala hili wao wali-*over look*, basi waseme kuwa lilikuwa haliwahusu.

Kama kuna mambo maalum ambayo sisi tulitakiwa tufanye basi watwambie mufanye hili na hili. Mimi ninasema kushauriana katika masuala ndivyo inavyotakiwa. Lakini si kuamuliana kwamba fanyeni hili na hili musifanye, munafanya hivi, hivi mufanye.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe ukubwa wa meli hizi wa zaidi ya tani milioni moja na laki, ni biashara kubwa. Na wiki mbili hizi ambazo tumezungumzia na ndilo gazeti lilivyozungumzia kama *frenquency* ni hiyo, wiki mbili una-*register one point three million* GRT, ni kwamba tuna vivutio vikubwa katika matangazo yetu hasa kwa kutumia agent aliyeopo Dubai.
Kama mfumo ni huo ni kwamba wengine wananyang'anywa, hizo meli ambazo zilizokuwa huko sasa zinakuja huku. Sasa ninasema tena inawezekana kabisa ni utaratibu mwengine wa kibiashara. Hivi sasa inaonekana kama Iran, ukizungumza Iran vikwazo labda nchi zitashtuka lakini ufafanuzi ni huu wa serikali.

Mimi ninasema tena kwamba Zanzibar ina haki ya kusajili meli.

Nilifikiri Mhe. Jabu Hashim ndio mwenye tabia hiyo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama nimekidhi haja ya Waheshimiwa Wajumbe walioiuliza maswali lakini kwa hapo hapo, huo ndio ufafanuzi wangu. Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue fursa hii nimpongeze sana Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa maelezo mazuri aliyotoa kwenye Baraza hili tukufu.
Lakini ningependa nitoe ufafanuzi mdogo tu kwamba ile bendera ni bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ile si bendera ya Tanzania Bara, maana yake ni bendera yenye ushiriki wa nchi mbili huru, ya Zanzibar na ya Tanganyika na tukaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo ni haki yetu kuitumia. Tuitumie ili itusaidie katika maendeleo yetu ya kukuza uchumi. Eneo hili linahusu uchumi wa Zanzibar. Kwa hivyo haki zake Zanzibar lazima izipate na zilindwe na kuendelezwa.

Kama kuna jambo lolote la mazungumzo tutazungumza lakini suala la kuendelea na usajili liendelee ili mapato yaingie katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe muda wetu uliobakia ni mchache kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais ambaye alikuwa yeye aje atupe hotuba yake hapa, lakini hotuba yake hiyo itachukua muda wa saa moja na dakika arobaini na tano na leo hii ni siku ya Ijumaa.
Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe nimuombe Mhe. Waziri afanye shughuli yake ya kuturuhusu kutuomba ili turuhusike kuahirish mpaka jioni.

Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa leo ni Ijumaa na kwa kuwa hotuba ya Waziri itachukua zaidi ya saa moja na dakika arobaini na tano, na tukitazama wakati wetu wa kawaida kwa siku ya Ijumaa utakuwa umekwenda zaidi kutokana na Kanuni zetu za siku ya Ijamaa.

Kwa hivyo naomba tuweke Kanuni kando ili tuakhirishe Baraza letu kwa sasa hivi twende Msikini tukasali na baadae Mhe. Waziri aje kusoma hotuba yake jioni hii ya saa 11.00 jioni. Naomba kutoa hoja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5.00 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema, na kuweza kukutana hapa katika kikao hiki muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Aidha, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuongoza, kutuelekeza na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa majukumu ya serikali kama ilivyoainishwa katika

miongozo iliomo katika Mipango Mikuu ya Kitaifa, Kimataifa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015.

Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri juhudi zake anazozichukua katika kulitumikia Taifa na kuweza kutenga muda maalum wa kukutana na watendaji, ili kupitia mipango ya utekelezaji wa bajeti ya kila Wizara bila ya kuchoka tena kwa uadilifu mkubwa, umahiri na umakini mkubwa umeleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji ndani ya serikali. Hakika changamoto anazotupa zimetufanya tuwe na mtizamo mpya katika upangaji na utekelezaji wa kazi zetu. Hatua hii imeleta uwazi, ubunifu na uwajibikaji katika kusimamia maadili ya matumizi ya fedha za umma. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu na afya njema ili aweze kuiongoza vyema nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Makamo wa Pili wa Rais, kwa kumsaidia kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa kazi zake. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuitumikia nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mhe. Spika yeye binafsi, Mhe. Naibu wake na nyinyi Waheshimiwa Wenyeviti kwa kuliongoza vizuri Baraza letu. Umahiri wenu katika kutuongoza, umepelekea kukua na kuimarika kwa demokrasia na mijadala iliyo wazi, inayosisimua na inayovutia wananchi wetu. Hali hii imejenga imani kubwa ya wananchi kwa chombo chao cha kutunga Sheria, pia kujenga imani kwa viongozi waliowachagua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee natoa pongezi maalumu kwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, zinazofanya kazi na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kamati hizo ni Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya uongozi wa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, ambae pia ni Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Vile vile Kamati ya Kusimamia Hesabu za Serikali (PAC) inayoongozwa na Mheshimiwa Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake. Ushauri na miongozo yao mizuri imesaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku, na tunawaahidi kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano wetu kwao. Naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ambao kwa namna moja au nyengine wamekuwa wakifanya kazi na Wizara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba yangu hii inalenga kutoa maelezo ya kina ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2011/2012. Aidha, nitaeleza pia muelekeo wa vipaumbele vya bajeti na malengo yatakayotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mwaka ujao wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa kipindi cha Julai- Machi 2011/2012 kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, umezingatia vipaumbele vilivyowekwa katika malengo ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2011/2012. Sambamba na malengo hayo, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar ilitekeleza miradi kumi ya maendeleo. Miradi hiyo ni kama ifuatayo:-

i. Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali (*State Lodges*)
ii. Kuimarisha Mawasiliano Ikulu
iii. Mageuzi ya Serikali za Mitaa
iv. Uendelezaji Vitambulisho
v. Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja
vi. Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
vii. Shamba la Mfano la Mbogamboga-Bambi
viii. Ujenzi wa Makao Makuu ya Valantia
ix. Ujenzi wa Hospitali mpya ya Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM)
x. Ujenzi wa Chuo Kipya cha Mafunzo Hanyegwa Mchana

Mhe. Mwenyekiti, Aidha, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilitekeleza Mradi wa Mpango wa Kuimarisha Huduma za Miji Zanzibar (*Zanzibar Urban Service Programme ZUSP*). Usimamizi wa utawala na fedha wa mradi huu upo chini ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, matayarisho ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa Mwaka wa fedha 2012/2013, yamezingatia mipango ya kisekta iliyowekwa katika Dira 2020 (*Vision 2020*), malengo ya maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala cha CCM ya 2010 – 2015, pamoja na vipaumbele ambavyo vimewekwa ili kutatua changamoto mbali mbali. Kwa ujumla, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inalenga kutekeleza vipaumbele katika mambo yafuatayo:-

i) Kuendeleza umoja wa kitaifa na mshikamano.
ii) Kusimamia utekelezaji wa miundo ya utumishi na uhakiki wa kazi kwa watendaji.
iii) Kuendelea kuimarisha makaazi na nyumba za Ikulu.
iv) Kuendelea kuimarisha mawasiliano na utoaji wa habari.
v) Kuendelea na jitihada za kufanya Mageuzi ya Serikali za Mitaa, ikiwemo kufanya mapitio ya mipaka ya maeneo pamoja na kusimamia utungaji wa Sheria kama inavyoelekezwa na matamko ya Sera ya Serikali za Mitaa.
vi) Kuimarisha uwezo na utoaji wa huduma ikiwemo usafi hasa mijini.
vii) Kuendelea kuimarisha na kuongeza uwezo wa Idara Maalum za SMZ, ikiwemo kuimarisha haki za binadamu kwa wanafunzi waliopo Chuo cha Mafunzo na kujenga Chuo kipya Hanyegwa Mchana.
viii) Mafunzo kwa wafanyakazi juu ya haja ya kubadilika kiutendaji na kufahamu dhamana walizonazo hasa katika mazingira wanayofanyia kazi.
ix) Kuimarisha tafiti kwa lengo la kupata taarifa zitakazowezesha kupanga mipango kulingana na matokeo ya tafiti hizo.
x) Kuendelea kuimarisha mfungamano wa Kikanda ili Wazanzibari waweze kuzitumia fursa za kiuchumi zinazotokana na Jumuia ya maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Jumuia ya Afrika ya Mashariki pamoja na Jumuia nyengine za Kikanda.
xi) Kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kushiriki na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi yao.
xii) Kutoa elimu kuhusu masuala mtambuka (*cross cutting issues*) ikiwemo huduma za watu wenye ulemavu, kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI na VVU.
xiii) Kwa kusaidiana na vyombo vyengine vya Kitaifa, kuimarisha ulinzi na usimamizi madhubuti wa mipaka yetu pamoja na kudhibiti magendo na uharamia.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na malengo na vipaumbele vya jumla, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itatekeleza jumla ya miradi minane ya maendeleo iliyopo hapa chini:-

i) Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali (*State Lodges*)
ii) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano - Ikulu
iii) Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa
iv) Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Ushoni *Zanzibar Quality Tailoring* cha Idara Maalum za SMZ
v) Ujenzi wa Hospitali ya KMKM
vi) Ujenzi wa Makao Makuu ya Kikosi cha Valantia
vii) Mradi wa Shamba la Mfano la Mboga Mboga JKU
viii) Ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo Hanyegwa Mchana

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu Serikali ilikuwa katika mchakato wa kuandaa Sera ya Serikali za Mitaa ambayo ndiyo muongozo wa utekelezaji wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Sera hiyo sasa imekamilika. Utaratibu wa maandalizi ya Sera hii, umefuata hatua kadhaa zikiwemo,

(a) Mapitio ya taarifa na Sera mbali mbali zikiwemo tafiti zilizofanywa juu ya mageuzi ya Serikali za Mitaa Zanzibar,
(b) Mapitio ya MKUZA na DIRA ya Maendeleo ya 2020,
(c) Mapitio ya Sheria mbali mbali zinazohusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
(d) Kufanya mapitio ya muundo wa Serikali za Mitaa
(e) Mahojiano na baadhi ya watendaji, na
(f) Mikutano ya Wadau Unguja na Pemba, kikiwemo kikao cha Makatibu Wakuu na Kamati ya Uongozi ya Wizara na hatimae kupitishwa rasmi na Baraza la Mapinduzi. Sera hii inakwenda sambamba na utekelezaji wa maazimio ya kupeleka madaraka kwa wananchi.

Aidha, Sera ya Serikali za Mitaa inatoa Mamlaka na nguvu za Utawala katika Serikali za Mitaa, na inalenga kutoa msukumo maalumu wa kuishirikisha jamii katika mipango ya kujiletea maendeleo kutoka katika ngazi ya chini kwa misingi ya ushirikishwaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liniruhusu kuwasilisha utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na mwelekeo wa bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Idara na Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

MUUNDO WA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inajumuisha Ofisi, Idara, Vitengo na Taasisi zifuatazo:-

a) Ofisi ya Faragha ya Rais
b) Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
c) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
d) Idara ya Uendeshaji na Utumishi
e) Idara ya Mawasiliano Ikulu
f) Kitengo cha Usalama wa Serikali (GSO)
g) Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba
h) Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho
i) Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje
j) Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (inajumuisha Serikali za Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa)
k) Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (inajumuisha Idara Maalum za SMZ).

OFISI YA FARAGHA YA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha ya Rais inashughulikia kuratibu shughuli za kila siku za Mhe. Rais wa Zanzibar, kusimamia ratiba za kazi, kuweka kumbukumbu za mazungumzo yanayofanyika na kutayarisha muhtasari wa ripoti. Kadhalika, Ofisi hii inasimamia upatikanaji wa huduma zote za Mhe. Rais na kushughulikia utunzaji na matengenezo ya nyumba zote za Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Faragha ya Rais iliidhinishiwa TZS 520 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Ofisi hii iliingiziwa TZS 466.3 milioni sawa na asilimia 89.7 ya makadirio ya matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha ya Rais imetekeleza vyema mujukumu na malengo yake kwa kuratibu ziara za Mhe. Rais ambapo alikutana na wananchi, viongozi wa Mikoa, Wilaya na baadhi ya Taasisi za Serikali. Kwenye ziara hizo, Mhe. Rais alishuhudia hatua mbali mbali za maendeleo na alielezwa changamoto na hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana nazo. Miongoni mwa Taasisi alizozitembelea ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Shirika la Utangazaji Zanzibar, Mamlaka ya Maji (ZAWA) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Katika Taasisi zote hizo alizozitembelea aliridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na Taasisi hizo na wananchi katika kujiletea maendeleo, na kutoa maelekezo ya namna ya kuimarisha huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ziara za Mikoa, Ofisi ya Faragha ya Rais iliratibu ziara hizo kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa. Katika kila Mkoa, Mheshimiwa Rais alipokea taarifa za utekelezaji na kupata ufafanuzi wa baadhi ya mambo muhimu. Aidha, Mheshimiwa Rais alikagua miradi ya maendeleo ikiwemo ya Serikali na iliyoanzishwa na wananchi wenyewe. Katika ziara hizo aliwasisitiza viongozi wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha kwamba wanatatua wenyewe migogoro ya ardhi iliyopo, na kuepukana na kuanzisha migogoro mipya ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine yaliyojitokeza ni pamoja na vitendo vya uharibifu wa mazingira na udhalilishaji wa kijinsia ambapo Mikoa yote imeagizwa kuandaa mikakati ya kuvidhibiti vitendo hivyo haraka iwezekanavyo. Kwa ujumla ziara hizi zimeonesha mafanikio makubwa na kuwafurahisha wananchi, ambapo walipata fursa za

kuainisha matatizo yao na kupatiwa ufumbuzi wa papo kwa papo. Kadhalika, ziara hizi zimesaidia kuongeza ukaribu kati ya wananchi na Serikali yao, na pia kuhuisha matumaini yao katika kujiletea maendeleo na kuendeleza hali ya amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2011/2012, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya ziara katika Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (Ras el Khaimah, Sharjah na Dubai). Mhe. Rais wa Zanzibar na ujumbe wake walikutana na Mtawala wa Ras el Khaimah Sheikh Saud Saqr Al Qasimi na Mtawala wa Sharjah Sheikh Dkt. Sultan bin Mohammed Al Qasimi. Serikali ya Ras el Khaimah na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetia saini mkataba wa makubaliano (*MOU*) katika Nyanja kadhaa za kiuchumi na maendeleo ya jamii. Kadhalika, Hospitali Kuu ya Ras el Khaimah imetiliana saini (*MOU*) na Wizara Afya ya Zanzibar kwa lengo la kushirikiana katika matibabu ya maradhi ya kisukari, figo, moyo na saratani. Sharjah nayo imekubali kimsingi kuisaidia Zanzibar katika utafiti wa maji yaliotuwama chini ya ardhi. Kwa jumla ziara ya Mheshimiwa Rais katika Falme za Kiarabu imefungua milango mipya ya ushirikiano katika nyanja zote muhimu, na itasaidia kuongeza kasi ya maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar amekutana na Viongozi na Mabalozi mbali mbali wakiwemo mwana wa Malkia wa Uingereza Mheshimiwa Prince Charles na mkewe Camilla Parker Bowles, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mhe. Dkt Asha Rose Migiro, Waziri anaeshughulikia Maendeleo ya Kimataifa wa Finland Mhe. Heldi Hantaka, na Waziri wa Afya wa Norway Mhe. Anne-Grete Strom-Erichsen. Viongozi wote hao walimueleza Mhe. Rais namna walivyofurahishwa na maendeleo ya Zanzibar pamoja na hali ya amani na utulivu. Viongozi wengine mashuhuri waliokutana na Mheshimiwa Rais wanaonekana katika Kiambatanisho Namba 1.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na mafanikio hayo, Ofisi ya Faragha ya Rais pia imetekeleza malengo yake mengine kama ifuatavyo:-

a) Kufanya matengenezo ya sehemu ya kufulia na varanda katika Ikulu Kuu ya Mnazi mmoja, pamoja na kufanya matengenezo ya kawaida Ikulu ya Chake Chake ikiwa ni pamoja na kuweka vipoza hewa.
b) Ofisi imewaongezea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wake watano (5) kwa kuwapatia mafunzo na kuwalipia ada na vifaa vya masomo katika nyanja za menejimenti na huduma za chakula na vinywaji katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi.
c) Ofisi imeifanyia matengenezo makubwa maktaba ya Mheshimiwa Rais. Maktaba hiyo imo katika hatua za mwisho za ujenzi.
d) Ofisi imenunua vifaa mbali mbali vya kazi za kila siku za ofisi ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuandikia, majalada, magazeti, kompyuta sita (6) pamoja na uchapishaji wa kadi na vitabu vya hotuba mbali mbali za Mheshimiwa Rais.
e) Ofisi imetoa huduma zote muhimu kwa wageni wa Mheshimiwa Rais, pamoja na kufanikisha sherehe mbali mbali zinazofanyika Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Faragha ya Rais imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kuimarisha shughuli za kila siku za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
b) Kuimarisha mazingira ya wafanyakazi (*Work environment*) na kununua vitendea kazi.
c) Kuendeleza matunzo ya nyumba za Ikulu na vifaa vinavyostahiki.
d) Kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wa Ofisi ya Faragha ya Rais.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Faragha ya Rais iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/13, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,908.3 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi inayoongozwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi imepewa uwezo wa Kikatiba na Kisheria wa kuratibu na kusimamia shughuli zote za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake mbali mbali, ikiwa ni pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (*Inter-Ministerial Technical Committee*).

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa TZS 836 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida, na hadi kufikia Machi 2012, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iliingiziwa TZS 644 milioni, sawa na asilimia 77.0 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imeandaa vikao 25 vya Baraza la Mapinduzi na vikao 21 vya Kamati ya Makatibu Wakuu na kujadili nyaraka mbali mbali, zikiwemo Sera na Miswada ya Sheria (Viambatanisho 2 na 3) vinatoa ufafanuzi zaidi.
b) Imeratibu na kusimamia vikao 8 vya Kamati Maalum ya Baraza la Mapinduzi, Kamati ya Fedha, Uchumi na Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati nyenginezo zilizopewa majukumu maalum ya kuyafanyia kazi.
c) Imeratibu mikutano 48 ya pamoja kati ya Mheshmiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
d) Imenunua meza na viti vipya pamoja na kufunga mtambo wa sauti katika ukumbi wa Vikao vya Baraza la Mapinduzi.
e) Imefanya matengenezo makubwa katika Ofisi zake ziliopo katika Jumba la wananchi Forodhani, ikiwa ni pamoja na kutengeneza chumba madhubuti (strong room) kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu muhimu na kutengeneza Ofisi tatu za Mawaziri wasio na Wizara Maalum.
f) Imehifadhi kumbukumbu za zamani za Baraza la Mapinduzi ili kuzinusuru kuharibika kwa kuzitengenezea vitabu, pamoja na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu hizo kwa njia ya elektroniki.
g) Imewapatia wafanyakazi wake watatu mafunzo ya muda mrefu katika fani za utawala, usimamizi wa fedha na uandishi wa sheria.
h) Imeandaa mafunzo maalumu kwa wafanyakazi wake kuhusu mbinu na mikakati ya kupambana na maambukizi mapya ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kuwa Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu wanatekeleza ipasavyo majukumu yao ya kikatiba na kisheria.
b) Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na watumishi wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.
c) Kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
d) Kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu muhimu za Ofisi
e) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia watendaji stahiki zao
f) Kutathmini utendaji na uwajibikaji wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,362 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kuandaa na kusimamia utayarishaji wa Sera, Sheria, Mipango na kufanya utafiti na tathmini kwa miradi ya maendeleo. Aidha, ina jukumu la kufuatilia, kukusanya na kuchambua takwimu zitakazosaidia kufanya tathmini na kupanga mipango ya maendeleo. Vile vile, Idara inaratibu utekelezaji wa DIRA 2020, MKUZA II, Mageuzi Makuu (*Core Reforms*), Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Chama Tawala ya mwaka 2010 – 2015, na mipango mengine mikuu ya Kitaifa na Kimataifa. Jukumu jengine ni kuratibu kazi za kuandaa ripoti za utekelezaji wa Bajeti na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango Sera na Utafiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa TZS 240 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2012, Idara hii iliingiziwa TZS 158.5 milioni sawa na asilimia 66.0 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imetoa elimu ya uibuaji na uimarishaji wa miradi kwa maofisa 25 wa miradi.
b) Imenunua samani pamoja na kukusanya vitabu kwa ajili ya kitengo cha nyaraka (*Documentation Centre*).

c) Imeanzisha tovuti (*Website*) ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kutayarisha Barua Pepe rasmi (*Official E-mail Address*) za maofisa wote na watendaji wengine.
d) Imeanzisha kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEKNOHAMA*), na kukipatia samani na vitendea kazi vikiwemo kompyuta tatu, 3G computer modem, anti virus software na vifaa vya kuhifadhia kumbukumbu.
e) Imewajengea uwezo watendaji wake kwa kufanya ziara za kujifunza katika Ofisi za Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*) zilizopo Dodoma na Dar es Salaam. Aidha, wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi, kati ya wiki mbili hadi nne katika fani za uchambuzi wa Sera, kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kuangalia matokeo pamoja na uwajibikaji katika bajeti, sambamba na kuendesha semina mbili kwa Maofisa Mipango 52 wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Unguja na Pemba ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na namna bora ya kuandika ripoti za utekelezaji.
f) Imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
g) Imenunua vitendea kazi vikiwemo kompyuta nne, fotokopi kubwa moja, skana moja, na samani za Ofisi zikiwemo meza na viti.
h) Imeandaa ripoti za utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2011/2012, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala cha CCM ya mwaka 2010-2015.
i) Imeratibu utekelezaji wa miradi 10 ya maendeleo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuitembelea na kufanya tathmini juu ya utekelezaji wake na kujua hatua iliyofikia.
j) Kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi na Uendeshaji, imetoa mafunzo juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI na VVU kwa watendaji 34.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliidhinishiwa kutekeleza miradi 9 ya maendeleo na fedha zilizotengwa kwa miradi hiyo ni TZS 1,930.0 milioni. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu utekelezaji wa miradi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Naomba kuitaja miradi hiyo kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali (*State Lodges*)
ii) Kuimarisha Mawasiliano Ikulu
iii) Mageuzi ya Serikali za Mitaa
iv) Uendelezaji Vitambulisho
v) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja
vi) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
vii) Shamba la Mfano la Mboga Mboga Bambi
viii) Ujenzi wa Makao Makuu ya Valantia
ix) Ujenzi wa Hospitali mpya ya Kikosi cha KMKM

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali uliidhinishiwa TZS 300 milioni, na hadi kufikia mwezi Machi 2012, mradi huu umeingiziwa TZS 300 milioni sawa na asilimia 100.0 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kukamilisha matengenezo ya Ikulu ndogo ya Migombani kwa kuweka *grill* za chuma sehemu 16 eneo la pwani, kutengeneza msingi unaopokea maji ya mvua mbele ya Geti kuu, kujenga ukuta mpya sehemu ya kufulia, kuweka paa, kutengeneza mageti matatu, kulipa gharama za matengenezo ya waya na vioo vya madirisha, kulipa gharama za uwekaji wa viegesho vya gari (*car parking shades*), kulipa gharama za matengenezo ya Msikiti, kulipia gharama za matengenezo ya jiko la nje, pamoja na kujenga ukuta (*fence*) sehemu ya pembeni ya eneo la nyumba ya Migombani.
b) Kulifanyia ukarabati jengo la Ikulu Kuu (Mnazi Mmoja), kwa kutia rangi ukuta na kutengeneza sehemu ya vyoo.

c) Kuanza ujenzi wa nyumba ya Ikulu ndogo ya Laibon Dar-es-salaam kwa kufanya marekebisho ya jikoni na kuweka makabati ya aluminium, kugharamia uwekaji wa mtambo wa Intercom, na kulipa gharama za kutengeneza na kufunga viegesho vya gari (*car parking shades*).

Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano – Ikulu

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa Kuimarisha Mawasiliano - Ikulu uliidhinishiwa TZS 100 milioni na hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizoingizwa ni TZS 100 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya matumizi. Fedha zote zimetumika kwa kununulia gari la mawasiliano aina ya Toyota VX na vifaa vyake vikiwemo mabomba, inverter, wireless microphones na amplifier.

Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa uliidhinishiwa TZS 150 milioni na hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizoingizwa ni TZS 86.3 milioni sawa na asilimia 57.5 na kutekeleza yafuatayo:-

a) Sera ya Serikali za Mitaa imekamilika. Viliandaliwa jumla ya vikao kumi vya wadau wa sera wakiwemo Makatibu wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Madiwani, Wenyeviti wa Halmashauri na Mabaraza ya Miji, Maofisa wa wizara za SMZ na Taasisi zisizo za kiserikali (*NGO'S*), kwa kukusanya maoni ambayo yalisaidia sana katika kukamilisha sera hiyo.
b) Imeandaa hadidu rejea za kutayarisha Mpango Mkakati.
c) Imeandaa madodoso ya kufanya utafiti unaolenga ukusanyaji wa mapato na uwezo wa kiutendaji katika Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi mingine sita (6) niliyoitaja awali nitaitolea maelezo yake katika Idara husika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mipango Sera na Utafiti imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuimarisha uwezo wa Idara katika kupanga, kuandaa na kuchambua Sera, kufanya tafiti pamoja na kuratibu shughuli za mipango na bajeti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
b) Kufanya uchambuzi wa Sera ya Serikali za Mitaa ili iweze kutekelezeka na kufanya uchambuzi wa Mpango Mkakati wa Chuo cha Mafunzo na kuhakikisha utekelezaji wake.
c) Kuandaa utafiti unaolenga kutanua wigo katika ukusanyaji wa Mapato kutoka Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana na Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
d) Kuratibu na kuandaa ripoti za utekelezaji wa malengo ya bajeti pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015.
e) Kuandaa mfumo shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini kwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
f) Kuimarisha uwezo wa watendaji kitaaluma.
g) Kuimarisha na kutunza kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA).
h) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia watendaji stahiki zao, kununua vitendea kazi vya kisasa vya Ofisini na samani**.**

MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itatekeleza miradi ifuatayo:-

i) Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali (*State Lodges*)
ii) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano - Ikulu
iii) Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa
iv) Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Ushoni cha "Zanzibar *Quality Tailoring*" cha Idara Maalum za SMZ

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itatekeleza miradi ifuatayo:-

v) Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali (*State Lodges*),
vi) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano – Ikulu,
vii) Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa,
viii) Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Ushoni cha "*Zanzibar Quality Tailoring*" cha Idara Maalum za SMZ.

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali *(State Lodges)*

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali utatekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kujenga nyumba mbili za wafanyakazi na walinzi ndani ya eneo la Ikulu ndogo ya Laibon Dar es Salaam.
b) Kuezeka nyumba ya Ikulu ndogo ya Mkoani na kutengeneza kibanda cha walinzi.
c) Kuanza ukarabati mkubwa wa nyumba tatu za Ikulu ya Chake Chake.
d) Kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Serikali ya mapumziko Micheweni. *(Makofi)*

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali unakadiria kutumia shilingi 400/= milioni.

Mradi wa Mawasiliano – Ikulu

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Mawasiliano – Ikulu utatekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kufanya matengenezo ya chumba kwa ajili ya utayarishaji wa vipindi;
b) Kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kurikodia sauti na picha na
c) Kununua mashine za kufanyia uhariri wa vipindi

Mradi wa Mawasiliano - Ikulu unakadiria kutumia shilingi 100/= milioni.

Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa utatekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kupitia na kuunda mipaka mipya ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
b) Kusambaza na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Serikali za Mitaa;
c) Kuunda vikundi kazi vitakavyotumika katika kupitia mfumo wa Kodi na Mapato wa Serikali za Mitaa na Muundo wa Serikali za Mitaa na Utawala;
d) Kupitia na kufanya marekebisho ya Sheria Namba 1 ya mwaka 1998, ya Mamlaka ya Utawala wa Mikoa na Sheria Namba. 3 na 4 ya mwaka 1995 ya Serikali za Mitaa.

Mradi wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa unakadiria kutumia shilingi 150/= milioni.

Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Ushoni
*"Zanzibar Quality Tailoring"*cha Idara Maalum za SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Mradi mpya wa Kukiimarisha Kiwanda cha Ushoni "*Zanzibar Quality Tailoring*" cha Idara Maalum za SMZ unakusudia kukipa uwezo kiwanda hicho kwa kununua vifaa vya kisasa vikiwemo vyarahani na mashine za kufumia. Mradi huu utakapokamilika unategemewa kushona aina zote za Sare za Idara Maalum za SMZ na kuondokana na utaratibu wa kuagizia vifaa hivyo kutoka nje. *(Makofi)*

Mradi wa Kuimarisha Kiwanda cha Ushoni cha Idara Maalum za SMZ unakadiria kutumia shilingi 256/= milioni.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 466.9/= milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 906/= milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kusimamia shughuli za Utawala na Utumishi zikiwemo kusimamia Sheria na Kanuni za Utumishi kwa wafanyakazi, kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi, kusimamia Sheria ya Ununuzi na uondoaji wa mali chakavu za Serikali, kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kusimamia maslahi yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa shilingi 1,858.5/= milioni kwa kazi za kawaida. Fedha hizi zilitumika pia kwa kulipia mishahara ya Ofisi ya Faragha ya Rais, Idara ya Mawasiliano – Ikulu, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, Idara hii iliingiziwa shilingi 1,810.4/= milioni sawa na asilimia 97.4/= ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Idara imenunua zana na samani za ofisi zikiwemo kompyuta sita, vespa moja, meza 13, viti 19, makabati mawili, mafriji manne, mafeni manne, vipoza hewa (*air condition*) vitano, fotokopi mashine moja pamoja na kufanya matengenezo ya ofisi na matengenezo ya magari;

b) Idara imesimamia maslahi ya wafanyakazi wakiwa kazini na baada ya kustaafu kwa kuwalipa maslahi yao;

c) Idara imeendesha vikao sita vya Bodi ya Zabuni na vikao vitatu vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani;

d) Idara imewajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi sita, na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi watatu.

   Aidha Idara imetoa taaluma ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI kwa wafanyakazi 38 wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sambamba na kutoa taaluma inayohusu maadili ya kazi na utunzaji wa siri za ofisi kwa watendaji 45 wa kada ya masjala. Idara pia imeratibu mafunzo kwa watendaji wa Idara zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

e) Idara imetoa motisha kwa wafanyakazi kwa kuwapatia malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi 28, sare kwa wafanyakazi 26 pamoja na kutoa zawadi kwa wafanyakazi bora watatu;

f) Idara imeweka mfumo bora wa usimamizi na utoaji wa taarifa katika uwajibikaji kazini, kwa kuendesha semina ya uandaaji wa taarifa za kiutumishi na Sheria ya Utumishi wa Umma kwa Maofisa Utumishi 35 wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Unguja na Pemba;

g) Idara imefanya uhakiki wa mahitaji ya mafunzo ya wafanyakazi, pamoja na kuandaa mpango wa mafunzo hayo. Kazi hiyo ipo katika hatua za mwisho kukamilika;

h) Idara imepitia majukumu ya kazi ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuyagawa majukumu hayo kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahiki zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani;

b) Kusimamia Sheria ya Manunuzi pamoja na kuratibu vikao vya kamati ya ukaguzi wa ndani;

c) Kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 3 katika ngazi za Shahada ya Uzamili, Shahada na Stashahada katika fani za Uongozi, Utawala na Uhasibu. Muda mfupi

wafanyakazi 2 katika fani za Udereva, na Katibu Mukhtasi. Aidha, Mfanyakazi mmoja kujifunza lugha ya alama;

d) Kuandaa Mafunzo ya Maadili na Kazi za Ofisi ya Rais (Ikulu);

e) Kusimamia upatikanaji wa Hati Miliki za Majengo yote ya Ikulu na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

f) Kutoa taaluma katika masuala mtambuka ikiwemo kujikinga na maambukizo mapya ya UKIMWI na huduma za watu wenye ulemavu;

g) Kuandaa mpango wa matumizi ya Rasilimali watu pamoja na kupitia muundo wa Utumishi na kupandisha daraja watumishi (*scheme of services*);

h) Kufanya uhakiki wa kazi na kutoa nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi na

i) Kukamilisha kufanya uhakiki wa mahitaji ya mafunzo na kuandaa mpango wa mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 1,247.3/= milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MAWASILIANO – IKULU

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano Ikulu ina jukumu la kutoa, kuratibu na kupokea taarifa za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali inayolenga kuwaletea maendeleo wananchi. Aidha, Idara hii ina jukumu la kuthibitisha na kuhakikisha kuwa taarifa zote za Mhe. Rais zinazotolewa kwa wananchi na wadau wengine ni sahihi na zinatolewa kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu mengine ni kutambua fursa ambazo zinaweza kutumika ili kuimarisha mawasiliano baina ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Taasisi za Serikali na wananchi pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wanaarifiwa kila hatua za yale yote yaliyoahidiwa kwao na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Lengo ni kuweka taswira nzuri baina ya Mhe. Rais wa Zanzibar, wananchi na washirika wengine wa maendeleo. Aidha, Idara ya Mawasiliano ina jukumu la kuandaa utaratibu utakaomuwezesha Mhe. Rais kukutana na kuzungumza na wahariri na waandishi wa habari juu ya mambo yanayohusu Zanzibar na maendeleo yake, na kwa mnasaba huo huzungumza na wananchi kila baada ya miezi mitatu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano Ikulu, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa shilingi 80.7/= milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Idara hii iliingiziwa shilingi 53.7/= milioni sawa na asilimia 66.5 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imeandaa vipindi 25 vya televisheni kuhusu utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama zilivyoelezwa kwenye Ilani ya Chama Tawala cha CCM pamoja na ahadi alizotoa wakati wa ziara za Mikoani;

b) Imetoa mafunzo kwa maafisa mawasiliano wa Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mafunzo hayo yaliyotolewa ni juu ya wajibu wa maafisa mawasiliano katika kutoa taarifa za serikali kwa wananchi;

c) Imewapatia mafunzo wafanyakazi watatu ambapo mfanyakazi mmoja anasomea fani ya ukatibu muhtasi, mmoja kujifunza programu maalum ya uhifadhi wa taarifa kwenye kompyuta, na mfanyakazi mwengine anasomea taaluma ya kazi kwa vijana katika Chuo cha Mwalimu Nyerere Tawi la Zanzibar;

d) Imechapisha matoleo matatu ya majarida ya Ikulu na toleo moja la kipeperushi lenye ujumbe wa mambo kumi ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa na watendaji pamoja na wananchi;

e) Imetembelea na kukutana na wakuu na waandishi wa vyombo mbali mbali vya ndani na nje ya Zanzibar kwa lengo la kuimarisha mawasiliano na
f) Imenunua vitendea kazi vikiwemo vifaa vya kuandikia, seti ya kompyuta na vifaa vya kutengenezea gari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mawasiliano Ikulu imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kulinda na kuendeleza taswira ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutoa habari sahihi na kwa wakati;
b) Kuratibu mikutano ya Mhe. Rais na Vyombo vya Habari**;**
c) Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi;
d) Kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, wafanyakazi wawili katika ngazi za Shahada na Cheti katika fani za Teknolojia ya Habari na Programu ya Kazi kwa Vijana. Muda mfupi mfanyakazi mmoja katika program maalum ya kuchambua habari za Magazeti na
e) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia watendaji stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mawasiliano Ikulu iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 174.9/= milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

KITENGO CHA USALAMA WA SERIKALI (*GSO*) ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*) Zanzibar kimeanzishwa kwa Sheria Namba 3 ya mwaka 1983 na kinatekeleza majukumu yake sambamba na Sheria ya Utumishi wa Umma "*Public Service Act* Nam. 2 ya mwaka 2011". Sheria hizi zimeainisha majukumu ya Kitengo cha Usalama wa Serikali kuwa ni udhibiti wa shughuli za Usalama wa Serikali na Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*) Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kiliidhinishiwa shilingi 49.8/= milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, kitengo hiki kiliingiziwa shilingi 27.5/= milioni sawa na asilimia 55.2 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kimefanya upekuzi kwa watumishi 554 kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali na kutoa ushauri unaofaa baada ya upekuzi huo;
b) Kimekagua jumla ya Taasisi 12 za Serikali katika kuangalia utunzaji wa siri za Serikali (idadi ya Taasisi zilizokaguliwa zinaonekana katika Kiambatanisho Namba 5);
c) Kimeweza kufanya ukaguzi wa Taasisi 12 zenye vituo muhimu katika kuangalia usalama wa vituo hivyo na kupendekeza njia bora za kudumisha usalama na
d) Kitengo kilitoa mafunzo ya Usalama na kuwaelimisha watumishi wa Taasisi nane ambazo zipo katika Kiambatanisho Namba 6.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*) kimekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kufanya upekuzi wa awali na upekuzi endelevu kwa watumishi 500 wa Serikali;
b) Kuendeleza ushirikiano na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kusimamia kanuni za utumishi na kuhakikisha zinatekelezwa hususan zile zinazogusa usalama wa mali na nyaraka za serikali;
c) Kuendelea kushirikiana na Maafisa Usalama wa Taasisi za Serikali katika kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa sheria zinazohusu utunzaji wa siri za serikali na
d) Kuweka mazingira bora ya kazi na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*) kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 54.9 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za utawala na huduma za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zinazofanyika Pemba.

Aidha, Ofisi hii inaratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Kimataifa wanaotembelea Pemba. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu usimamizi wa nyumba za Ikulu. Vile vile, Ofisi ya Afisa Mdhamini inaratibu shughuli za Idara Maalum za SMZ pamoja na Mamlaka za Serikali za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa shilingi 365.5/= milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Ofisi hii iliingiziwa shilingi 322.5/= milioni sawa na asilimia 88.2 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imeratibu ziara sita za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ziara moja ya Mhe. Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kisiwani Pemba.
b) Imewapatia nafasi za mafunzo wafanyakazi sita, wanne katika ngazi ya stashahada, wawili katika ngazi ya cheti na mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo ya muda mfupi Tanzania Bara.
c) Imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 50 juu ya umuhimu wa kupima VVU, ili kujua afya zao, kubadili tabia na kuacha unyanyapaa kwa wafanyakazi wanaoishi na VVU pamoja na maradhi ya UKIMWI.
d) Wafanyakazi 16 wamepatiwa mafunzo ya siku mbili (2) juu ya umuhimu wa Daftari la Kudumu la Mali za Serikali (*Fixed Asset Register*).
e) Imefanya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Afisa ya Mdhamini na imenunua vitendea kazi vikiwemo vespa moja, kompyuta mbili na samani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa upande wa Pemba ikiwemo ziara za Viongozi Wakuu.
b) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi saba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika kiwango na fani tofauti.
c) Kufanya matengenezo madogo ya jengo la Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.
d) Kuratibu mafunzo ya kujenga uwezo wa Taasisi za Mabaraza ya Miji na Halmashauri katika kuzidi kuinua kiwango cha ukusanyaji mapato na uibuaji wa miradi ya jamii.
e) Kuendelea kuwajengea uelewa wafanyakazi juu hatua za mapambano ya UKIMWI, utunzaji mazingira na uimarishaji wa utawala bora sehemu za kazi.
f) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahiki zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 462.4/= milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zikijumuisha shilingi 115.7/= kwa ajili ya ruzuku za Halmashauri za Pemba.

OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imeanzishwa rasmi mwaka 2005 chini ya Sheria Namba 7 mwaka 2005 ikiwa na wajibu wa kuwasajili na kuwapatia vitambulisho Wazanzibari wakaazi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Aidha, ofisi ina wajibu wa kutunza taarifa zote za wananchi zilizokusanywa kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa shilingi 1,248/= milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 150/= milioni kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi

2012, Ofisi hii iliingiziwa shilingi 886.9/= milioni sawa na asilimia 71.1 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 150/= milioni sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imesajili Wazanzibari wakaazi 10,578 waliotimiza masharti ya usajili na kutengeneza upya vitambulisho 3,932 ambavyo vimemaliza muda wake wa matumizi na kuvigawa kwa wahusika.
b) Imetengeneza vitambulisho 10,393 vya wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zake ambazo zimewasilisha taarifa za wafanyakazi kwa kutengenezewa vitambulisho.
c) Imeandaa Rasimu ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili Namba 7 ya 2005, ili kuruhusu utoaji wa vitambulisho vya wageni wanaoishi nchini, rasimu hiyo tayari imeshapita Baraza la Mapinduzi na inasubiri kuwasilishwa kwenye Baraza lako Tukufu. Taratibu zote za kiutendaji zimekamilika ikiwa ni pamoja na mfumo wa utengenezaji wa vitambulisho hivyo, pamoja na fomu za maombi ya usajili.
d) Ofisi imerusha hewani jumla ya vipindi 18 kupitia Shirika la Utangazaji la *ZBC*, juu ya kuelimisha matumizi bora ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.
e) Imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi 9 kwa kuwasomesha katika viwango vya Vyeti na Stashahada pamoja na Shahada ndani na nje ya nchi.
f) Imenunua kompyuta 7 mpya kwa kubadilisha za zamani zilizokwisha muda wake.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyengine zilizofanywa na Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ni kufanyiwa ukaguzi wa kimataifa kwa mara ya sita juu ya muundo, mfumo na taratibu zake za kiutendaji na imethibitishwa kuwa inaendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vilivyowekwa na *International Standard Organisation* na *IQ Net.*

Aidha, imekarabati vyumba viwili katika jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kati, ili Ofisi yake ya Tunguu iweze kuhamia Dunga kuondosha usumbufu wa kufuata huduma Tunguu katika jengo la Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kuwasajili Wazanzibari Wakaazi 10,500 wanaotimiza masharti ya usajili na kuwapatia Vitambulisho.
b) Kuendelea kutengeneza vitambulisho vipya kwa ajili ya kubadilisha vitambulisho vilivyomaliza muda wake wa matumizi. Pia kuwabadilishia vitambulisho vipya vya Wazanzibari Wakaazi walioomba kufanya mabadiliko halali ya taarifa zao binafsi na waliopoteza.
c) Kuendelea kubadilisha na kutengeneza vitambulisho vya wafanyakazi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kuzingatia muundo mpya wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
d) Kuanza kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum (*Residence Permit*) na kutunza taarifa zilizokusanywa kwa ajili hiyo katika *data base* ya Serikali mara baada ya marekebisho ya Sheria ya Usajili Namba 7 ya mwaka 2005 kupitishwa na Baraza la Wawakilishi.
e) Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora na sahihi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kama ambavyo sera inavyoelekeza.
f) Kuendelea kuwajengea uwezo kielimu wafanyakazi wa ofisi.
g) Kuendelea kununua malighafi za utengenezaji wa vitambulisho, sambamba na kubadilisha mitambo iliyochakaa na kwisha muda wake zikiwemo seti za kupigia picha (*kits*).
h) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 1,593/= milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA SHUGHULI ZA WAZANZIBARI WANAOISHI NCHI ZA NJE

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje, imeendelea na utekelezaji wa majukumu ya kuimarisha Mtangamano wa Kikanda kwa kuratibu ushiriki wa sekta mbali mbali za Zanzibar katika mikutano hiyo, na kuhakikisha kwamba Zanzibar inatumia fursa za kiuchumi

zinazotokana na Jumuia ya Afrika Mashariki, Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Jumuia nyengine za Kikanda.

Aidha, imeendelea kusimamia uimarishaji wa ushirikiano mwema na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa pamoja na kuratibu shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje, na kuwashajihisha Wazanzibari hao kushiriki katika kuiletea Zanzibar maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa shilingi 671/= milioni kwa kazi za kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi 2012, ofisi hii iliingiziwa shilingi 554/= milioni sawa na asilimia 82.6 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Iliratibu, ilishiriki na kufuatilia shughuli za Ushirikiano wa Jumuia mbali mbali za Kikanda na kuwawezesha wataalamu wa Sekta mbali mbali kuhudhuria katika mikutano ya Kikanda na ya Kimataifa katika nchi za Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, India, Angola na Mauritius.
b) Iliendelea kuimarisha juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uhusiano mwema na Nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa. Idara ilikutana na Wawakilishi wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), na wameonesha nia ya kusaidia kuzijengea uwezo Kitengo cha *Diaspora* na Idara Maalum za SMZ.
c) Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitayarisha semina juu ya fursa na faida zitokanazo na Soko la Pamoja la Jumuia ya Afrika Mashariki kwa wafanyabiashara na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.
d) Iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika vikao vya matayarisho ya mikutano ya Jumuia mbali mbali za kikanda na Kimataifa kwa lengo la kupata msimamo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mikutano hiyo
e) Ilitayarisha Mpango Mkakati wa *Diaspora*.
f) Maafisa wa Kitengo cha *Diaspora* na wadau wengine wamefanya ziara katika nchi za Falme za Kiarabu (Oman na Dubai) kwa lengo la kukutana na Wazanzibari, ili kuwashajihisha kushiriki katika kuchangia maendeleo ya Zanzibar.
g) Iliitangaza dhana ya *Diaspora* kwa kutayarisha vipindi vilivyorushwa hewani na *ZBC* TV na Redio, na watendaji walihudhuria mikutano ya Diaspora iliyofanyika Uganda na Afrika ya Kusini.
h)

Jumuia ya Afrika Mashariki

Mhe. Mwenyekiti, mkutano wa 13 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki ulifanyika tarehe 30 Novemba, 2011 nchini Burundi. Mkutano huo uliichagua Jamhuri ya Kenya kuwa Mwenyekiti wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Miongoni mwa mambo muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni kupitisha Sera na Mkakati wa Viwanda wa Jumuia ya Afrika Mashariki, Itifaki ya kuzuia na kupambana na rushwa, Itifaki ya ushirikiano wa ulinzi, Himaya moja ya Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki na maombi ya Jamhuri ya Sudan na Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuia ya Afrika Mashariki.

Wakuu wa Nchi walikubaliana kuwa Jamhuri ya Sudan haiwezi kuwa mwanachama kutokana na kutotimiza vigezo vya kujiunga na Jumuia hiyo. Kwa upande wa Jamhuri ya Sudan Kusini, Wakuu wa Nchi waliliagiza Baraza la Mawaziri kupitia vigezo na baadae wawasilishe maoni yao katika mkutano wa 10 wa dharura wa Wakuu hao. Wakati huo huo, Wakuu wa Nchi waliunga mkono hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Kenya ndani ya Somalia, ili kulinda amani, usalama na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki ulifanyika tarehe 28 Aprili, 2012. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulimchagua Naibu Katibu Mkuu Mheshimiwa Jesca Eriyo kutoka Uganda na kumuongezea muda wa kuwa Naibu Katibu Mkuu Mhe. Jean Claude Nsengiyumva kutoka Burundi.

Aidha, mkutano huo ulipokea taarifa ya Baraza la Mawaziri katika hatua zilizofikiwa katika Himaya moja ya Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki na taarifa ya vigezo vya Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuia. Katika mkutano huo, Baraza la Mawaziri liliagizwa kuharakisha mchakato wa kuangalia vigezo iwapo Jamhuri ya

Sudan Kusini inaweza kujiunga na Jumuia. Hata hivyo, Wakuu wa Nchi walisikitishwa na mgogoro unaoendelea kati ya Jamhuri ya Sudan na Jamhuri ya Sudan Kusini.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa Soko la Pamoja la Jumuia ya Afrika Mashariki bado unasuasua. Katika mkutano wa 15 wa Kisekta wa Baraza la Mawaziri uliofanyika Kampala mwezi Januari 2012, nchi wanachama walielezea wasiwasi wao wa kutoridhishwa na mwenendo wa ratiba ya kufungua maeneo yaliyokubalika, pamoja na marekebisho ya Sheria za Nchi katika utekelezaji wa Soko la Pamoja.

Katika kulipatia ufumbuzi suala hili, Baraza la Kisekta liliamua kuunda Kamati za Kitaifa za utekelezaji wa Soko la Pamoja kwa kila Nchi Mwanachama. Katika Kamati hiyo, Zanzibar inawakilishwa na Makatibu Wakuu watatu kutoka Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, majadiliano ya Itifaki ya Umoja wa Sarafu yanaendelea katika ngazi za wataalamu. Vikao saba vimefanyika na jumla ya Ibara 59 za Itifaki hiyo zimejadiliwa.Mambo muhimu ambayo wataalamu wamekubaliana ni pamoja na Nchi mwanachama kujiunga na Umoja wa Sarafu pale tu itakapotimiza vigezo vya kufanya hivyo. Aidha, majadiliano ya Eneo Huru la Biashara la Utatu (*COMESA*, *EAC* na *SADC*) yataanza rasmi mwezi wa Agosti 2012.

Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2011/2012, Soko hili litakuwa ni kubwa lenye jumla ya nchi 26 na idadi ya watu isiyopungua 600 milioni. Jumuia ya Afrika Mashariki imeamua kuingia katika majadiliano hayo kwa pamoja – *Regional Economic Community (REC)*. Mambo yatakayojadiliwa ni Uasili wa Bidhaa, Uondoshaji wa Vikwazo vya Biashara na Ushirikiano wa Kiforodha.

Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Bara la Afrika (SADC)

Mhe. Mwenyekiti, mkutano wa 31 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini Mwa Afrika ulifanyika tarehe 17 Agosti, 2011 nchini Angola. Mkutano huo ulimchagua Mhe. Jos□e Eduardo do Santos Rais wa Jamhuri ya Angola kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo. Pia mkutano huo ulimchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama. Mkutano huo ulipokea taarifa ya hali ya kisiasa, ulinzi na usalama katika eneo la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Bara la Afrika. Kwa ujumla, wakuu hao waliridhika na hali hiyo, hata hivyo walisisitiza migogoro ya nchi za Lesotho, Madagascar na Zimbabwe iendelee kutatuliwa. Aidha, mkutano huo ulizungumzia kuhusu maendeleo ya Miundombinu ya Nishati na ikaagiza uharakishaji wa Mpango Mkuu wa Miundombinu katika Nchi za SADC.

Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (*IOR-ARC*)

Mhe. Mwenyekiti, mkutano wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (*IOR-ARC*) unaoshirikisha nchi 19 wanachama wa Jumuiya hiyo ulifanyika nchini India – Bungalore tarehe 15 Novemba 2011. Katika mkutano huo, India iliteuliwa kuwa mwenyekiti na Balozi K.V Bhagirath kutoka India kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo. Mkutano huo ulizungumzia mambo mbali mbali yakiwemo biashara, uwekezaji, uharamia, taaluma, mashirikiano katika nyanja za Sayansi na teknologia, utamaduni, utalii na kubadilishana utaalamu kwenye maeneo ambayo nchi hizi zina maslahi ya aina moja. Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla zinaweza kufaidika sana na fursa nyingi zilizomo katika Jumuiya ya *IOR – ARC* hasa katika maeneo ya Utalii na uvuvi.

Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (*Diaspora*)

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari wanaoishi nchi za nje imetayarisha Mpango Mkakati wa miaka mitano ambao unatoa muongozo wa utekelezaji wa shughuli zitakazoimarisha na kuwashajihisha *Diaspora*. Utekelezaji wa mkakati huu, utapelekea upatikanaji wa michango na uekezaji katika sekta za kijamii na kiuchumi kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuwatafuta na kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje, Idara imeendelea kuwa karibu na kuwasiliana na Jumuiya mbali mbali za Wazanzibari zikiwemo *ZAWA* – Uingereza, *ZACADIA, ZANCAN* za Canada na nyenginezo. Matokeo ya ukaribu na mawasiliano haya yamepelekea Wazanzibari

wanaoishi Nchi za Nje kuitikia wito wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuekeza katika sekta za kijamii, elimu na afya. Kwa mfano ujenzi wa madarasa matano katika skuli ya Unguja Ukuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendeleza na kuimarisha juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uhusiano mwema na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa.
b) Kuwawezesha wataalamu wa Zanzibar kushiriki katika mikutano ya kikanda na ya kimataifa.
c) Kutayarisha Sera ya *Diaspora*.
d) Kuaanda mazingira bora yatakayowawezesha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kuweza kuekeza kwa urahisi ndani ya Zanzibar.
e) Kuanzisha mfumo wa mawasiliano utakaowawezesha wanadiaspora kupeana taarifa mbali mbali.
f) Kushirikiana kwa karibu na Idara inayoshughulikia Watanzania Waliopo Nje (*Diaspora*) ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.
g) Kuijengea uwezo Idara pamoja na watendaji wake.
h) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia watendaji stahili zao**.**
i) Kuelimisha masuala mtambuka yanayohusiana na jinsi ya kujikinga na maradhi yenye kuambukiza pamoja na UKIMWI kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 884.0 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kufuatilia na kuratibu uendeshaji wa shughuli zote za Mamlaka ya utawala wa Serikali za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, inaratibu, kutoa maelekezo ya kitaalamu na kuzishauri Serikali hizo juu ya utendaji bora wa kazi zao za kila siku sambamba na kusimamia utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo, uwajibikaji na uhusiano bora wa kisekta. Idara hii pia inajukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria katika mamlaka za Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa TZS 200 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Idara hii iliingiziwa TZS 114.9 milioni sawa na asilimia 57.5 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Idara kwa kushirikiana na watendaji wa Idara ya Mazingira imefanya ziara katika maeneo ya Muambe, Kangagani na Micheweni kuangalia uharibifu na utunzaji wa Mazingira na kushauri njia bora ya kudhibiti uharibifu wa Mazingira.
b) Mafunzo na mikutano ya kitaalamu ilifanyika katika Serikali za Mitaa na matokeo yake yameweza kuongeza mapato, udhibiti na usimamizi wa fedha. Mapato ya Serikali za Mitaa yamefikia wastani wa asilimia 102 ya lengo la mwaka.
c) Watendaji na Madiwani katika Serikali za Mitaa wameweza kufahamu mipaka ya kazi zao na wajibu wao kwa jamii.
d) Semina za mafunzo zenye lengo la kuimarisha mahusiano ya kiutendaji kati ya wananchi, Madiwani na watendaji zimefanyika kwa ufanisi na kwa sasa Madiwani na Watendaji wanafanyakazi kwa mashirikiano.
e) Idara kupitia Mabaraza ya Halmashauri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekamilisha utayarishaji wa Sheria ndogo ndogo za Serikali za Mitaa. Sheria hizo ni pamoja na Kanuni za Madiwani, Kanuni za udhibiti wa wanyama na uzoaji taka.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea na azma yake ya kuziendeleza huduma za Mijini kupitia Mradi wa Kuimarisha Huduma za Mjini (*ZUSP*). Katika kutekeleza hatua ya kwanza na ya pili, Mradi huu umeshatekeleza shughuli zifuatazo:-

a) Kutafuta mshauri mwelekezi (*Consultant*) wa usimamizi wa kazi za ukarabati na ujenzi wa misingi ya maji ya mvua kwa ajili ya maandalizi ya kutafuta Mkandarasi wa ujenzi. Maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni Ziwa la Sebleni, Ziwa la Mtumwajeni, Ziwa la Kwa-binti Amrani, Ziwa la Mwantenga, Kwamtipura, Kilima hewa, Karakana, Sogea, Mpendae, Jan'gombe (*Botanical garden*), Uwanja wa Demokrasia na Shauri Moyo.
b) Serikali imewasilisha ripoti katika Benki ya Dunia kwa ajili ya kuthibitishwa ili hatua za kumtafuta Mjenzi wa silabu193 za kuweka makontena ya kuwekea taka. Aidha, ripoti ya kutafuta kampuni ya kununua gari za kubebea taka na maji machafu pamoja na taa za barabarani tayari imewasilishwa Benki ya Dunia kwa kuthibitishwa.
c) Serikali kupitia Mradi wa *ZUSP* imenunua baadhi ya vifaa na tayari vimeshafika Zanzibar na vengine vinatarajiwa kufika hivi karibu; vitu hivyo ni gari 5 za wakuu wa Idara za Manispaa, Vespa 10 za Manispaa, Vespa 15 na gari 6 za kubebea taka kwa ajili ya Mabaraza ya Miji Pemba, Honda 3, gari moja ya Idara ya Mipango Miji na gari moja ya Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
d) Serikali imeshatayarisha hadudi rejea za kumtafuta mshauri wa kusimamia uwekaji wa taa za barabarani na zimeshawasilishwa Benki ya Dunia kwa kuthibitishwa. Maeneo yatakayonufaika kutokana na mpango huu ni Mwanakwerekwe hadi Amani, Amani hadi Mwembeladu, Magomeni hadi Kariakoo, Kikwajuni hadi Baraza la Wawakilishi la zamani, Barabara ya Mazizini lilipo jengo la Bodi ya Mapato ya Zanzibar, maeneo ya Kiponda, Shangani na Mkunazini.
e) Serikali imeshatayarisha hadudi rejea za kumtafuta mjenzi wa utanuzi wa ukuta unaopita pembezoni mwa pwani ya Forodhani na zimeshawasilishwa Benki ya Dunia kwa kuthibitishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuimarisha Uratibu wa Serikali za Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa Pamoja na kuimarisha ushirikiano na *TAMISEMI* Tanzania Bara
b) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Serikali za Mitaa itakayowezesha ushirikishaji wa wananchi.
c) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.
d) Kufanya uchambuzi wa ripoti za utekelezaji wa Taasisi za Serikali za Mitaa.
e) Kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa maafisa watano katika fani za mipango, utawala bora, utawala na rasilimali watu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kupanga kutekeleza malengo niliyoyataja hapo juu, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaratibu kwa karibu utekelezaji wa Mradi wa *ZUSP*. Shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

a) Kufanya matengenezo ya ujenzi wa misingi ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 3,339 katika maeneo ya Uwanja wa Mnazi Mmoja, Magogoni, Amani, Sebleni na Sogea.
b) Ujenzi wa slabu 78 za kuwekea taka katika maeneo ya Mji Mkongwe na Ng'ambo.
c) Matengenezo na uwekaji wa taa za barabarani katika maeneo ya mjini yakiwemo maeneo ya mji Mkongwe.
d) Kutafuta taarifa muhimu na kufanya tathmini ya taarifa za vyanzo vya mapato, miundo ya utumishi, kanuni na sheria ziliopo kwa ajili ya kupendekeza na kutoa mikakati ya utekelezaji kwa lengo la kuinua uwezo wa utendaji wa Baraza la Manispaa (*Institutional strengthening*).
e) Kufanya Ubunifu (*structural design*) na tathmini ya gharama za ujenzi wa utanuzi wa ukuta wa pwani ya Forodhani wenye urefu wa mita 340 kwa ajili ya matayarisho ya vitabu vya zabuni ya kumtafuta mkandarasi wa ujenzi.
f) Kuibua miradi midogo midogo na kuifanyia tathmini na kutayarisha vitabu vya zabuni ya kutafuta mkandarasi na kuandaa mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa Mabaraza ya Miji ya Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 1,992.4 milioni. Kati ya hizo TZS 701.4 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zikijumuisha TZS 255 milioni kwa ajili ya ruzuku za Halmashauri za Wilaya za Unguja. Aidha, ruzuku ya Baraza la Manispaa ni TZS 1,291 milioni.

MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mikoa zina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo, kutafsiri sera, sheria pamoja na kuratibu amani na utulivu.

MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 uliidhinishiwa TZS 744 milioni kwa matumizi ya kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Mkoa huu uliingiziwa TZS 637 milioni sawa na asilimia 85.6 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kupitia kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa, Wilaya na Shehia, Mkoa ulisimamia hali ya ulinzi na usalama kwa kufuatilia matukio mbali mbali yaliyoripotiwa, kutoa elimu kwa wananchi juu ya suala la ulinzi na usalama.
b) Mkoa kwa kushirikiana na sekta mbali mbali umefanikisha kampeni za chanjo kwa watoto, zoezi la upigaji dawa majumbani, ugawaji wa vyandarua, uandikishaji wa watoto waliofikia umri wa kuanza skuli, ujenzi wa madarasa mapya, kufanikisha mazingira mazuri ya mitihani ya Kitaifa, uhamasishaji wa kilimo cha mazao ya biashara na matunda.

   Aidha, umesimamia ugawaji wa misaada ya wazee wasiojiweza ambapo jumla ya wazee 2,071 wamepatiwa misaada hiyo. Kati ya hao 1,619 kutoka Wilaya ya Mjini na 452 kutoka Wilaya ya Magharibi. Mkoa umeshiriki kampeni za kupiga vita udhalilishaji wa wanawake na watoto. Jumla vijana 4,159 wameorodheshwa na Mkoa kwa lengo la kuwatafutia ajira, kati ya hao wanaume ni 2,328 na wanawake ni 1,831.
c) Wafanyakazi 12 wamepatiwa elimu katika ngazi ya stashahada ya uzamili, stashahada na cheti kwa fani za utawala wa umma, utunzaji wa kumbukumbu, uhandisi wa magari na uhasibu.
d) Jumla ya kamati 37 za maendeleo za Shehia zimepatiwa mafunzo ya uandaaji wa mipango na usimamizi wa fedha za miradi. Pia Masheha 72 wamepatiwa mafunzo ya utawala bora.
e) Wafanyakazi 29 na Masheha 28 wamepatiwa mafunzo ya uelewa wa usawa wa jinsia. Wafanyakazi 36 na Shehia 27 wamepatiwa mafunzo ya UKIMWI na unyanyapaa. Aidha, ziara zimefanyika kufuatilia uharibifu wa mazingira pamoja na kufanya vikao kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Bazara la Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kuzungumzia usafi wa mji na uzururaji wa wanyama.
f) Mkoa umeratibu na kusimamia miradi mbali mbali inayoanzishwa na wananchi na kuona utekelezaji wake. Kiambatanisho Namba 7 kinatoa ufafanuzi wa miradi iliyotekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Mkoa wa Mjini Magharibi umekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya sekta mbali mbali.
b) Kuratibu na kusimamia shughuli za ulinzi na usalama.
c) Kutatua migogoro ya ardhi inayoukabili Mkoa kuanzia ngazi ya Shehia, Halmashauri, Baraza la Manispaa, Wilaya na Mkoa pamoja na kushirikiana na Wizara husika.
d) Kusimamia uimarishaji wa usafi wa mji, udhibiti wa wanyama wanaozurura na udhibiti wa uchimbaji holela wa mchanga. Shughuli hizi zitafanywa kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.
e) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Ofisi za Mkoa lililopo Amani na kufanya matengenezo ya jengo la Ofisi za Mkoa Vuga.
f) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi

g) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi.
h) Kuzijengea uwezo Kamati mbali mbali zinazosimamia maendeleo ya Shehia.
i) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.
j) Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI, utunzaji wa mazingira na usawa wa jinsia.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Mijini Magharibi uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,099 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 uliidhinishiwa TZS 774 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 60 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Mkoa huu uliingiziwa TZS 711.8 milioni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na TZS 60 milioni sawa na asilimia 100 ya kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Umesimamia shughuli za ulinzi na usalama kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vilivyomo Mkoani.
b) Mkoa umeendelea na ujenzi wa Ofisi ya Mkoa
c) Mkoa umefanya utafiti juu ya sababu zinazopelekea vitendo vya ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia. Ambapo utafiti umebainisha kuwa vijana kushiriki katika vikundi hatarishi na utumiaji wa madawa ya kulevya ni chanzo kikuu cha ubakaji na unyanyasaji kijinsia.
d) Kwa kushirikiana na Ofisi za kilimo za Mkoa na Wilaya, Mkoa uliwashajihisha wananchi kulima kilimo cha juu na mabondeni kwa mazao ya chakula na biashara ili kuhakikisha uhakika wa chakula, kuongeza kipato na kupunguza umasikini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012 Mkoa umelima jumla ya ekari 22,229 sawa na asilimia 37.25 ya lengo, kati ya hizo ekari 6,429 za mpunga, kilimo cha juu ekari 15,800 na kilimo cha maweni ni ekari 21,351.
e) Kwa upande wa mazao ya biashara, misitu na matunda, hadi kufikia mwezi Machi, 2012 Mkoa umeweza kuatika jumla ya miche 239,000 sawa na asilimia 77.59. Kati ya hiyo, mikarafuu 62,000, miche ya misitu ni jumla 99,000 na miche ya mazao ya matunda na biashara ni miche 78,000.
f) Mkoa umeshajihisha viongozi na wananchi kujenga jumla ya madarasa 39 na kutoa elimu kwa Wazazi jinsi ya kuondoa tatizo la kutofaulu kwa wanafunzi.
g) Mkoa umewashajihisha wananchi juu ya umuhimu wa usafi wa mazingira, chanjo za watoto, kujikinga na malaria. Pia usimamizi na ushajihishaji wa uvuvi, upatikanaji wa maji safi na salama, utawala bora ulifanyika kwa mafanikio makubwa.
h) Mkoa ulisimamia matayarisho ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja kwa kununua kiwanja na kukisafisha.
i) Mkoa ulikarabati nyumba ya Mkuu wa Mkoa kwa kuezeka paa jipya, ukarabati wa madirisha na miundombinu ya umeme.
j) Jumla ya wafanyakazi 8 walijengewa uwezo kwa viwango tofauti katika fani za Kompyuta wafanyakazi wawili, Utawala (cheti) mfanyakazi mmoja, Utawala (Diploma) wafanyakazi watatu, Mipango (*PG*) mfanyakazi mmoja na Shahada ya kwanza mfanyakazi mmoja.
k) Umetoa elimu ya kijikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI na uelewa wa jinsia

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Mkoa wa Kaskazini Unguja umekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kusimamia shughuli za Ulinzi na Usalama.
b) Ukamilishaji wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuanza ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya
c) Kuandaa Mpango kazi wa Mkoa
d) Kuendeleza juhudi za kupunguza migogoro ya ardhi kwa kushirikiana na wizara husika pamoja na wadau wengine zikiwemo Halmashauri za wilaya na jamii yenyewe**.**
e) Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo.
f) Kuratibu na kusimamia malengo ya sekta mbali mbali.
g) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.
h) Kuwajengea uwezo wafanyakazi 10 kwa kuwapeleka masomoni katika ngazi za cheti na Stashahada katika fani za Mipango Vijijini na Utawala na Uendeshaji
i) Kuratibu shughuli mtambuka ikiwemo Ukimwi na jinsia.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,083 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Unguja, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 uliidhinishiwa TZS 761 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 20 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Mkoa huu uliingiziwa TZS 642.3 milioni sawa na asilimia 84.4 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na TZS 20 milioni sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Mkoa kwa kushirikiana na Kamati za ulinzi na usalama umeweka hali ya utulivu na amani kwa kuwashajihisha wananchi kuunda Kamati za Polisi shirikishi jamii ambapo Shehia zote 61 za Mkoa zimeshaunda Kamati hizo. Aidha, jumla ya vikao 36 vya ulinzi na usalama vilifanyika.
b) Mkoa kwa mashirikiano na Wilaya zake umeratibu na kusimamia utekelezaji wa sekta mbali mbali kama vile ujenzi wa ukumbi wa skuli ya Sekondari ya Makunduchi, ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba ya walimu Charawe kwa kiwango cha uezekaji, umalizaji wa nyumba za madaktari, ukamilishaji wa majengo ya madarasa matano kwa skuli za Kidimni, Miwaleni, Unguja Ukuu Msingi, Kiboje na Ndijani Mseweni kwa hatua ya utiwaji plasta pamoja na umaliziaji wa ujenzi wa skuli za Mwera Sekondari, Ubago, Mtende Sekondari na Jumbi.
c) Mkoa umeratibu zoezi la Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa chanjo kwa watoto 17,340 chini ya umri wa miaka mitano, zoezi la utoaji wa vyandarua 56,888 na upigaji wa dawa ya malaria katika nyumba 20,252.
d) Umewapatia Masheha 61 mafunzo ya utawala bora kwa kuendesha semina ili kuongeza uwajibikaji na utoaji wa huduma kwa jamii.
e) Mkoa umeweza kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kiwango cha utiaji wa rangi, shata na viyoo vya madirisha, feni, viyoyozi kwa baadhi ya vyumba pamoja na mageti ya nje.
f) Umefanya matengenezo madogo madogo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini kwa kutia rangi.
g) Umeanza matayarisho ya ujenzi wa Ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya ya Kati ambapo hatua ya kupata hati miliki na kusafishwa eneo imekamilika.
h) Wafanyakazi wanne wa Mkoa wanaendelea kupatiwa mafunzo katika ngazi ya cheti, Diploma na Shahada ya pili ndani ya nchi katika fani za usimamizi wa ofisi na Utawala.
i) Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya zake umewapatia wafanyakazi wake semina juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI. Jumla ya wafanyakazi 113 wamepatiwa mafunzo hayo.
j) Mkoa kwa kushirikiana na maafisa husika umehamasisha miradi mbali mbali ikiwemo ya kijamii na vikundi ili kuwa endelevu. Jumla ya miradi 25 ya Mkoa imefanyiwa ukaguzi ikiwemo miradi ya kilimo, ufugaji, vyama vya ushirika (*SACCOS*), wajasiriamali na wakulima wa mwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Mkoa wa Kusini Unguja umekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za ulinzi na usalama.
b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya sekta mbali mbali zilizomo ndani ya Mkoa kama vile sekta ya elimu, kilimo, afya, utawala bora, maji safi na salama, uvuvi, miundombinu, ustawi wa jamii, ufugaji, vijana, wanawake na watoto na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
c) Kuratibu na kusimamia miradi ya wananchi
d) Kuanza ujenzi wa msingi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati.
e) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini kwa kutia vigae na samani za Ofisi.
f) Kumaliza ujenzi wa Uzio wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja na kuweka vigae vya sakafu.
g) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 6 ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Stashahada ya uzamili katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, utawala na uongozi.
h) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.
i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli mtambuka zikiwemo, UKIMWI, jinsia, madawa ya kulevya na ajira za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,064 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

MKOA WA KUSINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Pemba, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 uliidhinishiwa TZS 1,164 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Mkoa huu uliingiziwa TZS 886 milioni sawa na asilimia 76 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-.

a) Umeendelea kusimamia amani, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi pamoja na kudumisha utulivu, ulinzi na usalama wa raia na mali zao.
b) Umeratibu utekelezaji wa shughuli za sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya kilimo, elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, umeme, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana, wanawake na watoto, uvuvi, ufugaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
c) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ujenzi wa uzio wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mkoani.
d) Jumla ya wafanyakazi 14 wa Mkoa na Wilaya zake wanaendelea na mafunzo katika ngazi za Cheti na Stashahada katika fani ya Uongozi wa Rasilimali Watu, Utawala na Biashara.
e) Jumla ya wafanyakazi 77 wa Mkoa na Wilaya zake wamefanyiwa semina juu ya kupambana na UKIMWI na Madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Mkoa wa Kusini Pemba imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kusimamia amani, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi pamoja na kudumisha utulivu, ulinzi na usalama wa raia na mali zao
b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya sekta mbali mbali zilizomo ndani ya Mkoa kama vile sekta ya elimu, kilimo, afya, utawala bora, maji safi na salama, uvuvi, miundombinu, ustawi wa jamii, ufugaji, vijana, wanawake na watoto na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
c) Kujenga nyumba ya Mkuu wa Mkoa, kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake na kununua jengo kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani.
d) Kuratibu shughuli za utekelezaji wa sekta mtambuka zikiwemo UKIMWI, jinsia, madawa ya kulevya na viashiria vya idadi ya watu.
e) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani**.**
f) Kuwajengea uwezo wafanyakazi 6 kwa kuwapatia taaluma katika ngazi tofauti, Cheti katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu, Stashada ya uhasibu, Manunuzi, Utawala na Uongozi na Shahada ya kwanza katika fani ya Uandishi wa habari.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Kusini Pemba uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,741 milioni. Kati ya hizo TZS 1,169 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 572 milioni kwa ajili ya ruzuku za Baraza la Mji la Mkoani na Chake Chake.

MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 uliidhinishiwa TZS 950 milioni kwa matumizi ya kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Mkoa huu uliingiziwa TZS 793 milioni sawa na asilimia 83.5 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Umesimamia amani, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi pamoja na kudumisha utulivu, ulinzi na usalama wa raia na mali zao.
b) Umeratibu na kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa sekta mbali mbali zinazoratibiwa na Mkoa ikiwemo, elimu, afya, maji safi, miundombinu, ufugaji, uvuvi, ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi.
c) Umeweza kuratibu na kusimamia miradi mbali mbali ya maendeleo.

d) Umewajengea uwezo wafanyakazi 5 katika fani za uhasibu, usimamizi wa biashara, rasilimali watu na sayansi ya jamii katika ngazi ya stashahada
e) Umehamasisha jamii juu ya masuala ya UKIMWI na jinsia kwa wafanyakazi na Masheha. Aidha, Mkoa umehamasisha NGOs zinazojihusisha na utowaji wa elimu ya UKIMWI kuendelea kuishajihisha jamii kujikinga na maambukizi mapya na kupunguza unyanyapaa ndani ya jamii.
f) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imefanyiwa matengenezo na ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo Vespa moja na kompyuta mbili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Mkoa wa Kaskazini Pemba imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuratibu na kusimamia shughuli za ulinzi na usalama katika Mkoa.
b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya sekta mbali mbali zikiwemo ya elimu, afya, kilimo, maliasili na mifugo, maendeleo ya jamii na mazingira
c) Kuratibu na kusimamia miradi mbali mbali ya maendeleo ya wananchi
d) Kufanya matengenezo ya nyumba za Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Wilaya.
e) Kuratibu ziara za Viongozi wa Kitaifa na Kimataifa wanaotembelea katika Mkoa
f) Kuendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi 11 wa Ofisi ya Mkoa na Wilaya zake katika ngazi ya Shahada ya kwanza, stashahada na cheti katika fani za usimamizi wa biashara, utawala na uendeshaji, Teknohama, utunzaji wa kumbukumbu, rasilimali watu na uhasibu.
g) Kuratibu na kuhamasisha jamii juu ya masuala mtambuka yakiwemo UKIMWI, jinsia na madawa ya kulevya.
h) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mkoa wa Kaskazini Pemba uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shilingi 1,384 milioni. Kati ya hizo Shilingi 1,109 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 275 milioni kwa ajili ya ruzuku za Baraza la Mji la Wete.

MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zimenzishwa kwa Sheria namba 3 na 4 za mwaka 2004 ya Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi, Mamlaka hizi zinajumuisha Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji pamoja na Halmashauri za Wilaya. Mbali na majukumu mengine ya msingi, Mamlaka hizi ziliweka kipaumbele katika kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vyao. Takwimu za makadirio ya makusanyo ya mapato katika Serikali za Mitaa zinaonesha matumaini mazuri. Wastani wa makusanyo umevuka lengo. Angalia Kiambatanisho Namba 15 kwa ufafanuzi zaidi.

BARAZA LA MANISPAA

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 liliidhinishiwa shilingi 1,041 milioni kwa ajili ya ruzuku na lililenga kukusanya Shilingi 1,094.9 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, Baraza liliingiziwa Shilingi 887.7 milioni sawa na asilimia 85.3 kwa ajili ya ruzuku na limekusanya Shilingi 987 milioni sawa na asilimia 90.1 na kutekeleza yafuatayo:-

a) Limeweza kukusanya na kuzoa taka wastani wa tani 25,920 sawa na asilimia 45 ya taka zote zinazozalishwa mjini.
b) Limesafisha barabara kuu za Mjini kwa kutumia vikundi vya mazingira. Barabara hizo ni pamoja na Mnazimmoja-Uwanja wa ndege, Kiembesamaki-Amani, Amani-Kwa Biziredi, Gulioni-Kilimani na barabara zote za ndani za Mji Mkongwe. Wameweza kusafisha kwa kushirikiana na vokundi hivyo nilivyovitaja.
c) Limeziba paa kwa kutiwa zege Soko la Mwanakwerekwe katika sehemu zilizokuwa zinavuja. Aidha, limerejeshewa huduma ya maji safi kwa kuwekewa mashine moja ya maji katika soko la Mombasa ili kutoa huduma ya maji katika soko hilo. Pia, limeimarisha soko la Mikunguni kwa kuweka huduma za maji safi na matengenezo ya paa.
d) Baraza limekamilisha michoro ya ujenzi wa Ofisi ya Mapato Darajani na kibali cha ujenzi kimeshapatikana kutoka Mji Mkongwe.

e) Limekamilisha kazi za ujenzi wa msingi wenye urefu wa mita 160 pamoja na uwekaji wa taa katika eneo la kituo cha biashara Saateni.
f) Limechangia miradi midogo midogo ya maendeleo ya wananchi katika Wadi zote zilizomo ndani ya Manispaa ya Zanzibar kwa lengo la kupunguza kero za jamii kwa kuchangia vifaa vya upatikanaji wa maji safi, ujenzi wa madarasa ya skuli na ujenzi wa vyoo
g) Limefanya matengenezo madogo katika msingi wa maji machafu wa Mpendae na wa Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui pamoja na matengenezo ya msingi wa Kwamtipura.
h) Limewajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi sita katika fani ya ukaguzi wa hesabu za ndani, mabadiliko ya tabianchi, usafi wa Mji pamoja na ukaguzi na usimamizi wa Masoko.
i) Limeendelea na zoezi la ukamataji wa wanyama wanaozurura ovyo ndani ya Mji. Jumla ya wanyama 35 wamekamatwa na kutozwa faini na gharama za kugomboa zenye thamani ya shilingi 2.3 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Manispaa limekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya mapato yatakayofikia Jumla ya Shilingi 1,874 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na Shilingi 1,291 ruzuku kutoka Serikali Kuu
b) Kujenga na kuezeka paa, kutia rangi pamoja na kutengeneza kuta katika soko la Mwanakwerekwe
c) Kufanya matengenezo ya misingi na kuimarisha huduma za maji safi katika soko la Darajani, Mombasa na Mikunguni.
d) Kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya mapato Darajani kwa kujenga ghorofa moja
e) Kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Funguni
f) Kujenga misingi ya maji ya mvua, uwekaji wa mabomba ya maji safi na umeme, ujenzi wa uzio pamoja na kituo kidogo cha polisi katika kituo cha biashara cha Manispaa kilichopo Saateni.
g) Kufanya matengenezo ya maegesho ya magari Darajani.
h) Uendelezaji wa bustani za ndani ya Manispaa ya Zanzibar (Bustani za Mjini)
i) Kuchangia miradi midogo midogo ya Maendeleo ya Wadi 20 zilizomo ndani ya Manispaa ya Zanzibar.
j) Kuimarisha na kuitunza michirizi ya maji machafu na ya mvua katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar.
k) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi wake saba katika fani za udereva, mafundi magari, maafisa usafirishaji na ukaguzi wa hesabu.
l) Kutekeleza mkakati mpya wa uzoaji taka na uondoaji wa wanyama wanaozurura ovyo ndani ya eneo la Manispaa ya Zanzibar na vitongoji vyake kwa kushajihisha vikundi vya mazingira katika Wadi zote 24 kwa kushirikiana na Madiwani na Masheha
m) Kutafuta eneo jipya la kutupia taka lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 15.
n) Kuimarisha na kuendeleza huduma ya Taa za Barabarani Mjini na kulipia gharama za umeme.
o) Kugharamia matumizi ya maji safi katika masoko na Ofisi zote za Baraza la Manispaa, bustani, pamoja na Karakana ya gari, Saateni
p) Kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi yanapatikana kwa mujibu wa sheria na kwa wakati ili kuweza kuimarisha ufanisi kazini.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Manispaa liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Shilingi 1,291 milioni kwa ajili ya ruzuku.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ililenga kukusanya Shilingi 400 milioni kupitia vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, ilikusanya Shilingi 570.1 milioni sawa na asilimia 143.0 na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imeendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri Mombasa
b) Halmashauri imejenga Silabu mbili za kuhifadhia taka katika maeneo ya Pangawe na Jumba la Benki Mwanakwerekwe.
c) Imekusanya na kuzoa taka wastani wa tani 24,958.
d) Imenunua gari ya ukaguzi.
e) Imeendelea na ujenzi wa jengo la Hospitali Mbuzini.
f) Imenunua mashine ya kutengenezea Matofali kwa ajili ya miradi ya wananchi.

g) Imesaidia utekelezaji wa miradi 16 ya Maendeleo ya wananchi katika Wadi zao (Kiambatanisho Namba 8 kinatoa ufafanuzi zaidi).

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya Shilingi 480.7 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Kuendeleza mradi wa usafi wa mazingira.
c) Uendelezaji wa ujenzi wa Hospitali Mbuzini kwa kutia sakafu, dari, milango, madirisha na kupiga plasta.
d) Kununua mashine ya kuchanganya mchanga na saruji kwa ajili ya utengenezaji wa matofali ya kujengea miradi ya maendeleo.
e) Kusaidia miradi 16 ya wananchi kupitia Wadi zao.

HALMASHAURI YA WILAYA KASKAZINI 'A'

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya Kaskazini 'A' Unguja, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ililenga kukusanya Shilingi 189.7 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Halmashauri imekusanya shilingi 144.4 milioni sawa na asilimia 76.1. Kati ya hizo, shilingi 59.7 milioni zilitumika kwa kazi za kawaida na Shilingi 78.9 milioni zilitumika kwa kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imefanya matengenezo ya jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Halmashauri Mkokotoni kwa kuweka mlango wa chuma Ofisi ya Mhasibu na kupiga plasta.
b) Imefanya matengenezo ya jengo la Skuli ya Msingi Chaani, Skuli ya Msingi Matemwe, Skuli ya Maandalizi Kikongeni.
c) Imefanya ujenzi wa madarasa manne ya Skuli ya Msingi Kinyasini na Ofisi za walimu.
d) Imefanya ujenzi wa msingi wa madarasa manne ya Skuli ya Kandwi na ujenzi wa Skuli ya Msingi Moga.
e) Imefanya ujenzi wa visima viwili Tumbatu Gomani na imefanya ununuzi wa mipira ya maji kwa ajili ya Changani Mnarani.
f) Imesaidia gharama za mafunzo kwa wafanyakazi watatu wanaosoma Chuo cha Utawala wa Umma ngazi ya cheti katika fani za Uhasibu, Katibu Muhtasi na masjala.
g) Halmashauri imeandaa michoro ya masoko ya Kinyasini, Mkwajuni, Bwekunduni, Mkokotoni na Soko la Vinyago Pwani Mchangani.
h) Imesaidia usambazaji wa maji katika Wadi ya Muwange, uwekaji wa kifusi katika njia ndogo za Chaani Mtakuja, Kinyasini Ziwani na Bwekunduni. Aidha, imejenga maduka ya wafanyabiashara Pwani Mchangani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/13, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' imelenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya Shilingi 205.3 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri – Mkokotoni.
c) Kuanza ujenzi kituo kidogo cha Halmashauri – Nungwi.
d) Kusaidia ujenzi wa maktaba Skuli ya Sekondari – Jongowe.
e) Kusaidia ukarabati na ujenzi wa vyoo Skuli za Msingi Kidagoni, Bwereu, Kandwi, Chaani Kubwa, Potoa na Kilima Juu.
f) Kujenga kituo cha kuhifadhia Mitihani – Mkwajuni.
g) Kujenga kiwanda cha kusagisha nafaka – Nungwi.
h) Kujenga masoko ya Bwekunduni na ujenzi wa Soko la Kinyasini.
i) Kuimarisha utendaji kwa kununua vifaa na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Halmashauri na kusaidia maendeleo ya elimu katika Wilaya Kaskazini 'A'.
j) Kujenga njia ndogo Tumbatu Gomani na Shindoni/Chutama.
k) Kuendesha semina kwa wafanyakazi na Madiwani wa Halmashauri.
l) Kununua gari na jenereta.
m) Kununua samani na mashine za Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri inakadiria kupata kiasi cha Shilingi 782 milioni, ikiwa ni ruzuku kupitia programu ya *Market Infrastructure Value Additional Rural Financing (MIVARF)* kwa ajili ya uboreshaji miundombinu ya masoko.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'B' UNGUJA

Mhe. Mewnyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B', kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ililenga kukusanya Shilingi 214 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Halmashauri imeshakusanya Shilingi 184.9 milioni sawa na asilimia 86.4. Kati ya hizo, Shilingi 68.7 milioni zilitumika kwa kazi za maendeleo na Shilingi 116 milioni zilitumika kwa kazi za kawaida.

Halmashauri imesaidia miradi ya maendeleo ya Wadi inayotekelezwa na wananchi yenye thamani ya Shilingi 65 milioni ikiwemo ujenzi wa Skuli, usambazaji wa maji safi, uchimbaji wa visima, ujenzi wa kituo cha afya na ujenzi wa jengo la ukumbi wa mkutano na Ofisi za Halmashauri (Kiambatanisho Namba 9 kinaonesha orodha ya miradi iliyotelekelezwa).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' imelenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya kiasi cha shilingi 275.6 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato
b) Kusaidia maendeleo ya elimu katika Wilaya ya Kaskazini 'B' kwa kufanya mikutano na wadau wa elimu na kusaidia vifaa vya ujenzi wa Skuli za Donge Mtambile, Donge Kipange, Pangeni, Mbaleni, Donge Kitaruni, Donge Muwanda, Makoba, nyumba ya Walimu Kiwengwa pamoja na jengo la Maktaba ya Mahonda.
c) Kusaidia ununuzi wa vifaa vya kusambazia maji safi na salama Mwembehamari, Donge Mbiji na Donge Chechele.
d) Kusaidia ununuzi wa vifaa vya kusambazia umeme Zingwezingwe na Kinduni.
e) Kusaidia ununuzi wa vifaa vya kuendeleza vituo vya afya Matetema na Bumbwini Kiongwe.
f) Uendelezaji wa jengo jipya la Ukumbi wa mikutano wa Halmashauri uliopo Kinduni.
g) Kusaidia vifaa vya ujenzi na ununuzi wa mbegu za mazao kwa vikundi vitatu vya ushirika vya Mahonda, Bumbwini Makoba na Matetema.
h) Kusaidia ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa masoko Donge Muwanda, Mahonda na Mtendeni Shehia ya Mangapwani.
i) Uendelezaji barabara za ndani (*feeder roads)* kwa kutia kifusi barabara ya Mkadini.
j) Kusaidia utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti pembezoni mwa barabara kuu.
k) Kujenga josho la wanyama Donge Muwanda.
l) Ununuzi wa vespa na gari moja aina ya (*Double cabin*).
m) Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu wa Halmashauri, wawili ngazi ya Shahada ya kwanza ya sheria na Utawala wa Umma na mmoja ngazi ya cheti katika fani ya Katibu Muhtasi.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ililenga kukusanya Shilingi 94.6 millioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, ilikusanya Shilingi 110 milioni sawa na asilimia 116.3 na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imesaidia miradi ya wananchi kwa kupeleka vifaa vya ujenzi vikiwemo saruji, milango na matofali katika Kituo cha Afya Bwejuu, Skuli ya Kiongoni, Skuli ya Muungoni, Ukamilishaji wa vyoo Skuli ya Paje na ujenzi wa wodi ya kituo cha Afya Mtende vyenye thamani ya Shilingi 27.8 milioni (Kiambatanisho Namba 10 kinatoa ufafanuzi zaidi).
b) Imeratibu ukusanyaji wa taka katika Hoteli za kitalii ili kuzuwia utupaji taka ovyo pamoja na uchafuzi wa mazingira.
c) Kuendelea kutayarisha mji wa kisasa wa Uswiswi kwa kuzingatia ujenzi unaofuata sheria na kanuni.
d) Imenunua vifaa vya ofisi ikiwa ni pamoja na gari moja, kompyuta na vifaa vya kuandikia.

e) Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ilishirikiana na Kamati za Mazingira za Shehia, imetoa vifaa vya kufanyia usafi kwa Shehia za Paje, Kizimkazi Mkunguni na Kajengwa vyenye thamani ya Shilingi 301,000.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyengine zilizotekelezwa ni kuwaelimisha wananchi kupitia mikutano ya hadhara katika Shehia zao ili waweze kufahamu kazi na wajibu wa Halmashauri ambapo jumla ya mikutano minane ilifanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imepanga kutekeleza malengo yafutayo:-

a) Kukusanya Shilingi 139.3 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato
b) Kutekeleza miradi ya wananchi kwa Wadi tatu ambayo ni kukamilisha ujenzi wa kituo cha Afya Kajengwa, kununua mipira ya maji yenye thamani ya Shilingi 5 milioni Muungoni na kuendelea na ujenzi wa kituo cha Skuli ya Maandalizi ya Jambiani Kibigija
c) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Kusini
d) Uendelezaji wa soko la Kitogani
e) Matayarisho ya ujenzi wa soko jipya Paje.
f) Ujenzi wa bustani na maegesho ya gari katika kijiji cha Makunduchi.
g) Ujenzi wa kitalu cha miti katika kijiji cha Kitogani.
h) Kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 3 katika ngazi za Cheti na Stashahada katika fani za Rasilimali Watu, Utunzaji Kumbukumbu na Uhasibu.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kati ililenga kukusanya Shilingi 174.5 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, ilikusanya Shilingi 137.6 milioni asilimia 78.9 na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imesaidia ujenzi wa Jengo moja la Madrasa Shehia ya Mchangani.
b) Imesaidia ujenzi wa Maduka Kipilipilini ambapo yamefikia hatua ya linta.
c) Imesaidia mradi wa usambazaji maji safi na salama pamoja na utiaji wa kifusi njia za Shehia ya Dunga Kiembeni.
d) Imesaidia ujenzi wa Skuli ya Chekechea Mpapa, madarasa katika Skuli ya Msingi Unguja Ukuu Tindini.
e) Imetandaza nyaya za umeme ndani ya kituo cha afya na nyumba ya daktari katika Shehia ya Tunguu.
f) Imenunua kompyuta moja kwa Skuli ya Sekondari Unguja Ukuu.
g) Ujenzi wa vyoo viwili katika Ofisi ya Halmashauri Dunga.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa mwaka 2012/2013, inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya jumla ya Shilingi 200 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato
b) Kujenga Skuli ya Maandalizi ya Kibele.
c) Kujenga Skuli ya msingi ya Mwera-Pongwe.
d) Kuezeka jengo la soko la Mgenihaji.
e) Kujenga Skuli ya Maandalizi Dunga.
f) Kujenga Skuli ya Sekondari ya Uroa
g) Kumaliza jengo la maduka ya Kipilipilini Chwaka
h) Kujenga Ofisi ya Halmashauri ya Tunguu.
i) Kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 3 katika ngazi za Stashahada na Shahada ya kwanza katika fani za Rasilimali Watu na Uhasibu.

BARAZA LA MJI MKOANI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji Mkoani lililenga kukusanya Shilingi 19 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Baraza limekusanya Shilingi 31.2 milioni sawa na asilimia 164.2 ya makadirio ya makusanyo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Limejenga sehemu ya paa la soko la Samaki na matunda la Mbuyuni Mkoani kwa thamani ya Shilingi 4.5 milioni
b) Limejenga Slabu nne za kuhifadhia taka Kinyasini, Makadara, Kanisani Ng'ombeni na Kipitacho.

Mhe. Mewnyekiti, shughuli nyengine zilizotekelezwa na Baraza la Miji Mkoani ni kusaidia miradi miwili ya jamii. Miradi hiyo ni ujenzi wa mahodhi mawili ya kuhifadhia taka pembezoni mwa fukwe za Mbuyuni na kuweka saruji kwenye mabanda mawili ya Skuli ya Chekechea Ng'ombeni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Mji Mkoani linakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya jumla ya Shilingi 35 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Uendelezaji wa ukarabati wa soko la matunda na samaki Mbuyuni Mkoani.
c) Uwekaji wa kifusi eneo la Mapinduzi na Ng'ombeni.
d) Kusaidia miradi ya jamii iliyomo katika eneo la Baraza.
e) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani**.**
f) Kuendeleza huduma za usafi katika eneo la Baraza la Mji wa Mkoani.
g) Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu wa Halmashauri, wawili ngazi ya Stashahada katika fani uhasibu.

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji Chake Chake lililenga kukusanya Shilingi 64 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Baraza limekusanya Shilingi 67.2 milioni sawa na asilimia 105 ya makisio ya makusanyo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Baraza limeezeka Soko la Machomane na limefanya matengenezo ya Ofisi ya Baraza kwa kujenga ukuta sehemu ya nyuma.
b) Limetoa misaada wa vifaa vya ujenzi kwa waliopata matatizo Madungu na Mtoni. Aidha, Baraza limeweka kifusi njia ya Machomane.
c) Limejaza kifusi katika eneo la wafanya biashara wadogo wadogo soko la samaki Chake Chake pamoja na kujenga bomba la kupitishia maji (*Culvat*), kujenga msingi wa maji machafu katika Mtaa wa Tenga na Silabu mbili katika maeneo ya Mtoni na Kilimatinde.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Mji Chake Chake linakusudia kutekeleza yafuatayo:-

a) Kukusanya jumla ya Shilingi 83 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato
b) Kuendeleza ujenzi wa Soko la Machomane
c) Matengenezo ya Ofisi ya Baraza
d) Kujenga msingi wa maji machafu Mkungumalofa
e) Kujenga Skuli ya Maandalizi Machomane mpaka kufikia linta
f) Kujenga daraja la Mtoni
g) Matengenezo ya machinjio Kisiwani
h) Kujenga Silabu tatu Bandataka, Mkungumalofa na Misufini.
i) Utiaji wa kifusi, usafishaji na utengenezaji wa eneo la kuegesha gari katika eneo la soko la samaki Chake Chake.
j) Kusaidia maafa ya kijamii.

k) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.
l) Kuendeleza huduma za usafi katika eneo la Baraza la Mji Chake Chake.
m) Kuratibu umaliziaji wa ujenzi wa msingi wa Msingini Mtoni unaosimamiwa na Idara ya Mazingira.
n) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wawili wa Baraza kwa kuwasomesha ngazi ya Stashahada ya Sheria na Uhasibu.

HALMASHAURI YA WILAYA MKOANI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya Mkoani ililenga kukusanya Shilingi 30 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Halmashauri ilikusanya Shilingi 44 milioni sawa na asilimia 146.7 ya makadirio ya makusanyo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kusaidia ujenzi wa Soko la samaki na matunda Mkanyageni kwa kuezeka paa.
b) Imesaidia ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Msikiti wa Michenzani, Madarasa Chumbageni, Skuli ya Sekondari Kengeja, Skuli ya Msingi Mahuduthi, Daraja la Mto Mkuu Kengeja, Madarasa ya Kengeja na Mwambe vyenye thamani ya Shilingi 4 milioni.
c) Imesaidia gharama za mitihani ya majaribio ya wanafunzi wa Wilaya ya Mkoani.
d) Imeweka kifusi barabara ya Likoni/Kengeja na Msikiti wa Maambani, Chambani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

a) Kukusanya mapato ya Shilingi 53.6 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Kuendeleza ujenzi wa Soko la Samaki na Matunda Mkanyageni.
c) Kujenga Ukuta Bandari ya Mbuyuni/Kengeja.
d) Kusaidia shughuli za maendeleo ya wananchi katika Wadi za Kisiwa Panza, Chokocho, Kangani, Mtambile, Kiwani na Mkanyageni.
e) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ilikusudia kukusanya Shilingi 35.2 milioni kutoka vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Halmashauri imekusanya Shilingi 36.8 milioni sawa na asilimia 104.5 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imesaidia ujenzi wa kituo cha afya Kibokoni kwa kupeleka vifaa vya ujenzi.
b) Imefanya matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Halmashauri kwa kuchora ramani na kutangaza tenda ya ujenzi.
c) Kusaidia ada za masomo ya wanafunzi 36 wa darasa la kumi katika Shehia ya Wesha na ukarabati wa njia ya Gombani/Ng'ambwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Chake chake inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya Shilingi 36 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la Halmashauri kwa kuweka msingi.
c) Kutia rangi na kuweka milango mitatu katika ukumbi wa mikutano jengo la zamani la Ofisi.
d) Kusaidia ununuzi wa vifaa vya ujenzi vituo vya afya Matale, Ndagoni na Kibokoni, Madrasa Ng'ambwa, Skuli za Kwale, Ziwani Sekondari, Shungi Sekondari, Mvumoni Msingi, Chanjamjawiri Msingi na Pujini Sekondari.
e) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.
f) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wanne wa Halmashauri, wawili katika ngazi ya Stashahada ya uhasibu na wawili katika ngazi ya Cheti (uhasibu na rasilimali watu).

BARAZA LA MJI WETE

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji la Wete lililenga kukusanya Shilingi 45.6 millioni kupitia vyanzo vyake na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Baraza limekusanya Shilingi 48.4 millioni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya mapato na kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Baraza limetengeneza Ukumbi wa Mikutano wa *Jamhuri Hall* kwa kutia plasta, rangi, umeme, mafeni na vigae vya sakafuni. Ukumbi huo sasa umeshakamilika na uko tayari kwa matumizi.
b) Limeendelea kuimarisha miradi ya jamii kwa kusaidia vifaa vya ujenzi na maji katika wadi 7, Kipangani, Selemu, Jadida, Utaani, limbani, Kizimbani na Bopwe venye thamani ya Shilingi 15 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyengine iliyotekelezwa na Baraza ni kushughulikia kazi za matengenezo ya Soko la samaki Bandarini kwa kuunga maji, kutia rangi na umeme.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Mji la Wete inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya jumla ya Shilingi 50 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Kuengeza ujazo wa kifusi katika kituo cha kuegesha gari Wete.
c) Kuendelea na ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano *(Jamuhuri Hall).*
d) Ukarabati wa barabara kutoka chinjioni mpaka Bandarini.
e) Kuendeleza huduma za usafi katika eneo la Baraza la Mji wa Wete.

HALMASHAURI YA WILAYA YA WETE

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Wete kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 ililenga kukusanya Shilingi 40 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Wete imekusanya Shilingi 59.2 milioni sawa na asilimia 148 ya makadirio na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imekamilisha ujenzi wa Msingi wa Ofisi ya Halmashauri, jumla ya Shilingi 15.8 milioni zimetumika.
e) Halmashauri imetoa msaada wa vifaa vya ujenzi katika Skuli za Maziwani, Mchangamdogo, Kojani, Daya, Ukunjwi, Mjini Kiuyu, Ole msingi, Pandani msingi, Bwagamoyo na Fundo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Wete imejenga vyoo vya bei nafuu Mchangamdogo na imetoa elimu ya Afya na kununua vifaa vya usafi Kojani vyenye thamani ya Shilingi 5 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyengine iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Wete ni kusaidia wananchi waliopata maafa kwa kuunguliwa moto nyumba zao katika maeneo ya Ole na Mzambarau Takao ambapo Shilingi 330,000 zimetumika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Wete inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya jumla ya Shilingi 75 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri wa Wilaya ya Wete iliyoko Bahanasa.
c) Kusaidia huduma za Afya na Mazingira kwa kutoa mafunzo katika Wilaya ndogo, Kojani.
d) Kusaidia vifaa vya ujenzi wa madarasa ya Skuli katika Wadi.
e) Kununua pikipiki itakayoimarisha shughuli za ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika mwaka wa fedha 2011/2012 ililenga kukusanya Shilingi 30 milioni kupitia vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia mwezi Machi 2012, imekusanya Shilingi 60 milioni sawa na asilimia 200 ya makadirio ya mwaka na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imeezeka na kupiga plasta Chinjio la Mziwanda, imejenga choo Konde Mjini, imesaidia matofali Skuli ya Sekondari Micheweni na imeanza msingi wa Skuli ya Msingi Mawe Matatu Makangale.
b) Imenunua vitendea kazi zikiwemo Vespa mbili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya Shilingi 77 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.
b) Kujenga ukumbi wa mikutano Micheweni kuanzia msingi hadi sehemu ya linta.
c) Kusaidia miradi ya jamii, wanafunzi na majanga.
d) Kusaidia ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Simai katika eneo la Machengwe.
e) Kusaidia kazi za kusambaza mabomba ya maji kijiji cha Kikunguni na Kibubunzi.
f) Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahili zao, kununua vitendea kazi vya kisasa na samani.

IDARA YA URATIBU IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti**,** Idara hii ina wajibu wa kusimamia na kuratibu kazi zote za Idara Maalum za SMZ ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera, Sheria na kanuni za Idara Maalum za SMZ, kusimamia vikao vya Tume ya Utumishi pamoja na Mahkama ya Rufaa za Idara Maalum ya SMZ. Aidha, inasimamia majukumu ya Kisera ya kuoanisha miundo ya kiutumishi, maslahi ya maafisa na wapiganaji, kuwajengea uwezo wa kitaaluma na kuratibu masuala ya michezo na utamaduni ndani ya Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti**,** Idara ya Uratibu Idara Maalum za SMZ, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa TZS 145 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Idara hii iliingiziwa TZS 84.1 milioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Imefuatilia kwa karibu shughuli zote za maendeleo na za kawaida zilizotekelezwa na Idara Maalum za SMZ.
b) Imefanikisha vikao vitatu vya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ.
c) Imefanikisha Vikao vitatu vya Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalum ya SMZ.
d) Idara imewajengea uwezo wafanyakazi wake wawili kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi
e) Imenunua vitendea kazi vipya ili kuboresha ufanisi kazini.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2012/1013, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kusimamia na kuratibu kazi za kawaida na miradi mitano ya maendeleo itakayotekelezwa Idara Maalum za SMZ.
b) Kufanikisha vikao vitano vya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ.
c) Kufanikisha vikao vitano vya Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ.
d) Kufanya mapitio ya Sera, Sheria na kanuni za Idara Maalum za SMZ.
e) Kuandaa mipango ya Rasilimali watu na kupitia miundo ya utumishi pamoja na kupandisha vyeo kwa Wapiganaji.
f) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi wa Idara katika ngazi ya Shahada ya Pili, Cheti na mafunzo ya muda mfupi.
g) Kukijengea uwezo wa uzalishaji Kiwanda cha Ushoni cha Idara Maalum za SMZ.
h) Kuhamasisha shughuli za michezo na utamaduni ndani ya Idara Maalum za SMZ

Mhe. Mwenyekiti**,** ili Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 200 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeanzishwa kwa Sheria Namba 1/2003 na kina jukumu la ulinzi na kupambana na shughuli za magendo na uvuvi haramu katika bahari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kiliidhinishiwa TZS 6,887 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Kikosi kiliingiziwa TZS 6,082.9 milioni sawa na asilimia 88.3 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na TZS 200 milioni sawa na asilimia 100 kwa matumizi ya kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kikosi kimewapatia sare na vifaa Maafisa na Askari wote.
b) Vyombo vikubwa na vidogo vya doria baharini vimekuwa katika hali ya utayari na vinaendelea kupata matengenezo yanayohitajika kila mara.
c) Kikosi kimefanya matengenezo ya banda la askari Msuka na Ofisi mpya ya uzamiaji (Diving) Makao Makuu Unguja. Aidha, ujenzi wa Hospitali ya Kibweni unaendelea katika ghorofa ya kwanza pamoja na ujenzi wa Laundry. Hanga la kulala askari la kambi mpya ya KMKM Tumbatu limeezekwa.
d) Chombo KM 204 Miwi na KM 103 vimeshashuka chelezoni baada ya kumaliza matengenezo yaliyokusudiwa.
e) Vifaa vya uzamiaji vimenunuliwa vikiwemo suti na mitungi ya gesi. Boti aina ya fibre na mashine yake imenunuliwa kwa ajili ya usafiri wa wazamiaji.
f) Ulinzi wa doria umeimarika zaidi baada ya kupata boti mpya tano za fibre, vile vile vifaa vya mawasiliano (Radio Base Station) vimenunuliwa.
g) Kikosi kimeweza kudhibiti utoroshaji wa zao la karafuu na jumla ya matukio 14 yalidhibitiwa. Pia Kikosi kimefanikiwa kukamata vitu vifuatavyo: - Mafuta ya Diesel 25,950 Litres, Mafuta ya Petrol 1,790 litres, Sukari 20,250 kgs, kgs 76,800 za mchele na karafuu mbichi 200 kgs.
h) Kikosi kimewapatia mafunzo Maafisa na Askari 42 katika fani ya uhasibu, sheria, utawala, afya, manunuzi, taaluma ya bahari na ufundi.
i) Vifaa vya upasuaji kwa Hospitali ya KMKM Kibweni vimenunuliwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendeleza kuimarisha nguvu za doria baharini.
b) Kuimarisha sehemu ya uzamiaji (Diving) kwa kununua mashine ya kuhifadhi maisha ya binaadamu chini ya bahari (chamber), vifaa vya uzamuaji (lifting bag), nguo za kuogelea na mashine ya kujazia hewa (compressor).
c) Kuhakikisha wafanyakazi wote wanawajibika ipasavyo kwa kuwapatia stahili zao
d) Kuendelea kuwapatia sare na vifaa vya kulalia Wapiganaji
e) Kuendelea kuwapatia elimu ya kazi wapiganaji nje na ndani ya Kikosi.
f) Kuendeleza matengenezo na ujenzi wa majengo KMKM katika kambi mbali mbali.
g) Kuendeleza ujenzi wa Hospital ya KMKM Kibweni.

Mhe. Mwenyekiti**,** ili Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 9,660 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 200 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Mhe. Mwenyekiti**,** Jeshi la Kujenga Uchumi limeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya mwaka 2003 na lina jukumu la kuwafunza vijana katika nyanja za uchumi, kilimo, viwanda vidogo vidogo, uvuvi na mafunzo ya amali pamoja na kutoa huduma ya ulinzi kwa Taasisi za Serikali. Vijana wa JKU hufunzwa kwa kufuata mfumo wa ujenzi wa Taifa ili waweze kujiajiri wenyewe wakati wanapomaliza mafunzo yao.

Mhe. Mwenyekiti**,** Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), kwa mwaka wa fedha 2011/2012 liliidhinishiwa TZS 4,668 milioni kwa matumizi ya kawaida na TZS 450 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, Jeshi la Kujenga Uchumi liliingiziwa TZS 4,431.7 milioni sawa na asilimia 94.9 ya matumizi ya kawaida na TZS 195.6 milioni sawa na asilimia 43.5 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Jeshi la Kujenga Uchumi limekamilisha uchoraji wa ramani ya ujenzi wa Skuli ya Sekondari pamoja na kukusanya vifaa mbali mbali vya ujenzi wa msingi wa jengo la ghorofa moja.
b) Wafanyakazi 25 wamepatiwa mafunzo katika fani ya sheria, udaktari, uuguzi, ualimu, uhasibu, ufugaji nyuki, ushoni na kompyuta.
c) Mazao ya aina mbali mbali yamelimwa ikijumuisha ekari 156 za mpunga, ekari 82 za mahindi na mtama, ekari 80 za muhogo, ekari 13 za kunde, ekari nne za viazi vitamu ekari 21 za bustani ya miti ya matunda.
d) Jeshi la Kujenga Uchumi limenunua mashine moja ya kutotoa vifaranga "incubator" ili kurahisisha upatikanaji wa vifaranga na kazi ya kuzalisha vifaranga tayari imeanza na inaonesha maendeleo mazuri.
e) Jeshi la Kujenga Uchumi limechimba kisima kimoja cha maji na cha pili kipo katika hatua za mwisho ili kurahisisha upatikanaji wa maji safi na salama katika Skuli ya Ufundi na Sekondari ya JKU Mtoni.
f) Baadhi ya zana za kufundishia zimenunuliwa kwa ajili ya kuimarisha mafunzo kwa vitendo katika Skuli ya Ufundi JKU Mtoni.
g) Ujenzi wa nyumba ya pili ya wataalamu Bambi umekamilika na kuanza ujenzi wa msingi nyumba ya tatu. Kuchimba kisima kimoja kwa ajili ya kuongeza uwezo wa maji ya umwagiliaji kwenye ekari 28 za mboga mboga na ekari 5 za alizeti ambazo zimelimwa.
h) JKU imefanya mapitio ya uendeshaji wa shamba la mboga mboga Bambi ili kuweza kuleta tija kama ilivyokusudiwa.
i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili, JKU imelima ekari 15 za mbegu ya mahindi, ekari 40 za mbegu ya mpunga aina ya Nerica, ekari 10 za mbegu ya mtama.
j) Kwa kushirikana na Vikosi vyengine JKU imeshiriki katika operasheni karafuu kisiwani Pemba katika msimu huu wa karafuu uliomalizika.
k) JKU kwa kushirikana na JKT, imeshiriki katika maonesho ya Saba Saba na Nane Nane katika Mikoa ya Dar es salam, Morogoro na Dodoma. Pia Jeshi la Kujenga Uchumi kwa njia ya uwakala limeleta matrekta 14 kutoka SUMA JKT kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa matrekta nchini.
l) Vituo vya afya vya JKU Saateni na Wawi vimetoa huduma kwa Askari na Maafisa wa JKU pamoja na raia wa maeneo jirani. Kwa mwaka 2011/2012, jumla ya wagonjwa 27,653 wamepatiwa huduma tofauti za matibabu katika vituo hivyo.
m) JKU imeshiriki katika michezo ikiwemo mpira miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, riadha pamoja na kutoa burudani kupitia vikundi vyake vya sanaa na utamaduni.
n) Jeshi la Kujenga Uchumi limeweza kufanya ukarabati mkubwa wa majengo mbali mbali ikiwemo jengo la Ofisi ya JKU Upenja, nyumba moja ya kuishi wafanyakazi na ukarabati mabanda ya kuku katika kambi ya JKU Upenja.
o) Kuendeleza ujenzi wa nyumba ya Kamanda wa JKU Pemba.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2012/1013, Jeshi la Kujenga Uchumi limejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuwaendeleza kielimu watumishi wa JKU katika fani na ngazi mbali mbali ili kuleta ufanisi katika kazi.
b) Kuendelea kutoa mafunzo ya uzalendo kwa vijana wa Zanzibar ili waweze kuitumikia nchi yao.
c) Kuimarisha ufugaji wa kuku na ng`ombe wa maziwa pamoja na kufufua ufugaji wa nyuki.
d) Kuimarisha kilimo cha mazao ya nafaka na miti ya matunda
e) Kuimarisha Skuli za Ufundi na Sekondari za JKU kwa kuzipatia vifaa vya kufundishia mafunzo kwa vitendo ili ziweze kutoa elimu bora kwa vijana.
f) Kuendelea kutoa elimu juu ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa ukimwi kwa wana JKU.
g) Kuimarisha na kupanua mafunzo ya kijeshi kwa watumishi wa JKU
h) Kuendeleza Michezo mbali mbali na utamaduni.
i) Kuendelea kutengeneza mazingira bora kwa kuwapatia wafanyakazi zana na vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi pamoja na kutoa maslahi kwa wapiganaji.
j) Kuendeleza uimarishaji wa miundombinu ya mradi wa shamba la mboga mboga liliyoko JKU Bambi.
k) Kujenga ghala la kisasa la kuhifadhia mazao na ujenzi wa nyumba ya tatu ya wataalamu Bambi.
l) Kununua samani na vifaa vya nyumbani, pamoja na kusimamia utendaji wa shughuli za kila siku za shamba.

Mhe. Mwenyekiti**,** ili Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) liweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 7,504 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 300 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

IDARA YA CHUO CHA MAFUNZO (MF)

Mhe. Mwenyekiti**,** Idara ya Chuo cha Mafunzo imeanzishwa kwa Sheria Namba 1 ya mwaka 1980 na ina jukumu la kuwapokea, kuwalinda wanafunzi na mahabusu kwa lengo la kuwarekebisha tabia na kuwapatia taaluma ili wawe raia wema. Pia Idara inashirikiana na Idara Maalum za SMZ na vikosi vya ulinzi na usalama vya SMT katika kuimarisha ulinzi, usalama, utulivu na amani wan chi yetu

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Chuo cha Mafunzo (MF), kwa mwaka wa fedha 2011/2012 iliidhinishiwa TZS 3,938 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 400 milioni kwa matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, Kikosi kiliingiziwa TZS 3,307.6 milioni sawa na asilimia 84.0 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na TZS 315.6 milioni sawa na asilimia 78.9 kwa matumizi ya kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo Cha Mafunzo kimepokea jumla ya wanafunzi 479. Kati ya hao, wanafunzi 462 ni wanaume na wanafunzi 17 ni wanawake. Idadi hii inaonesha kuongezeka kwa wanafunzi 17 waliopokelewa Chuoni hapo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2010/2011 kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Namba 11.

Mhe. Mwenyekiti**,** Chuo Cha Mafunzo kimepokea jumla ya mahabusu 2,620, kati ya hao 2,510 ni wanaume na 110 ni Wanawake. Mahabusu 2,110 waliruhusiwa kwa dhamana na wengine kuachiliwa kwa kuonekana hawana hatia na waliobakia wanaendelea kusubiri hatma ya kesi zao. Makosa makubwa ya wanafunzi wanaoletwa chuoni ni kuua, wizi wa kutumia silaha, wizi wa mazao, shambulio, kubaka na kuvunja nyumba na kuiba. Hakuna mtu hata mmoja aliopo kizuizini kwa masuala ya kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Chuo cha Mafunzo imetekeleza malengo yafuatayo:-

Malengo yanaonekana kuanzia (a) mpaka (i)

a) Imepima mashamba ya Hanyegwa Mchana na Kambi ya Kinumoshi na eneo la ujenzi wa gereza jipya Hanyegwa mchana.
b) Imefanya matengenezo ya kuezeka Chuo cha Mafunzo cha Ubago.
c) Imeendelea na ujenzi wa Bweni la kulala Wanafunzi Kinumoshi kwa kuweka madirisha 4 mapya na hatua ya plasta inaendelea.
d) Vifaa vya kuezekea nyumba ya familia mbili Kangagani Pemba vimenunuliwa.
e) Wanafunzi wote wamebadilishiwa kivazi kwa kushonewa sare za rangi ya machungwa.
f) Imeimarisha huduma za chakula kwa wanafunzi na wanapata chakula cha kutosha kwa siku.
g) Imelima Ekari 50 za mpunga, Ekari 100 za muhogo, Ekari 5 za Viazi vitamu na Ekari 25 za Mahindi katika mashamba yake ya Kengeja, Kangagani, Ubago, Tungamaa, Kinumoshi na Langoni.
h) Imepitia Sera ya Idara na kutayarisha Mpango Mkakati kwa hatua ya awali.
i) Mradi wa ujenzi wa Chuo kipya Cha Mafunzo umeshaanza kwa kusafisha eneo la ujenzi, kununua vifaa vya ujenzi ikiwa ni pamoja na mashine za kufyatulia matofali, dampa moja na kusogeza miundombinu karibu na eneo la ujenzi kama vile maji na umeme.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Chuo cha Mafunzo Kimekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendelea kuyapima na kuyapatia hati miliki mashamba ya Chuo cha Mafunzo Ubago, Kengeja, Langoni, Tungamaa na Kangagani.
b) Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo cha Ubago, Bweni la Wanafunzi Kinumoshi na Bweni la Wanafunzi Kengeja.
c) Kuanza Ujenzi wa Ofisi Kuu ya Chuo Cha Mafunzo Pemba na kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Zoni ya Mashamba Unguja.

d) Kulima Ekari 50 za mpunga, Ekari 130 za muhogo, Ekari 3 mbaazi, Ekari 55 za mahindi na Ekari 3 za kilimo cha mbogamboga na kuendeleza kilimo cha Mikarafuu katika mashamba yake ya Kengeja, Kangagani, Ubago, Tungamaa, Kinumoshi, Langoni na Hanyengwa Mchana.
e) Kuweka vyoo katika Mabweni ya kulala Wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo cha Langoni.
f) Kuanza ujenzi wa majengo ya Chuo kipya cha Mafunzo Hanyegwa Mchana.
g) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Idara ya Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti**,** ili Idara ya Chuo cha Mafunzo (MF) iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 5,890 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 400 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

KIKOSI CHA ZIMA MOTO NA UOKOZI ZANZIBAR (KZU)

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeanzishwa kwa Sheria Namba 7 ya mwaka 99 na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu. Vile vile kikosi kina jukumu la kutoa huduma za zimamoto kwenye viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba. Aidha, Kikosi kinatoa ushauri wa kujikinga na moto kwa wananchi, Taasisi za Serikali na za watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU), kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kiliidhinishiwa TZS 1,883 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2012, Kikosi kiliingiziwa TZS 1,869 milioni sawa na asilimia 99.3 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kikosi kimenunua gari mbili za kisasa za kuzimia moto na gari moja limepelekwa Pemba. Vile vile, vifaa vya aina mbali mbali vimepatikana kwa upande wa Unguja na Pemba.
b) Mawasiliano ndani ya Kikosi yameimarika kwa kununua redio mpya 4, kufanyia matengenezo mbali mbali ya redio zilizopo Kikosini na Uwanja wa Ndege.
c) Kikosi kimesafisha na kuchimba msingi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mapumziko Chanjaani Pemba.
d) Kikosi kimejenga banda la kuweka gari za kuzimia moto katika Kituo cha Mwanakwerekwe.
e) Kikosi kimejenga nyumba ya vyumba vinne katika kituo cha Kigunda na kutia sakafu, plasta na sehemu ya mapokezi imewekwa dari.
f) Kikosi kimenunua mabati kwa ajili kuezekea Kituo cha Zimamoto Kitogani.
g) Kikosi kimejenga hodhi la kuhifadhia maji katika kituo cha Chanjaani.
h) Kikosi kinaendelea na ujenzi wa uzio wa Kituo cha Mahonda.
i) Kikosi kimenunua vifaa na samani kwa vituo vyake vya Unguja na Pemba.
j) Kikosi kimewapatia Maofisa na Askari sare na vifaa vya kazi.
k) Maafisa watatu wamehudhuria mafunzo nchini Singapore, maafisa 6 fani ya uhasibu, 11 mafunzo ufundi, watatu shahada ya sheria, wanne fani ya uboharia na manunuzi, 30 mafunzo ya uongozi mkubwa na 35 mafunzo ya uongozi mdogo
l) Elimu imetolewa kwa njia ya redio na TV ambapo jumla ya vipindi 36 vilirushwa hewani. Aidha, vipeperushi juu ya kujikinga na majanga ya moto vimetengenezwa na maonesho ya utumiaji wa kifaa cha kuzimia moto kinachoitwa "*Dry Sprinkler Power Aerosal*" (DSPA) yamefanyika kwa Taasisi mbali mbali za binafsi na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kikosi kimekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

Malengo yanaoneshwa kuanzia (a) mpaka (h)

a) Kuendelea kununua vifaa na gari za kutoa huduma za kuzima moto na uokozi.
b) Kuimarisha mawasiliano ya uhakika ndani ya Kikosi.
c) Kundelea kufanya matengenezo ya majengo na kujenga vituo vipya katika maeneo mapya.
d) Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi.
e) Kuboresha huduma za kiutawala na michezo.
f) Kukuza uwezo wa kiutendaji kwa Maafisa na wapiganaji kwa kuwapatia mafunzo ndani na nje ya nchi.
g) Kuongeza uhusiano na mashirikiano ya namna ya kukabiliana na majanga mbali mbali kitaifa na kimataifa

h) Kukuza uwelewa kwa wananchi, Taasisi za serikali, sekta binafsi, ili kuchukua hatua za tahadhari ya kujikinga na majanga ya moto.

Mhe. Mwenyekiti**,** ili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 3,099 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi cha Valantia kimeanzishwa kwa Sheria Namba 5 ya mwaka 2004 na kina majukumu ya kutoa ulinzi kwa kushirikiana na Vikosi vya ulinzi na usalama vya SMT na SMZ, kusaidia kulinda raia na mali zao, kutekeleza shughuli za kijeshi kwa wakati wa dharura..

Mhe. Mwenyekiti**,** Kikosi cha Valantia (KVZ), kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kiliingiziwa TZS 2,452 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 100 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, Kikosi kiliingiziwa TZS 2,086.7 milioni sawa na asilimia 85.1 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na TZS 50 milioni sawa na asilimia 50 kwa matumizi ya kazi za maendeleo na kutekeleza yafuatayo:-

a) Kikosi kimeshiriki katika majukumu ya ulinzi na shughuli za uokozi kwa kushirikiana na vikosi vya SMT na SMZ.
b) Kimewapatia elimu wapiganaji wake 13 katika fani za udaktari, uhasibu, mawasiliano ya redio, manunuzi na ugavi, utawala wa umma, TEKNOHAMA, utunzaji wa kumbukumbu, raslimali watu na mafunzo ya ufundi ndani na nje ya Zanzibar.
c) Kikosi kimewapatia elimu ya ushauri nasaha juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI wapiganaji wake wote Unguja na Pemba.
d) Kikosi kimewapatia sare Wapiganaji wake kwa kushonewa sare 500 na nyengine zinaendelea kushonwa katika kiwanda cha Ushoni cha Idara Maalumu za SMZ.
e) Kikosi kimeendelea kuyafanyia matengenezo ya vibanda vitatu vya walinzi Makao Makuu Mtoni, matengenezo ya Kambi ya Kisakasaka na matengenezo ya Kambi ya Pangatupu kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba Kikosi kimefanya matengenezo katika Kambi ya Ndugukitu.
f) Kikosi kimeyapatia hatimiliki maeneo mawili (Kambi ya Mtoni na Kambi ya Micheweni) na maeneo yaliyobakia taratibu za kupatiwa hatimiliki zinaendelea.
g) Kikosi kimekamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu na ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa uko katika hatua za mwisho.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na kutimiza majukumu hayo iliyojipangia pia Kikosi cha Valantia Kwa kushirikana na vikosi vyengine kimeweza kushiriki katika operasheni karafuu kisiwani Pemba katika msimu huu wa karafuu uliomalizika hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Kikosi cha Valantia kitatekeleza malengo yafuatayo:-

Malengo yanaoneshwa kuanzia (a) mpaka (f)

a) Kuimarisha nguvu za ulinzi na usalama.
b) Kuwaongezea uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia elimu Wapiganaji kwa kozi mbalimbali ndani na nje ya kikosi.
c) Kuweka mazingira mazuri ya kazi ikiwemo unununzi wa gari.
d) Kuendelea kuwapatia sare na vifaa vya ulinzi wapiganaji wote wa Kikosi.
e) Kutengeneza majengo ya kikosi na kuendelea kuyapatia hatimiliki maeneo ya kikosi Unguja na Pemba.
f) Kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu yakiwemo ujenzi wa mesi na ujenzi wa ukumbi wa mkutano.

Mhe. Mwenyekiti**,** ili Kikosi cha Valantia kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 3,784 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 100 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

JUMLA YA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo juu ya utekelezaji wa malengo ya Idara na Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo ya muhutasari wa maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012 na jumla ya matumizi hadi kufikia Machi 2012 na maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2012, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ilikadiriwa kutumia TZS 34,176.5 milioni. Kati ya hizo TZS 30,435.5 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 1,930 milioni kwa kazi za maendeleo na TZS 1,811.0 milioni kwa ajili ya ruzuku za Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Mkoani, Chake Chake na Wete. Hadi kufikia Machi 2012, Ofisi imeingiziwa TZS 26,570.8 milioni sawa na asilimia 87.3 kwa kazi za kawaida, TZS 1,477.3 milioni sawa na asilimia 76.6 kwa kazi za maendeleo na TZS 1,381.7 milioni sawa na asilimia 76.3 za ruzuku.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza malengo na majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, inaomba kuidhinishiwa jumla ya TZS 50,698.1 milioni. Kati ya hizo, TZS 46,654.1 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, TZS 1,906.0 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo na TZS 2,138 milioni ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji (Mabaraza ya Miji ya Mkoani, Chake Chake na Wete).

Mhe. Mwenyekiti**,** maelezo ya uchambuzi wa kina wa fedha zilizoombwa kwa mwaka 2011/2012, fedha zilizopatikana hadi mwezi Machi 2012, asilimia ya fedha zilizopatikana hadi mwezi Machi 2012 na makisio ya bajeti kwa mwaka 2012/2013 kwa kila Idara zimeoneshwa katika Viambatanisho Namba 12, 13 na 14. Aidha, Kiambatanisho Namba 15 kinatoa uchambuzi wa makushanyo ya fedha kutoka katika vyanzo vyao vya mapato ya Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji ya Mkoani, Chake Chake na Wete na Halmashauri 9 za Wilaya.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia hotuba hii, naomba kuchukua fursa nyengine kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini wa kusimamia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuendelea kunipa dhamana ya kuiongoza Ofisi hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuendeleza hali ya amani na utulivu iliyopo, kabisa tusiichezee amani. Natoa wito kwa wananchi kuendelea kuheshimu Sheria za nchi tulizoziweka wenyewe kwa lengo la kujenga mustakbali mwema wa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti**,** mwisho kabisa, nawashukuru viongozi, watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wao wa karibu wanaoendelea kunipa kila siku katika kutekeleza kazi zetu. Nawashukuru wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote na natanguliza shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa michango mtakayoitoa katika kujadili hotuba ya bajeti hii.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho Namba 1: Wageni Waliotoka Nje ya Tanzania Kuja Kuonana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Julai 2011 Hadi Machi 2012

Tarehe	Jina	Sehemu Anayotoka
27/07/2011	Mhe. Abdalla Abdi	Balozi mdogo wa Oman, Zanzibar
02/08/2011	Mhe. Dkt. Asha Rose Migiro	Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa
05/08/2011	Mhe. Levis longilonga Mayunda	Balozi wa Zambia, Tanzania

Tarehe	Jina	Sehemu Anayotoka
09/09/2011	Dkt. George Cooper	Rais wa State University of South Carolina
	Ms. Diana Cooper	Mke wa Rais wa State University of South Carolina
	Dkt, Leonard Madunlyre	Mkurugenzi wa uandishi wa vitabu vya Sayansi na Hesabati State University of South Carolina
	Lamin Drammen	Manager wa Uandishi wa Vitabu vya Sayansi na Hesabati State University of South Carolina
21/09/2011	Mhe. Klaus Peter Brandes	Balozi wa Shirikisho la Ujerumani
21/09/2011	Mhe. Harrashi Nakagawa	Balozi wa Japan, Tanzania
27/09/2011	Mhe. Joseph Chenoth Kuaga	Balozi wa Vatican, Tanzania
30/09/2011	Mhe. Peirlingi Veraladi	Balozi wa Italy, Tanzania
22/10/2011	Bwana. Zhon Zhengxing	Msaidizi Mkurugenzi wa Mji wa Jingsu China
	Ms. Li yu	Msaidizi Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa
	Bwana. Jin Changan	Vice Director, Zhengjian Municipal Health Bureau Zhengjiang
	Bwana. Zhang Sen	Deputy Secretary – General Suzhou City Government, Suzhou
	Bwana. Chen Xiaokang	Vice Director, Suzhou Municipal Health Bureau, Suzhou.
	Bwana. Hong Zhicheng	President, Suzhou Municipal Hospital
	Bwana. He Changjun	Director of Personnel Division Suzhou Municipal Health Bureau
	Bwana. Yan Weiban	Director of Organization Section Suzhou Municipal Food & Drug Administration, Suzhou Municipal Health Bureau
	Bwana. Ni Chwanming	Director of Medical administration Suzhou City health bureau, Vice President Suzhou Municipal Hospital
	Bwana. Ge Huinan	President, Suzhou City Hospital of Traditional Chinese Medicine
	Bwana. Yin Cuangzhong	Executive Vice – President Suzhou city Guangji Hospital
	Bwana. Yang Zhingiang	Director of Inspectorate Suzhou Municipal Food & Drug Administration, Suzhou Municipal Health Bureau
25/10/2011	Mhe. Antila Sinika	Balozi wa Finland, Tanzania
25/10/2011	Mhe. Fatma Nyirakubwa Ndangizi	Balozi wa Rwanda, Tanzania

Tarehe	Jina	Sehemu Anayotoka
27/10/2011	Mhe. Heldi Hantaka	Waziri anayeshughulika Maendeleo ya Kimataifa Finland
8.11.2011	H.R.H. Prince Charles na mkewe	Mwana wa Malikia wa Uingereza
9/11/2011	Mhe. Masaki Okada	Balozi wa Japan nchini Tanzania
5/12/2011	Mhe. Tim Clarke	Balozi wa Jumuiya ya Ulaya
6/12/2011	Mhe. Marcel Escure	Balozi wa Ufaransa, Tanzania
19/12/2011	Mhe. Sander Gurbuz	Balozi wa Uturuki, Tanzania
	Mhe. Mansoor Nasser Mansoor Al-Busaid	Balozi Mdogo wa Oman, Zanzibar
7/1/2012	Mhe. Anne-Grete Strom-Erichsen	Waziri wa Afya wa Norway
30/1/2012	HE. Alberic Kacou	Mwakilishi Mkaazi wa UNDP nchini Tanzania
31/1/2012	Mhe. Alfonso Lenhardt	Balozi wa Marekani, Tanzania.
10/2/2012	Mhe. Dr. Yassir Mohamed Ali	Balozi wa Sudan, Tanzania
15/2/2012	Dkt. Rufaro R. Chatora	Mwakilishi Mkaazi wa WHO, Tanzania.
29/2/2012	Bwana Alexio Musinde	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa- ILO
	Bibi Anna Collins – Falk UN WOMEN	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa- Falk UN WOMEN
	Bwana Phillemon Mutashubirwa	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa- UNHABITAT
	Bwana Luc Barrierre Constantin	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa- UNAIDS
	Bwana Daniel Churioux	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa- IOM
	Bwana Emmanuel Kalenzi	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa-UNIDO
	Bibi Vibeke Jensen	Mwawkilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa-UNESCO
	Bibi Diana Ellen Tempelman	Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa- FAO
1/3/2012	Bibi Tonia Kandiero	Mwakilishi Mkaazi wa ADB nchini Tanzania
6/3/2012	Bw. John Hendra	Msaidizi Katibu Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji kwa Masuala ya Sera na Miradi, Kitengo cha UN WOMEN
13/3/2012	Mhe. Hossam Eidin Moharam	Balozi wa Misri, Tanzania
4/4/2012	Mhe. Lorcan Fullam	Balozi wa Ireland,Tanzania

Tarehe	Jina	Sehemu Anayotoka
12/4/2012	Mhe. Issa Ntambuka	Balozi wa Burundi, Tanzania
	Mhe. Ali Davutoglu	Balozi wa Uturuki nchini Tanzania
	Mhe. James Alex Msekela	Balozi wa Italy, Tanzania
13/4/2012	Mhe. Lou Youging	Balozi wa China, Tanzania
	Mhe. Dalip Singh Singal	Balozi Mdogo wa India, Zanzibar
30/4/2012	Mhe. Hani Abdulla Mohammed Mu'minah	Balozi wa Saudi Arabia, Tanzania
	Mhe. Mohsen Movahhed Ghomi	Balozi wa Jamhuri ya Kiislam ya Iran, Tanzania
2/6/2012	Seneta Christopher Coons	Jimbo la Delaware, Marekani
7/6/2012	Mhe. Amour Zacaria Kupela	Balozi wa Msumbiji, Tanzania
	Mhe. Lennarth Hjelmaker	Balozi wa Sweden, Tanzania.

Kiambatanisho Namba 2: Sera Zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi Katika Kipindi cha Mwaka 2011/2012

Namba	Jina la Sera
1.	Sera ya Serikali za Mitaa
2.	Sera ya Mifugo
3.	Sera ya Afya
4.	Mapitio ya Sera ya Afya, 2011

Kiambatanisho Namba 3: Rasimu ya Miswada ya Sheria Iliyojadiliwa na Baraza la Mapinduzi Katika Kipindi cha Mwaka 2011/2012

Namba	MSWADA WA SHERIA
1.	Mswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
2.	Rasimu ya Kuanziswa kwa Sheria ya Maafisa wa Afya ya Mazingira
3.	Marekebisho ya Sheria Na.6/2009 ya Kamisheni ya utalii

Namba	MSWADA WA SHERIA
4.	Sheria ya Kuanzishwa kwa Bodi ya upimaji na Tathmini ya Elimu na mambo yanayohusiana na hayo
5.	Marekebisho ya Rasimu ya Sheria ya Uundwaji upya Tume ya Mipango
6.	Mapendekezo ya mswada wa kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo
7.	Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.2 ya mwaka 2011
8.	Mapendekezo ya Mswada wa kuanzishwa Mfuko wa Baraza la Wawakilishi
9.	Mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria Na.4/2008 na Sheria Na.6/1999 na kuanzisha sheria mpya ya marupurupu ya viongozi wa Kisiasa baada ya kustaafu
10.	Mapendekezo ya Mswada wa Rasimu ya Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kuzuwia rushwa na Uhujumu uchumi
11.	Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC)
12.	Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria Na.9/2009 ya Udhibiti wa dawa za kulevya.

Kiambatanisho Namba 4: Wafanyakazi Waliopatiwa Udhamini wa Masomo kwa Mwaka 2011/2012

S.N	KIWANGO CHA ELIMU	AINA YA MAFUNZO	IDADI
1	Shahada ya Uzamili	Sheria, Utawala, Uchumi na Fedha, Mipango na maendeleo ya miji na Uhusiano wa Kiuchumi	8
2	Stashahada ya Uzamili	Manunuzi, Uhasibi na Uongozi	4
3	Shahada	Utawala, technolojia ya habari na mawasiliano, uboharia, sheria na uongozi.	8
4	Stashahada	Uhifadhiwa kumbukumbu, utawala, manunuzi, uongizi wa R.watu, uongozi wa Utalii, Teknolojia ya habari na mawasiliano, uongozi wa serekali za mitaa,fedha na uchumi, mfumo wa benki ya kiislamu, uchapaji, uvuvi,biashara na uhasibu	53

5	Cheti	Uongozi wa Rasilimali watu, chakula na vinywaji, utunzaji wa nyumba, upishi, maendeleo ya vijana, ufundi, Teknolojia ya habari na mawasiliano, uchapaji, uhifadhi wa kumbukumbu, udereva, uongozi, uhasibu, mahusiano, biashara na lugha ya kiingereza.	41
		Jumla kuu	**114**

Kiambatanisho Namba 5: Taasisi Zilizokaguliwa Juu ya Utunzaji wa Siri na Nyaraka za Serikali

Namba	WIZARA/TAASISI
1.	Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
2.	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
3.	Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano – Pemba.
4.	Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Unguja na Pemba.
5.	Wizara ya Kazi Uwezeshaji, wananchi, Kiuchumi na Ushirika.
6.	Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kati.
7.	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini – Unguja.
8.	Mamlaka ya Maji (ZAWA).
9.	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar.
10.	Idara ya Ardhi na Usajili, Mipango Miji na Vijiji na Upimaji wa Ramani.
11.	Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO).
12.	Shirika la Bandari Zanzibar.

Kiambatanisho Namba 6: Taasisi Zilizokaguliwa na Kupewa Mafunzo ya Usalama

Namba	WIZARA/TAASISI
1.	Watumishi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa Waandishi wa Habari, Wapiga picha, Wazalishaji vipindi, Watangazaji, Fundi Mitambo, Waunga picha, Watunza Uwanja, Watunza ghala, Watunza ukumbi, Karani Masjala, Madereva, Mafundi Umeme, Maafisa Michezo na Walinzi.
2.	Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano – Pemba kwa Makarani Masjala na Viongozi wote wa Vitengo viliopo ofisi ya Ofisa Mdhamini.
3.	Halmashauri Wilaya ya Kati Unguja.
4.	Idara ya Ardhi na Usajili, Upimaji na Ramani, Mipango Miji na Vijiji.
5.	Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi watumishi wa Kada za Masjala Unguja na Pemba.
6.	Idara ya Uhamiaji Unguja na Pemba.
7.	Shirika la Umeme – Pemba Makarani na Watumishi wapya.
8.	Makatibu Muhtasi na Makarani Masjala wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kiambatanisho Namba 7: Baadhi ya Miradi Iliyoanzishwa na Wananchi Ikiwemo Isiyokamilika Katika Kipindi cha Mwaka 2011/2012 kwa Mkoa wa Mjini Magharibi

NAMBA	JINA LA MRADI	SHEHIA	HATUA ILIYOFIKIA	GHARAMA ZILIZOTUMIKA	GHARAMA ZINAZOHITAJIKA
1.	Ujenzi wa kituo cha afya	Bumbwisudi	Hakukuwa na mabadiliko (Kimeezekwa)	13,236,300	20,154,000
2.	Ujenzi wa nyumba ya daktari	Shakani	Hakukuwa na mabadiliko (Haujaanza)	-	11,527,450
3.	Ujenzi wa madarasa 6 na Afisi 2 za Skuli mpya	Kijitoupele	Hakukuwa na mabadiliko (Haujaanza)	-	30,243,000
4.	Ujenzi wa madarasa 4, ofisi, ghala na vyoo Skuli mpya ya Kihinani	Kihinani	Vyumba 2 na Ofisi ya Mwalimu Mkuu vimeezekwa	25,673,800	16,121,800
5	Ujenzi wa skuli ya ghorofa mbili	Nyerere	Hakukuwa na mabadiliko (Haujaanza)	-	550,000,000
6.	Utiaji wa sakafu Skuli	Muungano	umekamilika	-	-
7.	Ujenzi wa Skuli ya Chekechea	Chumbuni	Milango, madirisha na sakafu vimetiwa	34,000,000	5,800,000
8.	Utoaji maji machafu	Kwa wazee	Mradi utaendelezwa na Manispaa	37,000,000	300,000,000
9.	Ujenzi wa msingi wa maji machafu	Meya	Mradi utaendelezwa na Manispaa	-	-
10.	Ujenzi wa skuli ya Chunga	Fuoni Kibondeni	Hakuna mabadiliko (Gable)	8,838,500	35,000,000
11.	Ujenzi wa kituo kidogo cha polisi	Pangawe	Umekamilika kasoro kuwekewa umeme	5,343,400	1,820,000
12.	Ujenzi wa Bwawa la kufugia samaki	Fuoni Kibondeni	Mradi umesita shughuli zake	2,300,000	5,250,000
13.	Ujenzi wa barabara	Pangawe	Njia imekarabatiwa upya	50,3000,000	-
14.	Ujenzi wa skuli ya maandalizi	Bweleo	Milango, madirisha, plasta na sakafu vimewekwa	12,000,000	146,000
15.	Ujenzi wa kituo cha Afya Mtoni	Mtoni	Hakuna mabadiliko (Kimeezekwa)	23,004,000	51,000,000
16.	Ujenzi wa kituo cha Afya Mwanyanya	Mwanyanya	Hakuna mabadiliko (Kimeezekwa)	13,180,000	90,000,000
17.	Ujenzi wa skuli ya msingi Sharifumza	Sharifumsa	Hakuna mabadiliko	9,500,000	65,000,000

NAMBA	JINA LA MRADI	SHEHIA	HATUA ILIYOFIKIA	GHARAMA ZILIZOTUMIKA	GHARAMA ZINAZOHITAJIKA
			(Gable)		
18.	Ujenzi wa ukumbi wa mitihani Mwera	Mwera	Hakuna mabadiliko (Linter)	6,862,500	35,495,500
19.	Ujenzi wa ukumbi wa mkutano wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi	Mwera	Madirisha 5, milango 2 na sakafu vimetiwa	10,303,000	33,456,815
20.	Ujenzi wa madarasa 4 skuli ya Kitongani	Fuoni Kitongani	Vyumba 2 vya madarasa vimetiwa sakafu na plasta	5,564,500	15,887,000
21.	Ujenzi wa skuli ya Maandalizi madarasa 4	Dole	Vyumba 2 vimefikia hatua ya gable	7,962,000	16,318,000
	Jumla			**717,768,000**	**1,283,219,565**

Kiambatanisho Namba 8: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

NAMBA	JINA LA MRADI	PAHALA UILIPO	LENGO LA AHADI	UTEKELEZAJI WA AHADI	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI
1.	Kusaidia ujenzi wa Skuli	Skuli ya Regeza Mwendo	1,500,000	1,500,000	100
2.	Kusadia kutia kifusi njia ya ndani	Kizimbani-Popona Kipange	1,500,000	1,500,000	100
3.	Kusaidia usambazaji wa maji safi	Mbuzini	1,500,000	1,500,000	100
4.	Kusaidi ujenzi wa Skuli	Kibweni	1,500,000	1,500,000	100
5.	Kusaidia usambazaji wa maji	Tomondo	1,500,000	1,500,000	100
6.	Kusadia ujenzi wa Ofisi ya SACCOS	Dimani	1,500,000	1,500,000	100
7.	Kusaidia usambazaji wa maji	Mfenesini	1,500,000	1,500,000	100
8.	Ujenzi wa Daraja	Kinuni	1,500,000	1,500,000	100
9.	Kusaidia usambazaji wa maji	Mwanakwe rekwe	1,500,000	1,500,000	100
10.	Ujenzi wa Msingi wa Maji machafu	Welezo – Uholanzi	1,500,000	1,500,000	100
11.	Usamambazaji wa maji	Mwanyanya	1,500,000	1,500,000	100
12.	Ununuzi wa Nguzo za umeme	Fuoni Kibondeni	1,500,000	1,500,000	100
13.	Usambazaji wa maji	Mtopepo	1,500,000	1,500,000	100
14.	Ujenzi wa Skuli	Kijitoupele	1,500,000	1,500,000	100
15.	Kusaidia ujenzi wa soko	Kiembesamaki	1,500,000	1,500,000	0
16.	Kusaidia Ujenzi wa Ofisi	Mwera	3,000,000	3,714,050	104
		Jumla	**25,500,000**	**26,214,050**	

Kiambatanisho Namba 9: Miradi ya Wananchi Iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B"

NAM.	JINA LA MRADI	PAHALA ULIPO	LENGO LA AHADI	UTEKELEZAJI WA AHADI	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI
1.	Msaada wa usambazaji maji	Shehia ya Mtambile	1,000,000	1,000,000	100
2.	Msaada wa Vifaa vya kufundishia	Kipange	1,000,000	1,000,000	100
3.	Ujenzi wa Vyoo vya skuli	Kilombero	2,000,000	2,000,000	100
4.	Usambazaji maji	Mahonda Minanasini	2,000,000	2,000,000	100
5.	Usambazaji maji	Makoba na Mafufuni	1,000,000	1,000,000	100
6.	Msaada wa Ujenzi wa holi la kufanyia Mitihani	Skuli ya Makoba	1,000,000	1,000,000	100
7.	Uwekaji wa mita ya Umeme	Skuli ya Mgambo	1,000,000	1,000,000	100
8.	Msaada wa usambazaji maji	Skuli ya Kinduni	1,000,000	1,000,000	100
9.	Msaada ujenzi wa kituo cha kuatika miche	Shehia ya Mbaleni	1,000,000	1,000,000	100
10.	Msaada wa usambazaji maji	Bundi, Muembe hemari na kwagube	1,000,000	1,000,000	100
11.	Msaada wa usambazaji maji	Muwanda	2,000,000	2,000,000	100
12.	Ujenzi wa Holi la Mitihani	Skuli ya Sekondari Misufini	1,000,000	1,000,000	100
13.	Uendelezaji wa skuli ya msingi	Manga pwani	1,000,000	1,000,000	100
14.	Usambazaji maji	Shehia ya D/Karange	1,000,000	1,000,000	100
15.	Msaada ujenzi wa kituo cha kuatika miche	Kitaruni	1,000,000	1,000,000	100
16.	Usambazaji maji katika shehia	-Mkadini -Matetema	1,000,000	1,000,000	100
17.	Ukarabati wa Kisima cha maji	Kazole	1,000,000	1,000,000	100
18.	Uendelezaji wa Ukumbi wa Halmashauri	Kinduni	53,000,000	43,000,000	81.1
19.	Ujenzi wa Maduka	*Kipandoni*	*15,000,000*	15,000,000	-
20.	Uendelezaji wa Kituo cha Afya	Kiongwe	10,000,000	10,000,000	-
21.	Upimaji wa Viwanja	Kiwengwa	2,000,000	2,000,000	100
	Jumla	-	**100,000,000**	**65,000,000**	**65**

Kiambatanisho Namba 10: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

SNO.	JINA LA MRADI	PAHALA ULIPO	LENGO	UTEKELEZAJI
1	Uendelezaji wa Kituo cha Afya Bwejuu	Bwejuu	2,232,200	1,350,000
2	Ukarabati wa Skuli ya Kiongoni	Mtegani/Makunduchi	2,033,900	368,000
3	Kusaidia ujenzi wa Wodi Kituo cha Afya	Mtende	2,600,000	1,330,000
4	Ujenzi wa Maegesho ya Magari	Makunduchi	4,966,500	5,490,000
5	Ukarabati wa Soko Kitogani	Kitogani	2,200,000	1,200,000
6	Kusaidia Vikundi vya ushirika wa kinamama	Baadhi ya Shehia	2,553,300	301,000
7	Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri	Kitogani	12,000,000	12,000,000
8	Ukarabati wa kituo cha Afya Kajengwa	Makunduchi	3,886,700	330,000
9	Ujenzi wa Madarasa (2) Skuli ya Muungoni	Muungoni	4,842,300	2,730,000
10	Ujenzi wa uzio Skuli ya Kikadini	Jambiani	4,842,300	1,310,000
11	Ukamilishaji wa vyoo vya Skuli	Paje	5,700,000	1,420,000
		Jumla	**47,857,200**	**27,829,000**

Kiambatanisho Namba 11: Idadi ya Wanafunzi Waliopokelewa Katika Chuo cha Mafunzo kwa Mwaka 2010/2011 Hadi 2011/2012

UMRI	WANAUME		WANAWAKE		JUMLA	
	2010/11	2011/12	2010/11	2011/12	2010/11	2011/12
11-20	68	70	2	3	70	73
21-30	256	258	7	9	263	267
31-40	110	111	3	2	113	113
41-50	23	23	-	2	23	25
51 na zaidi	2	-	-	1	2	1
Jumla	**459**	**462**	**12**	**17**	**471**	**479**

Kiambatanisho Namba 12: Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2011/2012 na Mapendekezo ya Bajeti ya 2012/13

Shilingi kwa Milioni

IDARA	MATUMIZI YALIYOIDHINI-SHWA 2011/2012	FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI 2012	ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI 2012	MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2012/2013
Ofisi ya Faragha ya Rais	520.0	466.3	89.7	1,908.3
Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	836.0	644.0	77.0	1,362.0
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	240.0	158.5	66.0	466.9
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,858.5	1,810.4	97.4	1,247.3
Idara ya Mawasiliano Ikulu	80.7	53.7	66.5	174.9
Kitengo cha Usalama wa Serikali (GSO)	49.8	27.5	55.2	54.9
Ofisi ya Afisa Mdhamini, Pemba	365.5	322.5	88.2	462.4
Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	1,248.0	886.9	71.1	1,593.0
Idara ya Ushirikiano na Kimataifa wa Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje	671.0	554.0	82.6.0	884.0
Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	200.0	114.9	57.5	1,992.4
Mkoa wa Mjini Magharibi	744.0	637.0	85.6	1,099.0
Mkoa wa Kaskazini Unguja	774.0	711.8	92.0	1,083.0
Mkoa wa Kusini Unguja	761.0	642.3	84.4	1,064.0
Mkoa wa Kusini Pemba	1,164.0	886.0	76.1	1,741.0
Mkoa wa Kaskazini Pemba	950.0	793.0	83.5	1,384.0
Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ	145.0	84.1	58.0	200.0
Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)	6,887.0	6,082.9	88.3	9,660.0
Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)	4,668.0	4,431.7	94.9	7,504.0

IDARA	MATUMIZI YALIYOIDHINI-SHWA 2011/2012	FEDHA ZILIZOP-ATIKANA HADI MACHI 2012	ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATI-KANA HADI MACHI 2012	MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2012/2013
Idara ya Chuo cha Mafunzo	3,938.0	3,307.6	84.0	5,890.0
Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	1,883.0	1,869.0	99.3	3,099.0
Kikosi cha Valantia	2,452.0	2,086.7	85.1	3,784.0
Jumla	**30,435.5**	**26,570.8**	**87.3**	**46,654.1**

Kiambatanisho Namba 13: Matumizi ya Ruzuku kwa Mwaka 2011/2012 na Mapendekezo ya 2012/2013

Shilingi kwa Milioni

TAASISI	MATUMIZI YALIYOIDHINIS-HWA 2011/2012	FEDHA ZILIZOPATI-KANA HADI MACHI 2012	ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATIK-ANA HADI MACHI 2012	MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2012/2013
Baraza la Manispaa	1,041.0	887.7	85.3	1,291.0
Baraza la Mji Mkoani	190.0	122.0	64.2	209.0
Baraza la Mji Chake chake	330.0	203.0	61.5	363.0
Baraza la Mji Wete	250.0	169.0	67.6	275.0
Jumla	**1,811.0**	**1,381.7**	**76.3**	**2,138.0**

Kiambatanisho Namba 14: Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 na Mapendekezo ya 2012/2013

Shilingi kwa Milioni

IDARA	MATUMIZI YALIYOIDHINISHWA 2011/2012	FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI 2012	ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI 2012	MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2012/2013
Kuimarisha majengo ya Ikulu	300.0	300.0	100.0	400.0
Kuimarisha mawasiliano - Ikulu	100.0	100.0	100.0	100.0
Kuimarisha Serikali za Mitaa	150.0	86.3	57.5	150.0
Ujenzi wa Hospitali ya KMKM	200.0	200.0	100.0	200.0
Kuimarisha kiwanda vha ushoni cha Idara Maalum za SMZ	-	-	-	256.0
Ujenzi wa Makao Makuu ya Kikosi cha Valantia	100.0	50.0	50.0	100.0
Mradi wa Shamba la mboga mboga JKU	450.0	195.6	43.5	300.0
Ujenzi wa chuo kipya cha Mafunzo	400.0	315.6	78.9	400.0
Mradi wa Kuimarisha Vitambulisho	150.0	150.0	100.0	-
Ujenzi wa Makao Makuu ya mkoa wa Kaskazini Unguja	60.0	60.0	100.0	-
Ujenzi wa Makao Makuu ya mkoa wa Kaskazini Unguja	20.0	20.0	100.0	-
Jumla	**1,930.0**	**1,477.5**	**76.6**	**1,906.0**

Kiambatanisho Namba 15: Makisio ya Makusanyo na Mapato Halisi ya Serikali za Mitaa kwa Julai 2011 – Machi 2012 na Makisio ya Mwaka 2012/2013

Shilingi kwa Milioni

TAASISI	MAKISIO YA MAKUSANYO 2011/2012	MAKUSANYO HADI MACHI 2012	ASILIMIA YA MAKUSANYO HADI MACHI 2012	MAKISIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2012/2013
Baraza la Manispaa	1,094.9	987.0	90.1	1,874.0

Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi	400.0	570.1	143.0	480.7
Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A'	189.7	144.4	76.1	205.3
Halmashauri ya Kaskazini 'B'	214.0	185.0	86.4	275.6
Halmashauri ya Wilaya ya Kusini	94.6	110.0	116.3	139.3
Halmashauri ya Wilaya ya Kati	174.5	137.6	78.9	200.0
Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani	30.0	44.0	146.7	53.6
Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake	35.2	36.8	104.5	36.0
Halmashauri ya Wilaya ya Wete	40.0	59.2	148.0	75.0
Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni	30.0	60.0	200.0	77.0
Baraza la Mji la Mkoani	19.0	31.2	164.2	34.9
Baraza la Mji Chake Chake	64.0	67.2	105.0	83.0
Baraza la Mji Wete	45.6	48.4	106.0	50.0
Jumla	**2,431.5**	**2,480.9**	**102.0**	**3,584.4**

((Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Salum Haji (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa) Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa dhati kabisa jioni hii kunipa nafasi ya kutoa maoni ya kamati.

Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba nisome maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/13.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kukutana kwa mara nyengine ili tuendelee kujadili majukumu tuliyopewa na wananchi wetu, likiwemo jukumu hili la kujadili suala la makadiro ya mapato na matumizi ya fedha ya taasisi mbali mbali za serikali ikiwa leo tunajadili makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2012/13.

Mhe. Mwenyekiti, pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisiwe mwizi wa fadhila kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji watendaji wake wote kwa mashirikiano waliyotupa katika shughuli zetu za kamati kwa Baraza kwa jumla. Vile vile ninapenda ninapenda kuishuru Ofisi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwasilisha mbele yetu mbele ya Baraza la Tukufu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/13, ili kama Katiba na Kanuni zinavyoelekeza yaridhiwe na wajumbe wako kwa njia ya mjadala na kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa kuwashukuru kwa dhati wajumbe wa kamati yetu kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu.

Aidha ninaomba niwashukuru wajumbe wa kamati kwa michango, maoni na ushauri wanaotoa wakati wanapokutana pamoja na kamati zetu pamoja na shughuli zetu za Baraza kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa heshima kubwa niwataje waheshimiwa wajumbe wa kamati kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Makamo Mwenyekiti
3.Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4.Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5.Mhe. Mohamed Haji Khalid	-	Mjumbe
6.Mhe. Salma Mohamed Ali	-	Mjumbe
7.Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9. Ndg. Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa kwa niaba ya kamati yetu naomba kuchangia hoja ya waziri kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya kamati yetu kama ifuatavyo.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kuanzisha Tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na kutayarisha barua pepe za watendaji wa ofisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaipongeza Idara hii kwa kuanzisha Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Kamati inaamini kuwa kuanzishwa kwa tovuti na kitengo hicho kutaiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufanya kazi zake kwa ufanisi, lakini pia kuiwezesha Ofisi hii kufahamika nje na ndani ya nchi yetu.

OFISI YA FARAGHA YA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza kwa dhati ziara za nje na ndani ya nchi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais na wajumbe wake mbali mbali. Kamati yetu inaamini kuwa ziara hizi zinaongeza chachu ya maenedeleo katika nchi yetu. Hata hivyo, kamati inaishauri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Ofisi ya Faragha kuwa katika ziara hizo, kadri itavyowezekana kuwakumbuka kuwajumuisha Wajumbe wa Kamati, ili nao wapate nafasi ya kujifunza na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati vile vile imefarajishwa na maelezo kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana saini Mkataba wa Makubaliano na Serikali ya Ras el Khaimah katika nyanja kadhaa za kiuchumi na maendeleo, kama vile masuala ya Afya kwa kusaidiwa katika matibabu ya maradhi ya kisukari, figo, moyo na saratani.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaomba ipatiwe ufafanuzi wa makubaliano hayo kwa maana Zanzibar itapatiwa madaktari na vifaa kutoka Ras el Khaimah? Au madakatari wetu watakwenda kujifunza huko? Au tutajengewa hospitali itakayojihusisha na maradhi hayo?

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yatakayotolewa na Mhe. Waziri, ni muhimu kukumbuka kuwa miongoni mwa mashaka makubwa yanayoikabili sekta ya Afya katika nchi yetu ni ukosefu wa vifaa vya kisasa, pamoja na uhaba mkubwa wa wataalamu kwa maana ya madaktari wa maradhi tofauti. Hivyo, kamati yetu inawaomba viongozi wetu wanapopata fursa ya kupatiwa misaada ya Afya, basi washawishi sana misaada hiyo ijikite kwa kupatiwa vifaa na kuwapatia madakatari wetu nafasi za masomo nje ya nchi ili wakapate mafunzo katika maradhi ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa sana hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, Sukari, Saratani, figo, shindikizo la damu na maradhi ya baridi ni miongoni mwa maradhi kadhaa na mazito yanayoitesa Zanzibar, ambayo yanahitaji vifaa na wataalamu wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaendelea kuipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kulifanyia matengenezo Jengo la Ikulu ya Mnazi mmoja na lile la Chake Chake. Hata hivyo, kamati yetu inaikumbusha Seriakali kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuyafanyia matengenezo makubwa Majengo ya Ikulu ya Mkoani na Dodoma. Kwa ujumla majengo haya ni chakavu na hayana hadhi ya makaazi ya Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia inaomba ipatiwe ufafanuzi wa kutosha kuhusu suala la kuliimarisha Jengo la Ikulu ya Kibweni kwa kulipaka rangi katika kuta zake za nje, pamoja na kuimarisha bustani ya Ikulu hiyo. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba ufafanuzi kwa sababu Jengo hilo lilipakwa rangi ambayo inaonekana haikuwa na kiwango lakini mazingira ya bustani yake hayaridhishi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia inaikumbusha Ofisi hii kuyafanyia matengenezo majengo ya Ikulu ya Mkoani na Dodoma ambayo kiukweli hayana hadhi ya kuwa Makaazi ya Mhe. Rais. Aidha, tunakumbushia suala la kuwekwa uzio katika eneo la Nyumba ya Serikali iliyopo Mkokotoni, ambako mazingira yake yanachafuliwa na wanyama wanaofungwa katika eneo hilo. Kamati bila ya kusahau, inaiuliza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ule mpango wa kulihami Jengo la Serikali liliopo Fumba, ambalo eneo lake linanyemelewa kuliwa na bahari, umefikia wapi? Au ndio limetiwa kapuni?

IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA SHUGHULI ZA WAZANZIBARI WANAOISHI NCHI ZA NJE

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari wanaoishi nchi za nje. Kamati inaamini kuwa wazo la kuanzishwa kwa Idara hii pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Idara hii kuwawezesha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kuisadia nchi yao kiuchumi na kijamii. Kamati katika kazi zake ilipewa taarifa kuwa Idara hii katika siku za usoni inatarajiwa kuhamishiwa katika eneo ambalo itaweza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Kamati inafarajishwa na taarifa hii kwa sababu eneo wanalolitumia hivi sasa ni finyu na halitoshelezi kwa shughuli zao za kiofisi. Kamati vile vile inaishauri Idara hii kushirikiana na Wazanzibari waliopo Zanzibar ambao waliishi nje ya nchi kwa miaka mingi, kwa lengo la kupata taarifa zitakazawasaidia katika kazi zao. Kamati yetu pia inaishauri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kupitia Idara hii kuendelea kujifunza katika nchi zilizofanikiwa na utekelezaji wa dhana ya Diaspora. Miongoni mwa nchi hizo ni Ghana, India na nchi za “Latin America”.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hutangaza dhana ya Diaspora kupitia ZBC TV na Redio. Kamati yetu inaamini kuwa kuitangaza dhana hii mpya kwa kutumia vyombo hivi pekee haitoshelezi. Hivyo, kuna haja ya kuitangaza dhana hii kwa kutumia vyombo vya habari zaidi ya hivyo ili iweze keeleweka vyema. Aidha, kwa kuwa dhana hii bado ni mpya kuna haja kwa viongozi mbali mbali wa nchi hii kupatiwa elimu ambayo itawapa uelewa zaidi kuhusu suala la diaspora na umuhimu wake katika maendeleo ya uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuanzishwa kwa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kwa lengo la kuwawezesha Wazanzibari wanaoishi za nje kuisaidia nchi yao, kamati yetu inaona kuwa, kuna changamoto za msingi zinazoikabili Zanzibar katika utekelezaji wa Ushirikiano wa Kimataifa na dhana nzima ya Diaspora. Miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili Zanzibar katika suala la Ushirikiano wa Kimataifa ni kwamba, kwa kuwa suala la Ushirikiano wa Kimataifa limewekwa katika masuala ya Muungano, Zanzibar imekuwa ikishiriki katika Vikao vya Kikanda na vya Kimataifa kwa mwamvuli wa Muungano huku ikichukuliwa kama vile kushiriki kwake katika vikao hivyo sio suala la lazima bali ni ihsani ya Jamhuri ya Muungano. Baya zaidi katika vikao hivyo kuna mambo yanayojadiliwa na kupitishwa si ya Muungano, lakini bado Zanzibar inashiriki kwa mwamvuli huo ambao kwa muda mrefu sasa umeonekana kuwa ni kero kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna mchakato wa utoaji wa maoni ya uundwaji wa Katiba mpya, kuna umuhimu kwa Wazanzibari kuhakikisha kuwa masuala ya Mambo ya Nje yanakuwa si ya Muungano, ili Zanzibar iwe na uwezo wa kushiriki katika vikao mbali mbali ikiwa nchi kamili.

KITENGO CHA USALAMA WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, kitengo cha Usalama wa Serikali kimepewa Majukumu muhimu sana kwa lengo la kuimarisha usalama katika taasisi na vituo muhimu vya Serikali. Hata hivyo, Kitengo hiki, mbali na jitihada kinazozichukua katika kutekeleza majukumu yake, hakipatiwi fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza kazi ilizopangiwa. Aidha, kitengo hiki hakina usafiri wa kufuatilia kazi zao, ingawa kwa mujibu wa Bajeti ya mwaka 2012/2013, kimetengewa fedha kwa ajili ya usafiri. Kamati inaisisitiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukipatia kitengo hiki fedha za kutosha ili kiweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi, zikiwemo kazi za kuyakagua majengo ya Taasisi za Serikali yaliyopo Tanzania Bara, ambayo yanashindwa kukaguliwa kutokana na ukosefu wa fedha. Aidha, kamati inaona kuwa kuna haja kwa kitengo hiki kupatiwa usafiri wa gari na vespa, ili kiweze kufuatilia kwa ufanisi kazi ilizopangiwa. Kamati pia inaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukisaidia kitengo hiki kwa kukiwezesha watendaji wake kupatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ili nao waweze kuimarisha utendaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati kwa mara nyengine inakikumbusha Kitengo cha Usalama wa Serikali kuhakikisha kuwa Taasisi zote za Serikali zinafuata Sheria na taratibu, kwa kuhakikisha kuwa Watumishi wa Serikali wanaajiriwa baada ya kufanyiwa upekuzi kwa maana ya "*Vetting*". Kamati kwa upande mwengine inaona kuwa kuna haja kwa Serikali kuwa na mipango ya kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa kigeni wanaofanya kazi katika sekta binafsi, nao wanafanyiwa upekuzi kwa lengo la kuimarisha usalama katika sehemu wanazofanyia kazi pamoja na nchi kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa suala hili likafanyiwa kazi, ili kuweza kuzifahamu tabia za wafanyakazi hao wanaofanyakazi katika sekta binafsi ili tuepukane na madhara yanayoweza kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Sheria ya Upekuzi kwa wafanyakazi ina mapungufu, kwa maana kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*) kinapobaini kuwa kuna udanganyifu umefanyika katika suala la upekuzi wa wafanyakazi wapya, wao hutoa ushauri tu kuwa wafanyakazi hao wasiajiriwe, lakini Sheria haiainishi waajiri na waajiriwa waliodanganya katika zoezi zima la uajiri wachukuliwe hatua gani. Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inapendekeza Sheria hiyo kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kukiwezesha Kitengo cha Usalama wa Serikali kuweza kuwachukulia hatua wale wote walioshiriki katika udanganyifu wa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuunganisha suala la usalama katika utekelezaji wa Sughuli za Serikali, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya Taasisi za Serikali, wahasibu na washika fedha wao huchukua pesa za mishahara kutoka benki bila ya kuwepo Ulinzi wa Polisi, ambao kupatikana kwake huwa hauna gharama yoyote ile. Mhe. Mwenyekiti, Suala hili kiusalama ni hatari na halikubaliki. Hivyo, kamati inaziagiza Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa pesa za mishahara zinazochukuliwa benki zinakuwa na ulinzi wa polisi.

Aidha, Kamati inaziagiza Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa watumishi wao wakiwemo washika fedha na wahasibu, kutozilaza funguo za ofisi majumbani mwao ili kuepuka uwezekano wa upotevu wa funguo hizo. Kamati inazishauri taasisi za Serikali kuweka sehemu maalum za kuweka funguo hizo (*combination lock*.) Kamati pia inaona kuwa kuna umuhimu katika milango ya wahasibu na washika fedha kuwekwa milango ya "*Grills*" kwa lengo la kuimarisha usalama katika ofisi hizo. Kamati yetu bila ya kusahau inazikumbusha Tasisi za Serikali kuweka vifaa vya kuzimia moto "*Fire Extinguishers*" katika majengo yao,ili ziweze kukabiliana na maafa ya moto yanayoweza kutokea.

OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Ofisi hii kwa kuendelea na jukumu la kusajili na kutoa Vitambulisho vya Ukaazi vya Mzanzibari. Hata hivyo, kamati inaona kuwa kuna haja ikatolewa elimu zaidi kwa wananchi kwa lengo la kuwahamasisha kuchukua vitambulisho vyao katika vituo walivyopangiwa. Mhe. Mwenyekiti, tunalisema hili kwa sababu wakati kamati ilipokuwa Pemba kikazi, ilifahamishwa kuwa kuna idadi kubwa ya wananchi waliokuwa hawajachukua vitambulisho vyao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza Ofisi hii kwa kutoa elimu kuhusu kuelimisha matumizi bora ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kupitia ZBC TV. Hata hivyo, kuna haja kwa Ofisi hii kutoa elimu hiyo kwa kuvitumia vyombo vya habari zaidi ili elimu hiyo iwafikie wananchi wengi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza hatua ya utayarishaji wa Rasimu ya Marekebisho ya Usajili Nambari 7 ya 2005, inayoruhusu Utoaji wa Vitambulisho vya Wageni wanaoishi nchini. Kamati inashauri kuwa marekebisho ya rasimu hiyo yanahitajika kuwa madhubuti, ili kuepuka changamoto zilizojitokeza hapo kabla katika suala zima la utoaji wa vibali vya ukaazi kwa wageni wanaoingia nchini.

IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri inaeleza kuwa Idara hii kupitia Mabaraza ya Halmashauri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imekamilisha utayarishaji wa Sheria ndogo ndogo za Serikali za Mitaa. Kamati inaikumbusha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuziwasilisha Sheria hizo hapa Barazani, ili zipitiwe na Kamati ya Sheria ndogo ndogo ambayo imejumuishwa katika Kanuni mpya za Baraza, toleo la mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza hatua zilizochukuliwa na Serikali kupitia Mradi wa *ZUSP* kwa kununu vifaa kama vile gari, vespa na Honda kwa ajili ya kuliimarisha Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji Pemba, Idara ya Mipango Miji na Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kamati inaamini kuwa upatikanaji wa vifaa hivyo utaziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zao, zikiwemo kazi za kusafisha miji kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati vile vile inafarajishwa na maelezo ya kuwa Serikali imekwishaziwasilisha katika Benki ya Dunia hadudi rejea za kumtafuta mshauri wa Kusimamia Uwekaji wa Taa za Barabarani. Mhe. Mwenyekiti, suala la uwekaji wa taa hizi katika mitaa na miji yetu, lina umuhimu wa pekee hasa ikitiliwa maanani kwamba, maeneo mengi ya Manispaa ya Zanzibar kutokana na ukosefu wa taa hizo nyakati za usiku huwa hayako salama kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza kwa dhati Serikali kwa kuchukua hatua za kulenga kumtafuta mjenzi wa utanuzi wa ukuta unaopita pembezoni mwa pwani ya Forodhani, bila shaka kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya maeneo hayo na kuweka usalama wa wananchi wanaotumia maeneo hayo.

MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA

Mkoa wa Mjini Magharibi

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali Masheha pamoja na Kamati zao za Maendeleo. Bila shaka mafunzo hayo yatawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri inaainisha kuwa Mkoa umefanya ziara kufuatilia uharibifu wa mazingira na kufanya vikao na wadau wengine, ili kuzungumzia usafi wa mji na uzururaji wa wanyama.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo, uharibifu wa mazingira katika Mkoa wa Mjini Magharibi umeenea kila pahala, kuanzia nchi kavu hadi baharini. Kamati inataka kuelewa baada ya ufuatiliaji huo, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Mkoa wa Mjini Magharibi imechukua hatua gani katika kudhibiti uharibifu huo katika maeneo hayo hususan maeneo ya Mbuyu Mnene, Amani, Maruhubi, Ukanda wa bahari wa Kizingo na kadhalika. Kuhusu suala la usafi kamati inaipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia taasisi zake pamoja na vikundi mbali mbali vya mazoezi na Jumuia zisizo za Kiserkali kwa kuchukua hatua za kuusafisha mji wetu kila Jumamosi ya Mwisho wa mwezi. Hata hivyo, tunaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuongeza vifaa vya usafishaji kwa lengo la kuimarisha usafi katika miji yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa malengo ya Mkoa kwa mwaka 2012/2013 ni kutatua migogoro ya ardhi inayoukabili Mkoa. Kamati inataka kufahamu kwa mwaka 2011/2012, Mkoa ulikuwa na migogoro mingapi ya ardhi na mpaka sasa imeshaitatua migogoro mingapi? Mhe. Mwenyekiti, tunalisema hili kwa sababu suala la migogoro ya ardhi limedumu kwa miaka mingi sasa, na kila mwaka liwekwe kama ni malengo ya Mikoa na taasisi nyenginezo. Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu ina wasi wasi kama migogoro hiyo itaweza kutatuliwa kwa sababu kuna shutuma kwamba migogoro hiyo inawahusisha baadhi ya wale waliopewa madaraka katika Mikoa, Wilaya na Shehia. Hivyo, kamati inashauri kuna haja migogoro hiyo ikatatuliwa na watu au taasisi ambazo hazikuhusika ama kushutumiwa kuwemo katika migogoro hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa inaanza matayarisho ujenzi wa jengo jipya la Ofisi yake huko Amaan na kufanya matengenezo ya jengo la ofisi yake hapo Vuga. Kamati inapongeza hatua hizo zinazotaka kuchukuliwa na Ofisi hii. Lakini kamati yangu haifurahishwi na matumizi mabaya ya eneo la mbele ya jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi hapo Amani, kwa kuwekwa yadi ya Magari jambo ambalo limeharibu mandhari nzima ya eneo hili. Kamati inaikumbusha Serikali kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa na mkakati wa kujenga majengo mapya na ya kisasa ya Serikali kwa Wakuu wa Mikoa na taasisi za serikali, ili kuwawezesha wafanyakazi wa taasisi hizi kufanyakazi katika mazingira mazuri. Mhe. Mwenyekiti, kuna haja kwa serikali kuwa makini na suala la kupanga utekelezaji wa ujenzi wa majengo mapya ya taasisi za serikali, vyenginevyo kuachiwa taasisi moja pekee kutaka kujenga jengo lake kwa kutegemea pesa za Matumizi Mengineyo, kutapelekea ujenzi wa nyumba hizo kuchukua muda mrefu hadi kukamilika kwake.

Mkoa wa Kaskazini, Unguja

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja, kamati inautaka Mkoa huu kulitekeleza suala la kusimamia shughuli za Ulinzi na Usalama kwa vitendo, kwa sababu katika eneo la Mkoa huo kumejitokeza vitendo vingi vya uhalifu katika baadhi ya hoteli za kitaalii jambo ambalo linatishia usalama wa wenyeji na wageni, kwa maana ya watalii na mali zao. Aidha, kuna haja kwa Mkoa huu kusimamia masuala ya ulinzi na usalama kwa vitendo, kwa kuwa katika Mkoa huu kuna baadhi ya maeneo zipo bandari bubu zinazotumika kusafirisha na kuingiza wageni kinyume na Sheria na taratibu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaukumbusha Mkoa huu kuhakikisha kuwa vibanda vilivyojengwa katika fukwe za bahari pembezoni mwa hoteli za kitalii vinabomolewa kwani vinaharibu mazingira ya fukwe, lakini pia vinaikosesha Serikali mapato kwa kuwa tumebaini kuwa vibanda hivi vimejengwa kwa maslahi ya wenye hoteli, na pengine baadhi ya watendaji katika Ofisi za Wilaya na Mikoa.

Mkoa wa Kusini, Unguja

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaupongeza Mkoa huu kwa kuwa na jengo lake ambalo hivi sasa linatumika kwa shughuli za ofisi. Tunaiomba Mikoa mengine iige mfano wa Mkoa huu kwa kuwa na majengo yao ya kisasa. Hata hivyo, Kamati yetu inauagiza Mkoa wa Kusini kupitia kamati yake na Ulinzi na Usalama kufuatilia kwa kina masuala ya ulinzi na usalama katika Mkoa huo, kwani kumebainika kuwa kuna baadhi ya wenyeji na hata wageni wanamiliki nyumba wanazikodisha kinyume na Sheria kwa wageni, na kupelekea kutishia usalama wa Mkoa na kuikosesha Serikali mapato.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inauagiza Mkoa huu kuhakikisha kuwa vibanda vyote na miamvuli iliyojengwa katika fukwe za bahari na kupelekea kuharibu mazingira vinabomolewa mara moja, kwa lengo la kudhibiti mazingira katika maeneo hayo. Aidha, kamati inauagiza Mkoa wa Kusini Unguja kwa kushirikiana na Ofisi za Wilaya na Masheha, Idara ya Ardhi kuhakikisha kuwa nyumba zote walizokodishwa wageni zinaorodheshwa na kutoa taarifa Polisi, Uhamiaji, Zipa, na *ZRB* ili kila taasisi iwajibike kwa lile linalowahusu. Pia kamati yangu inazitaka Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya, kushirikiana na masheha kuzibua njia zote zilizozibwa na wawekezaji za kuteremkia Pwani, ili wananchi kuweza kupita kwa urahisi wanapokwenda na shughuli zao mbali mbali za kiuchumi na kawaida huko pwani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inawakumbusha Viongozi katika Mkoa, Wilaya na Shehia za Mkoa wa Kusini kuhakikisha kuwa mapato yanayokusanywa katika hoteli za kitalii yanasimamiwa ipasavyo, kwa lengo la kufaidisha Serikali na wananchi wake. Mhe. Mwenyekiti, kamati inalikumbusha suala hili kwa viongozi hawa kwa kuelewa kuwa katika Mkoa wa Kusini, mapato yanayotokana na kodi ya hoteli za kitalii yanavuja kutokana na kutosimamiwa vyema na viongozi hao. Kamati yetu pia inawakumbusha viongozi hawa kuwa kwa mujibu wa Sheria za Kodi wanatakiwa wajielewe wao ndio wasimamizi wa kodi katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na udhaifu unaooneshwa na baadhi ya viongozi hao na wengineo, pamoja na baadhi ya watendaji wa Serikali wanaopelekea kupotea kwa mapato ya Serikali, kamati inashauri pale inapobainika kutokea kwa upotevu huo, hatua za kisheria zinafaa zichukuliwe kwa wahusika. Aidha, kamati inashauri kuwa somo la kodi liingizwe katika mitaala ya skuli za sekondari, ili kuwawezesha wananchi kuyajua majukumu yao ya kulipa kodi tangu wakiwa wadogo, vyenginevyo wananchi wengi huwa hawana utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari zao, lakini pia huchangia kuwasaidia wageni nao kwa njia moja au nyengine kushiriki kutolipa kodi.

Mkoa wa Kusini, Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaupongeza Mkoa wa Kusini Pemba kwa jitihada inazozichukua katika kutekeleza majukumu iliyojipangia, likiwemo jukumu la kuwa na mpango wa kujenga nyumba ya Mkuu wa Mkoa, kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake na kununua jengo kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba kiukweli halina hadhi ya kuwa Ofisi ya Mkoa. Aidha, haipendezi kwa Mkuu wa Mkoa kutokuwa na nyumba ya serikali, na badala yake kutegemea nyumba ya kukodi ambayo bila shaka huwa na gharama zake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ujenzi wa nyumba na Ofisi za Serikali kwa Viongozi wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wilaya, lina umuhimu wa pekee na linahitaji kutekelezwa kwa vitendo, vyenginevyo suala hili litaishia kwa kuelezwa katika hotuba mbali mbali za viongozi pasi na kutekelezwa.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwenyekiti(Mhe. Mgeni Hassan Juma): Mhe. Ali Salum Haji, tunaomba kidogo tumuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, atusaidie kutengua muda, ili tuweze kuendelea na shughuli zetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia kanuni ya 156 naomba tutenge kanuni kando ili Baraza lisiahirishwe saa 1:45 usiku, hadi hapo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, atakapomaliza hotuba yake. Naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti (Mhe.Mgeni Hassan Juma):: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubali hoja ya Waziri. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ali Salum Haji: (Kny: Mhe. Hamza Hassan Juma: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniruhusu kwa mara nyengine kuendelea na hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaona kuwa, mbali na jitihada za Serikali kuzitengea pesa taasisi zake kwa ajili ya ujenzi wa Majengo ya Serikali, kiuhalisia pesa hizo hazitoshi katika kufanikisha ujenzi wa majengo ya kisasa na yanayokubalika kiofisi, na hasa ikitiliwa maanani katika miaka hii tuliyonayo wakati gharama za ujenzi zinapanda kila leo, bajeti ya majengo na masuala mengine ya maendeleo inapungua. Kamati yetu bado ina mashaka kuwa ujenzi uliokusudiwa, utaendelea kutekelezwa kwa utaratibu ule ule uliozoeleka wa Ofisi hii na nyenginezo kusubiri pesa za Matumizi Mengineyo kila baada ya mwezi ama miezi. Ukweli ni kuwa pesa za Matumizi Mengineyo hazina uwezo wa kujenga jengo linalohitajika kiofisi, bali litajengwa jengo la kubahatisha, lisilovutia na ukamilikaji wake huchukua miaka na miaka.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haitochoka kupiga mayowe hapa Barazani kuhusu Serikali kuwa "*serious*" katika kuhakikisha kuwa linakuwa na Mradi utakaotekelezwa kwa ujenzi wa nyumba na ofisi mbali mbali za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, suala hili linawezekana ikiwa Serikali itafikiria kukaa kitako na kuwatafuta marafiki wetu wa kweli, kwa maana ya Wachina na wengineo ili waangalie uwezekano wa kutusaidia.

Mkoa wa Kaskazini, Pemba

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba, ingawa jengo lao ni la kale, angalau wanafanya kazi zao katika eneo linalotizamika. Hata hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini, Pemba, ni miongoni mwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa ambazo zinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na Watumishi wa Serikali, kwa maana ya Wawakilishi kutoka taasisi mbali mbali za serikali, hali ambayo imepelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri serikali, ili kuitafutia ufumbuzi changamoto, hii kuweka mipango ya kuhakikisha kuwa Ofisi za Mikoa na Wilaya zinakuwa na watumishi wa kutosha kutoka kila taasisi inayohitajika.

MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Baraza la Manispa,

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Baraza la Manispaa katika kutekeleza majukumu yake, yakiwemo majukumu ya kusimamia na kuimarisha usafi katika Manispaa ya Zanzibar. Kamati inalitaka Baraza hili kuendelea na jitihada hizo ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa Rwanda ya pili katika masuala ya usafi. Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, ili Baraza hili liweze kufikia lengo la kuhakikisha kuwa Manispaa yetu inakuwa katika mazingira ya usafi tunayoyataka, kunahitajika mashirikiano ya dhati kati ya Baraza la Manispaa na wadau wengine kama vile Serikali kuu, vikundi mbali mbali vinavyotunza mazingira na masuala ya usafi, viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, tunaliainisha hili kwa sababu wengi wetu tuna fikra suala la kusafisha Manispaa na kuimarisha mazingira ni la Baraza la Manispaa pekee, na kusahau kuwa wadau wengine mbali mbali nao wanahitajika kuhakikisha kuwa wanachangia nguvu zao kwa kuhakikisha kuwa wanasafisha maeneo yao kwa lengo la kutunza mazingira. Serikali kwa upande wake inahitajika kulisaidia Baraza hili kwa kulipatia vitendea kazi vya kutosha na maslahi bora kwa watumishi, ili Baraza liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, Serikali inahitajika kulisaidia Baraza la Manispaa kwa kuliachia vianzio vya mapato, ambavyo vitaliwezesha Baraza kujiendesha. Hata hivyo, kuna umuhimu mkubwa kwa Baraza la Manispaa kujielewa kuwa mapato ya Serikali si mali ya mtu bali ni mali ya Serikali. Hivyo lihakikishe kuwa kodi zinazokusanywa ni kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu

Mhe. Mwenyekiti, katika kazi zake, mwezi wa Mei mwaka huu. Kamati yetu ilipata fursa ya kukutana kwa pamoja na Uongozi wa Baraza la Manispaa na vikundi vinavyojihusisha na masuala ya utunzaji mazingira na masuala ya usafi kwa lengo la kubadilishana mawazo na kuhamasisha utekeleza wa dhana ya Ushirikishwaji wa Pamoja kati ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP).* Kamati kwa ujumla imefarajishwa na matokeo ya kikao kile kwa sababu kimepelekea washiriki wa kikao hicho, sio tu kuielewa dhana hiyo bali pia kujenga mashirikiano katika shughuli zao za utunzaji mazingira na masuala ya usafi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufanikisha kwa pamoja shughuli za Serikali kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali na Jamii kuhamasisha utekelezaji wa dhana ya Ushirikishwaji wa Pamoja kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (**PPP).** Hivyo Kamati yetu inatoa wito kwa Serikali na jamii kutoa elimu kwa viongozi, watendaji wa Serikali na wananchi kwa ujumla ili kuweza kuielewa dhana hii mpya. Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, kuna haja kwa Serikali kuijengea uwezo sekta binafsi ili iwe nayo ina uwezo wa kuitekeleza kwa ufanisi dhana hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inalitaka Baraza la Manispaa kuwa na utaratibu mzuri katika utekelezaji wa miradi katika Wadi mbali mbali zilizopo katika Manispaa ya Zanzibar. Kamati inaliainisha hili kwa sababu imekuwa na mashaka kuwa Baraza limekuwa likitoa fedha za miradi hiyo, lakini utekelezaji wa miradi hiyo huwa hauonekani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja kuwashirikisha madiwani na masheha katika Utekelezaji wa Miradi katika wadi ili kuhakikisha ufanikishaji wa miradi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Halmashauri na Mabaraza ya Miji mbali mbali Unguja na Pemba. Hata hivyo, mbali na jitihada zinazofanywa na taasisi hizi, Halmashauri na Mabaraza mengi ya Miji yanakabiliwa na changamoto kadhaa kama vile ukosefu wa wataalamu hususan wanasheria na watoza kodi, ukosefu wa vitendea kazi, kuchelewa kukamilika kwa Mabadiliko ya Sheria ya Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji, kukosekana kwa mashirikiano kati yao na taasisi nyengine za Serikali katika suala zima la ukusanyaji mapato na udhibiti wa mazingira. Hali hii kwa ujumla inazipelekea taasisi hizi kutofanya kazi zao kwa ufanisi hususan katika suala la ukusanyaji wa kodi.

IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inavipongeza vikosi vyote vya SMZ kwa kazi kubwa wanazofanya kwa kusaidia ulinzi katika nchi yetu, lakini pia kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, kamati yetu inaikumbusha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa suala la nyongeza za mishahara katika

Vikosi vya SMZ bado ni tatizo kwa maana wapo walioongezwa, lakini nyongeza hiyo ni ndogo lakini nyongeza hizo hazikuzingatia muda wa mtu kuwepo kazini kwa maana mpiganaji mwenye cheo cha koplo ambaye amekipata cheo hicho leo hii, mshahara wake utakuwa sawa na koplo aliyedumu katika cheo hicho kwa miaka mingi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo ambalo ukweli limechangiwa na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kutekeleza majukumu ya kurekebisha mishahara ya vikosi na taasisi nyenginezo bila ya kuzishirikisha Tume za Utumishi za taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu bado inaisisitiza Serikali kufanya marekebisho hayo kwa kuwapatia wapiganaji wetu haki zao za msingi wanazozidai. Aidha, kamati inaishauri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwapatia "*salary slips*" mara baada ya kulipwa mishahara yao, ili kuepusha malalamiko miongoni mwa wapiganaji.

Kikosi cha Zima Moto na Uokozi

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inazipongeza kwa dhati kazi zinazotekelezwa na kikosi hiki. Aidha, kamati inakipongeza kikosi hiki kwa kupatiwa eneo la Mwanakwerekwe ili kiweze kutanua shughuli zake. Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla kikosi hiki kinafanya kazi kubwa usiku na mchana kwa lengo la kufanya uokozi wa aina mbali mbali. Hata hivyo, kikosi hiki kinakabiliwa na changamoto kadhaa, na miongoni mwa hizo ni ukosefu wa vitendea kazi, kutoshirikishwa na Idara ya Ardhi pamoja na jamii katika masuala ya ujenzi wa nyumba ili kiweze kutoa ushauri wake, kupewa mawasilano ya uongo na baadhi ya wananchi, hali ambayo inapelekea kupoteza mafuta ambayo nayo hayatoshelezi kwa matumizi ya kikosi. Changamoto nyengine kwa kikosi hiki ni kutokuwa na majengo katika maeneo ya Viwanja vya ndege na kupelekea kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu kwanza inaipongeza Serikali kwa kukiongezea kikosi hiki fungu la pesa kwa mwaka 2012/2013. Hata hivyo, kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kukifikiria kikosi hiki kadri inavyowezekana kwa kukipatia pesa zaidi ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.
Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaiomba Serikali kukiwezesha kikosi hiki kwa kukipatia majengo ya kudumu katika maeneo ya uwanja wa ndege, ili kiondokane na usumbufu uliopo.

Jeshi la Kujenga Uchumi (J. K.U)

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na kikosi hichi kwa kuendeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Lakini pia kikosi kinapongezwa kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa vijana wanaojitolea kupitia kikosi hichi ambao ni nguvu kazi ya taifa letu. Mbali na hayo kikosi kinakabiliwa na changamoto ikiwemo madeni wanayodaiwa na wafanyabiashara binafsi, ukosefu wa hati miliki katika maeneo yao, ukosefu wa umeme kwa baadhi ya kambi pamoja na vitendea kazi, huduma duni kwa vijana wanaojitolea katika kikosi na uhaba wa bajeti, hali ambayo inapelekea kukwama kwa baadhi ya malengo waliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaomba Serikali kukiangalia kikosi hichi kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba ya kamanda huko Pemba, kuimarisha mashamba yao kwa kuchimba visima kwa ajili ya umwagiliaji maji,pamoja na kuwafikiria vijana wanaojitolea kwa kuwaajiri inapotokezea nafasi za ajira, ili kuwatia moyo na wengine kuweza kujitolea.

Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo (K.M.K.M)

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa pongezi kwa kikosi cha KMKM kwa kujiimarisha kwa kukipatia wataalamu waliokuja kutoa mafunzo kwa ajili ya uokozi, pamoja na kuongeza vifaa vya kuzamia jambo ambalo litasaidia kuwa na nyenzo za kuokolea pale maafa yatakapotokea. Pia kikosi hiki kinakabiliwa na uchakavu wa majengo yake ambayo huwafanya baadhi ya askari wake kuishi katika mazingira magumu, kwenye majengo ambayo hayastahiki kuishi askari. Changamoto nyingine tulioiona ni kuwepo kwa rasilimali ya chelezo hapo Kibweni. Kamati yangu inaitaka Serikali kukitengeneza chelezo hichi ili kuongeza mapato, na pia kurahisisha matengenezo ya vyombo vyao. Kamati yangu bado inakitaka kikosi kuwa na kitengo cha kuzamia katika kisiwa cha Pemba ili kusaidia uokozi pindipo itakapotokea maafa. Changamoto nyingine ni upungufu wa mafuta ya kufanyia Doria kwani maumbile ya kazi yao ni kulinda baharini.

Idara ya Chuo Cha Mafunzo

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inathamini kazi zinazofanywa na Chuo cha Mafunzo. Hata hivyo, pamoja na kazi kubwa zinazotekelezwa na Chuo hiki, Chuo cha Mafunzo kinakabiliwa na changamoto kama vile kuwa na uhaba wa pesa zinazoingiziwa kwa ajili ya kuwahudumia wanafunzi. Hali hii husababisha Chuo kupata mzigo mkubwa kutokana na kuwepo kwa idadi kubwa ya mahabusu, ukilinganisha na idadi ya wanafunzi (wafungwa). Hivyo, tunaitaka Serikali kuongeza fungu hili ili kuweza kukidhi mahitaji ya chakula kwa wanafunzi na mahabusu. Pia kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Kikosi cha mafunzo kujenga magereza yanayokwenda na wakati, kwani haya yaliyopo yamepitwa na wakati na mazingira yake hayaridhishi kiafya. Pia tunaomba kujengwa majengo maalum ya watoto ili wasichanganywe na wanafunzi watu wazima,

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaiomba Serikali kupitia Chuo cha Mafunzo kuyafanyia ukarabati mkubwa majengo wanayoishi Askari Unguja na Pemba, kwani mengi yao yamezeeka na kuchakaa sana. Pamoja na hayo kamati yangu imepata malalamiko kutoka kwa baadhi ya Askari kuwa kuna baadhi yao wamepewa barua za uhamisho kutoka Pemba kuja Unguja lakini wanaambiwa wajitegemee kwa kuwa hakuna pesa za Uhamisho. Sasa Mhe Waziri, ukija hapa kutujibu tunaomba jawabu katika hilo.

Pia Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia ushauri wa kamati kuwa, Askari wote wa Vikosi vya SMZ wasilazimishwe kukatwa pesa katika mishahara yao bila ya kushauriwa kwani mshahara ni haki ya muajiriwa na inabidi kila atakachokatwa basi iwe ni lazima kwa mashauriano na muajiri wake, Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inaitaka serikali kupitia chuo cha mafunzo, kuwapeleka mawakili ili kwenda vyuo vya Mafunzo kuwasaidia wanafunzi kukata rufaa kwa wale wanaohitaji.

Kikosi cha Valantia, Zanzibar (KVZ)

Mhe. Mwenyekiti, Kamati vile vile inakipongeza kikosi hichi kwa kazi kubwa wanazozifanya hasa katika suala la kuimarisha ulinzi kwenye maeneo mbali mbali hapa nchini, lakini tunaomba uongozi wa kikosi hicho kwanza wao wenyewe viongozi wakuu, wawe na maelewano makubwa kwani bila ya mashirikiano yao, basi kikosi kitayumba. Kamati yetu pia inaitaka Serikali kumtafutia makaazi yanayostahiki Mkuu wa kikosi hiki kwa upande wa Pemba, kwani kumpatia chumba kimoja yeye na familia yake ni kumdhalilisha, kwa hiyo tunaomba suala hili lifanyiwe kazi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kusikitisha kabisa. Mhe. Mwenyekiti, nani kati yetu sisi anataka alale katika chumba kama hichi?

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nichukue fursa hii, nikushukuru kwa mara nyengine na niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba nitamke kwamba, kwa niaba ya Kamati yetu naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha hotuba hiyo, kwa heshima kubwa na kwa sababu na mimi sitopata nafasi ya kuchangia, naomba uniruhusu nichangie neno dogo tu katika hotuba ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu nimeuelekeza katika taasisi ya Baraza la Manispaa. Naamini Mhe. Waziri anafahamu kwamba Mhe. Ali sehemu ya damu yake basi ni Baraza la Manispaa. Hilo limetokana na kufanya kazi katika taasisi ile kwa muda mrefu, kwa vipindi viwili yaani miaka kumi.

Mhe. Mwenyekiti, katika taasisi hii mchango wangu zaidi unakuja katika kuangalia hali halisi za Waheshimiwa Madiwani. Tukitaka tusitake Mhe. Mwenyekiti, hali za madiwani wetu katika suala zima la kipato basi linasikitisha sana, pamoja na kwamba sheria imewapa uwezo kwa kupitia sheria zao za nambari 3 kwa Baraza la Manispaa nambari 4 kwa Halmashauri ya Miji, kujipangia posho pale wanapohisi kuna haja hiyo na kupata-*prove* kutoka kwa Mhe. Waziri. Lakini kutokana na suala zima la makushano, basi imekuwa suala la kujipangia posho zao imekuwa kuna unyeti.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kuangalia namna gani ya kuweza kuwanusuru madiwani, kwa sababu madiwani ni sehemu ya wana siasa kama sisi kama Wabunge au kama Wawakilishi. Hata sisi sote tulipokwenda katika hatua za kuomba kura, basi tunakuwa tunakwenda sambamba, sasa katika hali ya kimaslahi basi ningemuomba Mhe. Waziri kuangalia ni namna gani tunaweza kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu kwa upande wa Tanzania Bara, Mhe. Waziri Mkuu kule ameelezea kwa uwazi zaidi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa upande wa madiwani wa Tanzania Bara, ameamua kuwaongezea posho, ili waweze kujisaidia katika shughuli zao za kimaendeleo. Pia katika hotuba yake ameweza kutoa misamaha kwa magari au vyombo ambavyo watahitaji madiwani wale kutumia katika shughuli zao. Kwa hivyo, ningeomba na serikali yetu basi ikawaonea huruma madiwani katika angalau kuwasaidia katika suala zima la kuwaongezea uwezo kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, kwa bahati nzuri au mbaya, kuna tatizo dogo tu limejitokeza hivi karibuni, baina ya taasisi ya Baraza la Manispaa na Wizara yetu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika eneo la uwekezaji hapa karibu Mazizini. Kuna jengo la *Diplomatic Supermarket*. Mhe. Mwenyekiti, suala hili Waheshimiwa Madiwani wamelizungumzia kwa kina zaidi na upeo, na kwa sheria ambazo wao wenyewe kwa mamlaka kama Baraza la Manispaa, kukodisha mali zao, au kutumia hata rasilimali zao kwa vile sheria zinavyoongoza. Lakini suala hili Mhe. Mwenyekiti, linaonekana kidogo lina *istifham*.

Sasa swahiba wangu Mhe. Waziri kwa sababu naamini hili analifahamu na *document* ambazo zinaonekana zina mvutano baina ya Manispaa, aliyekodi na taasisi yetu hapajakaa vizuri. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kwa hekima zake na busara zake, akajaribu kuliangalia suala hili ili kulipa baraka, na ili ile *istifhamu* iliyotokezea, kuweza kuiondosha kwa haraka na kutenga imani baina ya serikali za mitaani na serikali kuu. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo, nakushukuru sana kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa zote mbili katika jioni hii, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti (Mhe. Mgeni Hassan Juma): Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji, ambaye umesoma hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana, kwa leo kutwa nzima mlikuwa na mimi, nawashukuru sana kwa mashirikiano mema. Kabla ya kuahirisha kuna tangazo moja linatoka kwa Mnadhimu wa CCM, anawaomba Wajumbe wote wa CCM, kesho siku ya Jumamosi kuhudhuria katika mkutano wa hadhara, katika tawi la CCM la Gulioni Jimbo la Rahaleo, saa 10:00. Mgeni rasmi atakuwa ni Makamo Mwenyekiti wa CCM Mhe. Aman Abeid Karume.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo tunaahirisha Baraza hili mpaka siku ya Jumatatu ya tarehe 02/07/2012, saa 3:00. Ahsanteni.

(Saa 2:00 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka

tarehe 02/07/2012 saa 3:00 za asubuhi)